# Nipashe

Jumanne Oktoba 29, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580061

www.ippmedia.com

The Guardian digital | nipasheTZ | nipasheTZ | nipasheTZ | 0745 700710




## Mfungwa aliyesamehewa adaiwa kuanzisha kikundi cha ujambazi

UKURASA 3


Nipashe TESA
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI
Wanasayansi wanachunguza jinsi saratani 'inavyozaliwa'
Mabadiliko ya tabianchi yatishia amani Somalia?
Ukoloni uliwadhalilisha mama wanene- Mhadhiri
Kahama yakabili changamoto zinazokwamisha wanafunzi wa kike

UKURASA 13

# Gari la 'washawasha' latumika kuzima moto

UKURASA 2




Gari la Jeshi la Polisi maalum kwa shughuli za kutuliza ghasia maarufu kama 'washawasha', likiwa kwenye eneo la tukio, baada ya nyumba ya Diwani wa Gongoni, kuwaka moto katika Mtaa wa Moshi mkoani Tabora juzi. **PICHA: MTANDAO**

Distributed via ippmedia




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play | App Store


## UCHAGUZI S/MITAA

# Jafo atoa maagizo 6 uchukuaji fomu

**AONYA** ukiukwaji wa kanuni, taratibu, kampeni kabla ya wakati...*Endelea ukurasa 2*

## IDADI YA VIFO VYA MAFURIKO YAONGEZEKA

UKURASA 3

**MICHEZO** YANGA: MSIMAMO HATIMA YA ZAHERA UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6

## HABARI KITAIFA

# Gari la washawasha latumika kuzima moto

**Na Halima Ikunji, TABORA**

KUTOKANA na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kukosa gari, Jeshi la Polisi mkoani Tabora limelazimika kutumia gari lake la maji ya kuwasha, kuzima moto kwenye nyumba ya Diwani wa Gongoni, Kessi Abdurahaman.

Tukio hilo lilitokea juzi saa tisa alasiri katika Mtaa wa Moshi, Kata ya Gongoni baada ya nyumba hiyo kushika moto, ikielezwa kuwa wakazi wa eneo hilo walitoa taarifa kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ambalo lilifika eneo la tukio na likiwa na gari dogo lisilokuwa na maji na kuahidi kupeleka gari kubwa.

Mliasanza Isiaka, mmoja wa mashuhuda wa tukio hilo, alisema moto huo ulianza majira ya saa 9:15 alasiri katika moja ya vyumba vya wapangaji katika nyumba hiyo.

Alidai wapangaji hao walitoa taarifa kwa jeshi hilo na kwamba robo saa baadaye, Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, alifika eneo la tukio na kusaidiana na wananchi kuzima moto huo wakitumia maji na matawi ya miti.

Shuhuda huyo alidai kuwa majira ya saa 10 jioni, aliona gari la maji ya kuwasha la Kikosi cha Kutulia Ghasia (FFU) cha Jeshi la Polisi lilifika eneo la tukio na kutumika kuzima moto huo.

Alidai kuwa pamoja na kufanikiwa kuuzima moto huo, karibu vitu vyote vilivyokuwa ndani ya nyumba hiyo viliteketea. Ilielezwa kuwa nyumba hiyo ilikuwa inatumiwa na familia nne.

"Karibu kila kitu kwenye ile nyumba kilikuwa kimeteketea kwa moto isipokuwa kitanda, godoro na kabati kutoka katika chumba cha mpangaji mmoja ambaye chumba chake kilikuwa mwisho.

Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji mkoani Tabora, Peter Mabusi, akizungumza na Nipashe jana ofisini kuhusu tukio hilo, alisema gari la kuzima moto katika Manispaa ya Tabora ni bovu kwa muda mrefu na linafanyiwa matengenezo makubwa.

Alidai matengenezo hayo yanatarajiwa kukamilika baada ya wiki moja au mbili kuanzia jana.

Mabusi alisema kuwa kwa sasa wanatumia njia nyingine mbadala kukabiliana na majanga ya moto ikiwa ni pamoja na kutumia magari ya Jeshi la Polisi.

Katika hatua nyingine, Kamanda Mabusi aliwataka wakazi wanaoishi katika maeneo ya mabondeni na wanaofanya shughuli za uchimbaji madini, kuchukua tahadhari ya kukumbwa na mafuriko katika msimu huu wa mvua.

Alibainisha kuwa katika kipindi cha kuanzia Julai mwaka jana hadi sasa, mkoa wake ulikuwa na matukio ya moto zaidi ya 200 na kwamba katika kipindi cha kuanzia Juni mwaka huu pekee, kuna matukio 50 ya moto.

Alisema taratibu zinawataka kuhakikisha kuwa katika kila eneo la mji wenye wakazi kati ya 200,000 hadi 300,000, kuwe na Kituo cha Zimamoto na Uokoaji chenye kikosi kazi na magari ya kutolea huduma pindi yanapotokea majanga mbalimbali.

Alisema serikali inaendelea na jitihada za kuongeza magari ili kuboresha huduma katika mkoa wake huo.



Rais John Magufuli akipokea hati ya utambulisho toka kwa Balozi mteule wa Umoja wa Ulaya (EU) nchini, Manfredo Fanti, katika hafla fupi iliyofanyika, Ikulu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Jafo atoa maagizo sita uchukuaji fomu

**Na Waandishi Wetu**

UCHUKUAJI na urejeshaji fomu kwa ajili ya kuwania nafasi mbalimbali za uongozi kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa, unaanza leo, huku serikali ikitoa maagizo sita kuhusu uzingatiaji kanuni katika mchakato huo.

Uchaguzi huo utafanyika Novemba 24, mwaka huu na nafasi zinazogombewa ni Mwenyekiti wa Kitongoji, katika Mamlaka za Miji Midogo, Mwenyekiti wa Mtaa na wajumbe wa Kamati ya Mtaa (Kundi mchanganyiko la wanawake na wanaume) na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa (kundi la wanawake) katika Mamlaka za Miji.

Nyingine ni Mwenyekiti wa Kijiji, wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji (Kundi mchanganyiko la wanawake na wanaume), Wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji (kundi la wanawake) na Wenyeviti wa Vitongoji katika Mamlaka za Wilaya.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, alisema uchukuaji na urejeshaji wa fomu utafanyika kwa siku saba ambao utaanza leo hadi Novemba 4, mwaka huu.

Alieleza kuwa fomu hizo zinapatikana kwa wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi kwenye ofisi za watendaji wa vijiji na mitaa.

Kutokuwa na muingiliano

Aliwataka wasimamizi wa uchaguzi kuhakikisha utoaji fomu hauingiliani na changamoto ya aina yeyote kama walivyopewa maelekezo.

"Watanzania wenye nia ya kushika nafasi mbalimbali kwenye mamlaka za serikali za mitaa huu ni muda mwafaka wa kufanya hivyo kupitia vyama vyao vya siasa vyenye usajili wa kudumu, ni kipindi muhimu watu wazingatie kanuni,"alisema.

Aliwasisitiza kusimamia kanuni katika mchakato mzima wa kuchukua na kurejesha fomu.

**KUSIMAMIA DEMOKRASIA**

Aidha, Jafo aliwataka wasimamizi wa uchaguzi kuhakikisha kila mwananchi anapata haki yake ya kidemokrasia kama ambavyo serikali inakusudia.

"Kumekuwapo na utulivu kila mahali, watu wanaotaka ufafanuzi... wamekuwa wakituma barua na tunatoa ufafanuzi, lengo letu ni kuhakikisha kila mtu anashiriki katika uchaguzi huu bila kukwazwa na jambo lolote," alisema.

Waziri huyo alisema serikali inataka kuona kila Mtanzania anapata haki yake ya msingi ya kutimiza matakwa ya kidemokrasia.

INAENDELEA UK 8

# Mabalozi wapya watangaza neema

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli jana alipokea hati za utambulisho za mabalozi wa Umoja wa Ulaya (EU), Manfred Fanti, wa Finland, Riitta Swan na wa Rwanda nchini, Meja Jenerali Charles Karamba, Ikulu jijini Dar es Salaam.

Wakizungumza baada ya kuwasilisha hati zao kwa nyakati tofauti, mabalozi hao wapya walitoa kauli za matumaini na manufaa kwa nchi zao na Tanzania.

Akizungumza baada ya kuwasilisha hati zake za utambulisho, Balozi Fanti aliishukuru Tanzania kwa kumpokea kuiwakilisha EU nchini na kwamba katika kuendeleza na kukuza zaidi uhusiano na ushirikiano na EU na Tanzania, atajielekeza zaidi katika masuala ya maendeleo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu, Balozi Fanti anaamini kuna mambo mengi na mazuri ya kufanya yatakayoiwezesha Tanzania kuingia katika uchumi wa kati kama ilivyopanga.

Aliongeza kuwa anaamini katika mazungumzo ya pamoja kati ya Tanzania na EU katika masuala mbalimbali na kwamba katika kipindi chake anatarajia kutilia mkazo miradi ya kuzalisha nishati ya umeme kupitia Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) na utekelezaji wa miradi mingine iliyoko katika makubaliano ya 11 ya mkataba wa mfuko wa maendeleo wa EU uliotengewa Sh. trilioni 1.583.

Rais Magufuli alimpongeza mwakilishi huyo kwa msimamo wake wa kuimarisha na kukuza zaidi uhusiano wa Tanzania na EU.

Alisema Tanzania inatambua uhusiano mzuri na wa kihistoria uliopo kati yake na EU na kwamba iko tayari kushirikiana na balozi huyo katika utekelezaji wa masuala yenye maslahi kwa pande zote mbili.

Naye Balozi Swan pamoja na kushukuru kwa kupokewa, alimpongeza Rais Magufuli kwa mafanikio makubwa katika kupambana na rushwa na akasema katika kipindi chake nchini atahakikisha maeneo ya uhusiano kati ya Tanzania na Finland yanaimarishwa ikiwamo mradi wa utunzaji wa mazingira, kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa kodi kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na utawala bora.

Rais Magufuli, kwa mujibu wa taarifa hiyo, alimshukuru kwa dhamira yake ya kukuza zaidi ushirikiano na uhusiano na Tanzania na kwamba

INAENDELEA UK 8

## HABARI KITAIFA



Baadhi ya wafanyakazi wa Hospitali ya Aga Khan, wakiwa wamekusanyika nje ya hospitali hiyo jijini Dar es Salaam jana, baada ya kutokea moto uliowaka katika jengo la duka la dawa za wagonjwa wa nje. Hakuna athari zilizotokea kwa wagonjwa, ndugu wa wagonjwa na wafanyakazi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mfungwa aliyesamehewa adaiwa kuunda kikosi kupora bodaboda

**Na Romana Mallya**

MFUNGWA aliyetoka gerezani kwa msamaha wa parole (jina linahifadhiwa), anatafutwa na polisi mkoani Kagera baada ya kudaiwa kuunda kikundi cha uporaji pikipiki.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera, Revocatus Malimi, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Malimi alisema mtu huyo baada ya kushtuka anatafutwa, amekuwa akijificha mpakani na wakati mwingine kukimbilia nchi jirani.

Kamanda Malimi alisema katika kipindi cha Septemba 11 hadi Oktoba 20, mwaka huu, kwa nyakati tofauti mkoani humo, kumejitokeza matukio ya wizi wa pikipiki. Alisema wahusika wa matukio hayo wamekuwa wakiwafuata madereva na kuwakodi na wakifika mbele huwapora.

Distributed via ippmedia

"Tulipata taarifa kuwa kuna kikundi kinajihusisha na wizi wa bodaboda kimeanzishwa na mtu mmoja jina limehifadhiwa ambaye alitoka gerezani kwa msamaha wa parole, ambaye amekiunda mahususi kwa ajili ya uporaji pikipiki.

"Taarifa zake tunazo, ameshatoroka, anakaa upande wa mpakani na wakati mwingine anakwenda nchi jirani. Tulifanya msako na tumekamata wezi wawili wa pikipiki ambao ni Hamdani Msandiku (27), Godwin Julius (31). Tumekamata pikipiki nne kwenye msako huo ambazo tunaamini ni sehemu ya zile zilizoibiwa," alisema.

Kamanda Malimi aliwaomba wale wote walioripoti kuibiwa pikipiki zao waende kituoni hapo ili kuzitambua.


**bgtl BEST GROUP (T) LIMITED**

Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

Under the Instruction from **AFRICAN BANKING CORPORATION TANZANIA LTD (Banc ABC),** we shall sale by Public auction the Legal Mortgage Securities which are Commercial/Residential properties. The public auction will be conducted from 09:00 am where the properties located as indicated below.

| s/n | DEBTOR/GUARANTER | LOCATION/DESCRIPTION OF THE PROPERTY | DATE OF AUCTION |
|---|---|---|---|
| 1 | SIX TELECOMS COMPANY LIMITED | Legal Mortgage over a property located on Plot No 97, Block "S", L.O No 83937 with Certificate of Title No. 033025/82. I.N.O PEM LIMITED. Situated at Nkomo Street, Mwanza Municipality. | 16/11/2019 |

**CONDITION FOR THE AUCTION**

1. Once the bidder has accepted he or she has to make payment of 25% of the bid price on the same day of auction. The remaining balance of 75% shall be paid within 14 days from the date of acceptance.
2. Failure to settle the remaining balance within 14 days shall resettle to forfeiture of 25% advance payment and properties we will re-auction. Or will give for the second bidder.
3. All expenses and costs in respect of inspecting the property and any other expenses incidental thereof shall be borne by the purchaser.

**For more Details Please Contact:**
**Managing Director**
**Best group(T) LTD**
**Alli Hassan Mwinyi Road.**
**Green Acres Building, 2nd Floor.**
**P.O BOX 1088**
**DAR ES SALAAM**
**MOBILE +255 715 363537/+255 765 363537**
**Email: info@bestgroup.co.tz**

**OR**

**MANAGING DIRECTOR,**
**Banc ABC,**
**Head House,**
**Bibi Titi Mohammed Road,**
**P.O BOX 31**
**DAR ES SALAAM**
**Tel: +255 22 2119422**
**+255 22 2112402**

215484702



**bgtl BEST GROUP (T) LIMITED**

Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

**Bank of Africa Tanzania Limited** inatoa notisi na tangazo la mnada wa hadhara kwa mdaiwa tajwa hapa chini kwenye jedwali. Benki inatoa wito kwa mteja wake kwamba afanye malipo ya mkopo wake kama yanavyojieleza kwenye akaunti yake, na endapo hatafanya hivyo benki itaendelea na kuuza dhamana zake kwa kupitia madalali kwa mnada wa hadhara baada ya siku 14 baada ya tangazo hili. Tafadhali wasiliana na Bank of Africa Limited kwa maelezo Zaidi.

| Na | JINA LA MDAIWA/MDHAMINI | DHAMANA/MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1 | HAPPINESS YESAYA MADANKA | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOSAJILIWA KWA HATI NA. 11568, OFISI YA ARDHI NA. 163368, KIWANJA NA. 8, KITALU "F", ILIYOPO MANISPAA YA MWANZA. ILIYOPO KWA JINA EMMANUEL ZEPHANIA MKUBWA | 15/11/2019 |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hiyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

215484702

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:**
**Mkurugezi Mtendaji**
**Best Group (T) LTD**
**Alli Hassan Mwinyi Road.**
**Green Acres Buliding, 2nd Floor.**
**P.O. BOX 1088**
**DAR ES SALAAM**
**MOBILE + 255 715-363537/ +255 765-363537**

**AU**

**Mkurugezi Mtendaji**
**BOA Bank**
**Head Office,**
**Ohio Street/Kivukoni Front,**
**P.O. BOX 3054,**
**DAR ES SALAAM**
**Tel: +255 22 2110104**
**+255 22 2111290**


## Vifo vya maji vyaongezeka Tanga

**Na Boniface Gideon, HANDENI**

WATU 15 wamepoteza maisha mkoani Tanga kwa muda wa siku tatu kufuatia mvua zinazoendelea kunyesha maeneo mbalimbali nchini.

Pia, Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) limeanza kujenga madaraja ya muda kwenye maeneo ambayo yalisombwa kwa maji na kukata mawasiliano ya pande zote.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Edward Bukombe, alisema kazi inayoendelea kwa sasa ni kurejesha mawasiliano ya barabara kwenye maeneo yaliyoharibiwa na mafuriko.

Alisema madaraja ya muda yanajengwa kwenye barabara inayonganisha Handeni na Kilindi, daraja la Nderema pamoja na daraja la Kidereko linalounganisha Handeni hadi Turiani mkoani Morogoro.

Kwa mujibu wa Kamanda huyo, abiria waliokuwa wamekwama kwenye eneo la Korogwe kutokana na daraja la Mandera kujaa maji, wameanza kupita baada ya maji kupungua.

Alisema barabara iliyokuwa mbadala wa Dar es Salaam kwenda mikoa ya Kaskazini ilikosa mawasiliano baada ya daraja la Mandera kusombwa na maji.

"Daraja la Korogwe liko salama, lakini kuna mahali limemomonyoka kutokana na mvua, kwa sasa kazi kubwa inayofanyika ni kujaza kifusi ili kuliimarisha zaidi maeneo yaliyoharibiwa," alisema.

Kamanda Bukombe aliwataka wananchi na watumiaji wote wa barabara hizo kuwa na tahadhari ikiwamo kuacha kupita kwenye madaraja yakiwa na maji mengi kama ilivyotokea kwa gari iliyotumbukia mtoni na kuua watu kumi.

Mkuu wa mkoa wa Tanga, Martine Shigela, akizungumza na gazeti hili kuhusiana na ujenzi huo, alisema utafanyika kwa wiki moja na kuwataka wananchi kuwa wavumilivu.

Naye, Mwenyekiti wa halmashauri ya Handeni mjini, Twaha Mgaya, akizungumzia madhara kwenye wilaya hiyo, alisema daraja la Sindeni na Komsala ambayo yanaunganisha wilaya za Handeni na Korogwe nalo liliharibika.

Vile vile, daraja la Magamba linalounganisha wilaya hiyo na mikoa ya Pwani na Morogoro limeathirika kwa nyufa.

# Atozwa mil. 26/- kukutwa na dizeli bila kulipiwa kodi

**Na Halima Ikunji, TABORA**

MFANYABIASHARA wa mafuta ya dizeli, ametozwa faini ya Sh. milioni 26, baada ya kukutwa na mafuta hayo wilayani Igunga Mkoa wa Tabora.

Mfanyabiashara huyo alikamatwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya wilaya ya Igunga kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) akiwa na lita 17,800 zenye thamani ya Sh. milioni 38.8.

Imeelezwa na Mkuu wa wilaya hiyo, John Mwaipopo, kuwa alikutwa na mafuta hayo kwenye gari aina ya Scania bila kuwa na nyaraka zozote zinazoonyesha kama yamelipiwa kodi.

Mwaipopo alisema lori hilo lilikutwa katika Kijiji cha Igogo Kata ya Nanga.

Alisema mwishoni mwa wiki alipokea taarifa za siri kutoka kwa raia mwema kuwa kuna lori la mafuta ya dizeli aina ya Scania kuwa wana shaka nalo.

Mwaipopo alisema baada ya kupata taarifa hizo aliitaarifu Kamati ya Ulinzi na Usalama ambapo walimtaarifu pia Kaimu Meneja wa TRA Igunga, Gabinas Ntabalizi, ambao wote walikwenda eneo hilo na kukuta lori hilo.

Kwa upande wake Ntambalizi alimtaja mmiliki wa lori hilo ni Bundala Kapela, mkazi wa Kata ya Nyandekwa Wilaya ya Igunga, na kuwa alipotakiwa kuonyesha nyaraka za mafuta hayo hakuwa nazo.

Meneja huyo wa TRA aliongeza kuwa alitozwa faini ya Sh. milioni 26, huku akisema kati ya fedha hizo, Sh. milioni 23 ni kodi aliyokuwa akidaiwa.

Kwa mujibu wa Ntambalizi, Sh. milioni 3 ni faini ya kuwazuia maofisa wa serikali kutotekeleza majukumu yao kutokana na mfanyabiashara huyo kutotoa ushirikiano.

Hata hivyo, alisema mfanyabiashara huyo alilipa fedha zote na kukabidhiwa gari lake.

Mkuu wa wilaya Mwaipopo aliwataka wafanyabiashara wenye tabia ya kukwepa kulipa mapato ya serikali kuacha mara moja na badala yake wawe wazalendo wa kupenda nchi yao kwani fedha wanazolipa ndizo zinafanya maendeleo ya nchi ikiwamo ujenzi wa miundombinu ya barabara, hospitali, huduma za maji na mambo mengine mengi.




Wananchi wakisaidia kukusanya maziwa yaliyomwagika barabarani kutoka kwenye gari ndogo la kubebea bidhaa hiyo, katika Barabara ya Chang'ombe, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

Distributed via ippmedia




# Watumishi waliopanda kulipwa mishahara mipya

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

SERIKALI imezitaka wizara na taasisi zote kuhakikisha zinawalipa mishahara pamoja na stahili zote watumishi ambao wamepandishwa madaraja kulingana na nafasi walizo nazo sasa kwa mujibu wa miongozo iliyopo ya utumishi wa Umma.

Agizo hilo lilitolewa jana jiji hapa na Waziri wa Nchi ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora), George Mkuchika, alipokuwa akizindua na kufungua mkutano wa Baraza Kuu la Nne la wafanyakazi katika utumishi wa Umma.

Mkuchika alisema kumekuwa na malalamiko katika maeneo mbalimbali nchini kuwa watumishi ambao serikali ilitoa maagizo kuwa wapandishwe madaraja mishara yao imebaki kama ilivyokuwa awali.

"Hivi karibuni nilikuwa mkoani Ruvuma huko pia nimekutana na malalamiko ya kutosha, kila mtumishi analalamika kuwa kapanda daraja, lakini mshahara bado haujapanda," alisema Mkuchika.

Alisema kutokana na hali hiyo viongozi wa serikali wanaohusika na suala hilo wanatakiwa kuhakikisha kuwa wanalifanyia kazi ili kuwapatia stahili zao watumishi wote waliopanda madaraja.

Pia aliagiza katika upandishaji wa madaraja kwa watumishi wapewe nafasi ya upendeleo wale ambao wanakaribia kustaafu.

"Serikali ilitangaza upandishaji wa madaraja kwa wenye sifa, lakini pia wanaotakiwa kupatiwa kipaumbele ni wale ambao wanakaribia kustaafu katika utumishi wa Umma ili waweze kupata stahiki ambazo zitawawezesha kujikimu kule wanakokwenda," alisema Mkuchika.

Alisema Novemba 1, mwaka 2017 serikali iliidhinisha watumishi wapatao 85,000 waliokasimiwa katika bajeti ya mwaka 2015/16 kupandishwa vyeo.

"Aidha awamu nyingine ya upandishaji wa vyeo imefanyika Mei 1, 2019 ambapo watumishi 193,166 waliokasimiwa katika bajeti ya mwaka 2017/18 wamepandishwa vyeo," alifafanua Waziri Mkuchika.

Mkuchika pia aliwapongeza watumishi wote wa Umma ambao wamekuwa mstari wa mbele katika kukusanya na kusimamia mapato ya serikali ambayo yanatumika katika kuboresha miundombinu mbalimbali.

"Niwapongeze sana watumishi kwani nyie ndiyo mmekuwa mkikusanya haya mapato ya serikali kwa kiasi kirefu kwani hapo zamani kabla ya hii awamu ya tano tulikuwa tukikusanya kwa mwezi kiasi cha Sh. bilioni 800, lakini sasa imefikia hadi Sh. trioni 1.7 kwa mwezi kiasi ambacho tunatakiwa kushikilia hapo hapo,"alisema

Vilevile, Mkuchika aliwataka watumishi wa Umma waliopo chini ya Ofisi ya Rais Utumishi na utawala Bora, kuhakikisha wanakuwa wa mfano katika suala la kupinga rushwa na kufanya kazi kwa uadilifu bila ya kuchagua maeneo ya kwenda kufanya kazi.

"Rushwa katika ofisi za Umma imekuwa kikwazo kwa wananchi wetu tunaowatumikia... naomba katika ofisi yangu watumishi wangu muwe watu wa mfano ambao mtakuwa hamjihusishi na rushwa hata kidogo ili kuakisi jina la utawala bora," alisema.

Akitoa neno la shukrani kwa mgeni rasmi Makamu Mwenyekiti wa Baraza hilo, Leah Ulaya, alisema moja kati ya changamoto ambazo zimekuwa kero kwa watumishi ni upandishwaji wa madaraja bila kuzingatia stahiki nyingine ikiwamo mishahara.

"Tunakuomba mheshimiwa waziri suala hili lifanyiwe kazi ili sisi watumishi ambao tumepata fursa ya kupanda madaraja tuweze kupata stahiki zetu kulingana na miongozo ya utumishi wa Umma," alisema Ulaya.

# TANGAZO

China Commercial Bank
中國商業銀行

## Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA, 2019
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka ya /Mwaka wa sasa 30.09.2019 | Robo Mwaka/Mwaka uliopita 30.06.2019 |
|---|---|---|---|
| **A. MALI** | | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 299 | 432 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 1,758 | 3,000 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 3,000 | 3,000 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 172 | 52 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | (8) | 22 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | 0 | 0 |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0 | 0 |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 1,000 | 1,466 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0 | 0 |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 685 | 477 |
| 12 | Mali Nyingine | 950 | 1,078 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 0 | 0 |
| 14 | Akaunti za udhamini | 0 | 0 |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 42 | 71 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **7,899** | **9,598** |
| **B.DHIMA** | | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 0 | 0 |
| 18 | Amana za Wateja | 704 | 1,485 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| 20 | Amana Maalumu | 0 | 0 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 0 | 0 |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 0 | 0 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 196 | 182 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 0 | 0 |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 117 | 167 |
| 27 | Dhima Nyingine | 348 | 1,477 |
| 28 | Madeni | 0 | 0 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **1,366** | **3,311** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI** ***(16 kutoa 29)*** | **6,532** | **6,287** |
| **C. FEDHA ZA WANAHISA** | | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 20,881 | 20,881 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 115 | 5 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (13,615) | (13,701) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (848) | (1,008) |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 0 | 110 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0 | 0 |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **6,532** | **6,287** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 1,272 | 8,560 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 86 | 328 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 86 | 275 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 3,000 | 4,630 |
| **D.BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 83% | 66% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 11% | 44% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 110% | 51% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 9% | 5% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 59% | 52% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -53% | -14% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -18% | -10% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30 SEPTEMBA, 2019
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo ya mwaka sasa 30-Sep-19 | Robo ya mwaka linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Sep-18 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-19 | Limbikizo la mwaka linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Sep-18 |
|---|---|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 256 | 235 | 424 | 1,121 |
| 2 Gharama za Riba | 0 | (23) | 0 | (314) |
| **3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **256** | **212** | **424** | **808** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | - | | - | |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 303 | (649) | 102 | (649) |
| 6 **Mapato Yasiyo ya Riba**: | **137** | **144** | **419** | **325** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha | 4 | 19 | 13 | 30 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 128 | 104 | 395 | 277 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | 5 | 20 | 12 | 19 |
| 7 **Gharama Zisizo za Riba:** | **(535)** | **(860)** | **(1,793)** | **(2,894)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 159 | 176 | 496 | 670 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 31 | 44 | 67 | 252 |
| 7.3 Gharama Nyingine | 345 | 640 | 1,229 | 1,972 |
| 8 **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **160** | **(1,153)** | **(848)** | **(2,410)** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 10 **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **160** | **(1,153)** | **(848)** | **(2,410)** |
| 11 Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | 0 | 0 | 0 | 0 |
| 12 **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **160** | **(1,153)** | **(848)** | **(2,410)** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 17 | 20 | 17 | 20 |
| 14 Mapato kwa Hisa | 246 | (662) | (1,299) | (2,269) |
| 15 Idadi ya Matawi | 1 | 1 | 1 | 1 |
| **Baadhi ya viashirio vya Ufanisi** | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 2% | -2% | -9% | -4% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 3% | -2% | -13% | -5% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 136% | -227% | 213% | -200% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 5% | 1% | 9% | 2% |

**Tarakimu za wastani zitakokotolewa kwa kujumlisha salio la mwisho kwa miezi inayohusika katika kipindi na kugawanya kwa idadi ya miezi katika kipindi hicho.**

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 SEPTEMBA, 2019
(Kiasi kwa shilingi milioni)

Tengo la Ziada ya

* Salio la mwisho wa Robo mwaka Iliyopita

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Robo Mwaka ya sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa Robo mwaka** | **20,881** | **-** | **(14,709)** | **110** | **5** | **-** | **6,287** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 160 | - | - | - | **160** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | 85 | - | - | | **85** |
| **Salio la mwisho wa Robo mwaka ya sasa** | **20,881** | **-** | **(14,464)** | **110** | **5** | **-** | **6,532** |
| **Robo Mwaka iliyopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa Robo mwaka** | **20,881** | **-** | **(14,256)** | **110** | **5** | **-** | **6,740** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (453) | - | - | - | **(453)** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa Robo mwaka Iliyopita** | **20,881** | **-** | **(14,709)** | **110** | **5** | **-** | **6,287** |

Distributed via ippmedia

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA
### KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 30 SEPTEMBA, 2019
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Robo Mwaka ya sasa 30-Sep-19 | Robo Mwaka iliyopita 30-Jun-19 | Limbikizo la mwaka wa sasa 30-Sep-19 | Limbikizo la Mwaka linganishi (Mwaka Uliopita) 30-Sep-18 |
|---|---|---|---|---|
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 160 | (453) | (848) | (2,436) |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | 0 |
| - Hasara Katika Mali | (93) | 293 | 498 | 1,178 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 561 | (26) | 551 | 550 |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | 0 | (4) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (781) | (236) | (3,285) | (12,559) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | 0 | 4,056 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (1,164) | (381) | (1,551) | 588 |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 62 | 84 | 322 | (373) |
| - Kodi Iliyolipwa | - | (9) | (9) | 0 |
| - Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(1,255)** | **(728)** | **(4,322)** | **(9,000)** |
| **II: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | 0 | (1) | (8) | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | 15 |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | (1,500) | (1,500) | (1,500) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **0** | **(1,501)** | **(1,508)** | **(1,485)** |
| **III: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | - | - | - | - |
| **IV: Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (1,254) | (2,229) | (5,830) | (10,485) |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 3,299 | 5,529 | 7,875 | 18,374 |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka** | **2,045** | **3,299** | **2,045** | **7,889** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA, 2019

Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| Jina | Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|---|
| Xiong Zhenglin | Ofisa Mtendaji Mkuu | ................................ | **28.10.2019** |
| Fadhili Sanga | Mkuu wa Fedha | ................................ | **28.10.2019** |
| Victoria Edward | Mkaguzi Mkuu wa Ndani | ................................... | **28.10.2019** |

Sisi tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa Taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathimini taarifa hizi,na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa vya uwasilishaji wa Taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya Benki na Taasisi za fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi

| Jina | Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|---|
| Liu Lin | Mwenyekiti wa bodi | ................................ | **28.10.2019** |
| Chao Jiang | Mjumbe wa bodi | ................................ | **28.10.2019** |

## The Banking and Financial Institutions (Disclosures) Regulations, 2014
## MINIMUM DISCLOSURES OF CHARGES AND FEES
## (Made under Regulation 11)

| No. | ITEM/TRANSACTION | CHARGE/FEE | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | **Current Accounts** | **TZS** | | **USD** | |
| | (a) Required minimum opening balance | | | | |
| | Personal Current Account | TZS | 100,000.00 | $ | 100.00 |
| | Business Account | TZS | 200,000.00 | $ | 200.00 |
| | Imperial Business Account | TZS | 5,000,000.00 | $ | 5,000.00 |
| | Community Account | TZS | 200,000.00 | $ | 200.00 |
| | Call Account | TZS | 10,000,000.00 | $ | 10,000.00 |
| | (b) Monthly service fee (break down per customer type) | | | | |
| | Personal Current Account | TZS | 12,980.00 | $ | 12.98 |
| | Business Account | TZS | 12,980.00 | $ | 12.98 |
| | Imperial Business Account | TZS | 25,960.00 | $ | 25.96 |
| | Community Account | Free | | Free | |
| | Call Account | Free | | Free | |
| | (c) Cheque withdrawal over the counter | TZS | 1,947.00 | 0.75% of withdrawal amount | |
| | (d) Fees per ATM Withdrawal | | | | |
| | Personal Savings (5 free withdrawals per month) | TZS | 1,300.00 | $ | - |
| | Imperial Savings (5 free withdrawals per month) | TZS | 1,300.00 | $ | - |
| | Student Boom Account | TZS | - | $ | - |
| | Junior Savings Account | TZS | - | $ | - |
| | Senior Savings Account (3 free withdrawals per month) | TZS | 1,300.00 | $ | - |
| | Personal Current Account | TZS | 1,300.00 | $ | - |
| | (e) ATM mini statement | TZS | 300.00 | $ | - |
| | (f) Interim statement (Below 3 months) | TZS | 3,894.00 | $ | 2.60 |
| | (g) Periodic scheduled statement | Free | | Free | |
| | (h) Cheque book (per leaf) | TZS | 519.20 | $ | 0.52 |
| | (i) Dishonoured Cheque | | | | |
| | Inward Unpaid Cheque | TZS | 12,980.00 | $ | 12.98 |
| | Outward Unpaid Cheque | TZS | 38,940.00 | $ | 38.94 |
| | (j) Special clearance | | | | |
| | Personal Accounts | TZS | 51,920.00 | $ | 51.92 |
| | Business Accounts | TZS | 64,900.00 | $ | 64.90 |
| | (k) Counter cheque (per leaf) | TZS | 12,980.00 | $ | 12.98 |
| | (l) Stop payment (per leaf) | TZS | 12,980.00 | $ | 12.98 |
| | (m) Standing order | | | | |
| | Internal | Free | | Free | |
| | External | TZS | 12,980.00 | $ | 12.98 |
| | Unpaid | TZS | 6,490.00 | $ | 6.49 |
| | (n) Balance enquiry | Free | | Free | |
| | (o) New ATM card issuance | Free | | Free | |
| | (p) ATM card renewal or replacement | TZS | 12,980.00 | $ | - |
| | (q) Overdrawn Account interest charge | 10% above the Banks Base Lending Rate | | | |
| | (r) Unarranged overdraft | 10% above the Banks Base Lending Rate | | | |
| | (s) Interbank transfer | TZS | 12,980.00 | $ | 12.98 |
| | (t) Bill payments through ATM | TZS | 713.90 | $ | - |
| | (u) Deposit fee | Free | | Free | |
| | (v) Other (please specify) | | | | |
| | ATM withdrawal limit per transaction | TZS | 400,000.00 | $ | - |
| | ATM withdrawal daily limit | TZS | 1,000,000.00 | $ | - |
| 2 | **Savings Accounts** | | | | |
| | (a) Required minimum opening balance | | | | |
| | Personal Savings Account | TZS | 50,000.00 | $ | 50.00 |
| | Student Boom | TZS | 20,000.00 | $ | 20.00 |
| | Senior Savings Account | TZS | 50,000.00 | $ | 50.00 |
| | Joint Savings Account | TZS | 50,000.00 | $ | 50.00 |
| | Imperial Savings Account | TZS | 2,000,000.00 | $ | 2,000.00 |
| | Junior Savings Account | TZS | 10,000.00 | $ | 10.00 |
| | (b) Monthly service fee | | | | |
| | Personal Savings Account | TZS | 9,086.00 | $ | 9.09 |
| | Student Boom | Free | | Free | |
| | Senior Savings Account | TZS | 9,086.00 | $ | 9,086.00 |
| | Joint Savings Account | TZS | 9,086.00 | $ | 9,086.00 |
| | Imperial Savings Account | TZS | 19,470.00 | $ | 19.47 |
| | - Imperial Savings Account | TZS | - | $ | - |
| | - Imperial Savings Account | TZS | - | $ | - |
| | - Junior Savings Account | TZS | - | $ | - |
| | (e) Deposit rate (Personal savings accounts) | | 2.5% | $ | 0.01 |
| 3 | **Electronic Banking** | | Free | | Free |
| | (a) Internet Banking monthly fee | | FREE | | FREE |
| | (b) Internet transfers | | FREE | | FREE |
| | (c )SMS Banking | | NA | | NA |
| | (d) Other | | | | |
| | E-Banking Statement request(Self downloaded) | | FREE | | FREE |
| | E-Banking Password resetting | | FREE | | FREE |
| | E-Banking Statement request (printed by the Bank) per page | | TZS 1,298 | | $1.298 |
| 4 | **Foreign Exchange Transaction** | | | | |
| | (a) Purchase/sale of TCs transactions over the counter | | - | | - |
| | (b) Purchase of foreign cheque | | - | | - |
| | (c) Sale/Purchase of cash passport | | - | | - |
| | (d) Telegraphic Transfer (TISS/RTGS) | | | | |
| | Outward TT | TZS | 12,980.00 | $ | 12.98 |
| | Inward TT | | Free | | Free |
| | (e) Telex/Swift | | | | |
| | Outward TT | | | $ | 64.90 |
| | Inward TT | | | $ | 12.98 |
| | (f) Transfer from foreign currency denominated Account to local current Account ( within bank and to other bank) | | - | | - |
| 5 | **Loans** | | | | |
| | (a) Processing/Arrangement/Appraisal fee | | | | |
| | (i) Personal loans | 2% of the facility amount | | | |
| | (ii) Overdrafts | 2% of the facility amount | | | |
| | (iii) Mortgage finance | 2% of the facility amount | | | |
| | (iv) Asset finance | 2% of the facility amount | | | |
| | (b) Unpaid loan instalment | 10% above interest rate | | | |
| | (c) Early repayment | 3% of amount to be settled early | | | |
| | (d) Valuation fees | As per service provider rates | | | |
| | (e) Legal Fees | As per service provider rates | | | |
| | (f) Base Lending Rates | | 21% | $ | 0.09 |
| | (g) Maximum Spread Above the Base Lending Rate (BLR) | | 5% | $ | 0.05 |

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| | Name | Signature | Designation | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Xiong Zhenglin | | Chief Executive Officer | 28.10.2019 |
| 2 | Joseph Phales | | Ag: Head of Business & Operations | 28.10.2019 |

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ndivyo tunavyoanza uchaguzi wa mitaa

**MCHAKATO** wa uchaguzi wa serikali za mitaa unaanza rasmi leo. Na huu ndiyo wakati wa wagombea wa nafasi mbalimbali za uongozi uwe katika serikali za vitongoji, vijiji na mitaa leo ndiyo siku muhimu ya kuanza kuchukua na kurejesha fomu kwa ajili ya uchaguzi huo unaofanyika mwishoni mwa mwezi ujao.

Tukumbuke kuwa uchaguzi huo utafanyika Novemba 24 na nafasi zitakazojazwa ni wenyeviti wa vitongoji, mitaa na wajumbe wa kamati ya mtaa, wenyeviti wa vijiji pamoja na wajumbe wa halmshauri za vijiji.

Kwa hiyo kuanzia sasa tunawakumbusha wagombea kuwa wana siku saba za kuchukua na kurejesha fomu hizo ambazo siku ya mwisho wa kuzirudisha ni Novemba 4, 2019.

Fomu hizo zinatakiwa kujazwa na kuwekewa taarifa zote za msingi za mgombea ambaye pamoja na mambo mengine usahihi ni jambo la kuzingatia.

Kwa ujumla tunapenda kuona uchaguzi huu wa ngazi za chini au kwenye mashina unaowahusu wananchi wetu, ukifanyika kwa amani na utulivu, usawa, maridhiano na zaidi kwa kuzingatia misingi ya kidemokrasia.

Mara nyingi kwenye mchakato wa kuchukua na kurudisha fomu ndiko kunakokuwa na mizengwe. Kuna madai kuwa mara nyingi wagombea wakirudisha fomu, maofisa wanaotakiwa kupokea fomu hizo hasa siku ya mwisho huingia mitini na wagombea wanapofika wanakuta ofisi zimefungwa.

Yote hayo yanadaiwa kufanyika ili kukwamisha baadhi ya wagombea kwa maelezo kuwa fomu zao hazikufikishwa kwa wakati.

Tunaomba wahusika wafanyekazi hizo kwa uadilifu na kwa haki kwa vile kila mshiriki ana haki kikatiba ya kuchagua na kugombea ili achaguliwe kuwa kiongozi ama awachague viongozi anaowapenda.

Tungependa kusisitiza kuwa mizengwe na udanganyifu si jambo jema wakati huu ambao watu wengi wanautizama uchaguzi wa serikali za mitaa kama hatua ya kwanza yakuelekea kwenye uchaguzi mkuu wa 2020.

Aidha, tunavikumbusha vyama kuwapa nafasi wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kushiriki kwa kuwapa maeneo ya kugombea kwani kuna nyadhifa mbalimbali.

Ikumbukwe kuwa huu ni uchaguzi mkubwa kwani takribani viongozi 1,000,000 wanachaguliwa nchini kote, hili si jambo la kuupuuzwa.

Ndiyo maana tunawasihi wasimamizi wa uchaguzi wanaoshughulikia kupokea fomu wawe watenda haki, wakati mwingine suala la kuweka mapingamizi limekuwa likifanywa pengine kwa nia ya kuharibiana.

Tungependa kusema hakuna sababu ya kuharibiana kwa kuzua na kutangaza ubaya usio na sababu dhidi ya mgombea kwa nia ya kuvuruga demokrasia.

Ni vizuri kila Mtanzania akapata haki yake ya msingi ya kutimiza matakwa ya kidemokrasia na kufanya kila jambo kwa hatua kama ambavyo serikali inaelekeza.

Wagombea wakumbuke kuwa kampeni wakati wa kuchukua fomu haziruhusiwi, licha ya kwamba wanaweza kuchukua fomu kwa namna wanavyotaka, lakini si kuleta mbwembwe zinazoashiria kufanya kampeni.

Kwa upande wa vyama huu ndiyo wakati wa kutumia wanachama wenye sifa ili kuondoa mafarakano ndani ya chama.

Tunavikumbusha vyama kuwa ni jukumu lake kuwadhamini kama ambavyo kanuni zinavyoelekeza.

Nasi tunaungana na maelezo ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) inayesema kuwa serikali haitarajii itokee changamoto ya aina yoyote kubwa ya kuvuruga uchaguzi.

Endapo kutatokea jambo lisiloeleweka wagombea na watu wengine waliulize kwa mamlaka za kusimamia uchaguzi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com






Na Raphael Kibiriti

## Muungwana Lazima Nilonge

# Serikali isimamie maelekezo ili wakulima wa pamba walipwe

**KUNA** maelezo mengi yanayoweza kutolewa kuhusu kadhia ya wakulima walio wengi wa pamba kutolipwa fedha zao hadi sasa, tangu msimu wa pamba ulipozinduliwa Mei 2, mwaka huu mkoani Katavi.

Hiyo ni pamoja na ukweli kwamba pamba waliyoiuza kupitia Vyama vya Ushirika vya Msingi (AMCOS), imeshasafirishwa na matajiri kutoka kwenye maghala ya vyama hivyo, bila ya kuwalipa stahiki yao.

Hata hivyo, lililo la msingi ambalo Muungwana analiona ni la kulipwa kwa fedha hizo za wakulima hawa ambao wengi wao ni wadogo wadogo, wakiendesha maisha kwa kulitegemea zao hili husus katika maeneo linakolimwa.

Nasema hili ni la msingi zaidi kwa sababu maelekezo mbalimbali ambayo yamekuwa yakitolewa na serikali kwa nyakati tofauti kuhusiana na kadhia hii, bado hayajatekelezwa kwa ukamilifu na wanunuzi wa zao hilo.

Na matokeo yake ni haya yanayoripotiwa kutoka maeneo mbalimbali, jinsi wakulima wanavyohangaikia kupata fedha hizo kwa miezi sasa.

Kwa muda wote wa takribani miezi sita iliyopita, Muungwana amekuwa akieleza jinsi hatua ya kutolipwa kwa fedha hizo inavyozidi kuwadidimiza wakulima hawa kimaisha na kukwamisha mipango yao ya kuongeza tija katika kilimo.

Muungwana anasema hivyo kwa sababu wakulima ambao pamba ni zao la biashara, wanalitegemea kama chanzo chao kikuu cha kuwaingizia mapato ambayo pamoja na mengine huyatumia kugharimia maandalizi ya mashamba, pembejeo na mahitaji mengine.

Lakini mapato hayo hutumika kwa minajili ya manunuzi ya chakula, ikichukuliwa ukweli kwamba baadhi ya maeneo ya mikoa kunakolimwa pamba hayakupata chakula cha kutosha msimu uliopita.

Kwa hali hiyo wanategemea fedha ya mauzo ya pamba ili wanunulie chakula, huku bei ya baadhi ya mazao ya vyakula kama mahindi sasa ikiwa imefikia kiasi cha 16,000/- kwa debe, kwenye maeneo yanayolima pamba kama zao la biashara.

Kwa mikoa ya Kanda ya Ziwa kwa mfano fedha zitokanazo na mauzo ya pamba ndizo hutumika katika ununuzi wa mifugo kama ng'ombe, ujenzi wa nyumba bora, ununuzi wa vifaa vya usafiri kama baiskeli, bodaboda, bajaji, tela za kukokotwa na wanyama na raslimali zingine.

Aidha, wanategemea mapato ya zao hilo kwa ajili ya kununulia sare za watoto wao, ada na mahitaji mengine muhimu ya kimaendeleo.

Sasa haya yote kimsingi yamekwama na ndiyo maana hali si nzuri kwa wakulima hawa, wakati tayari katika maeneo yao msimu mpya wa kilimo umeshaanza na mvua zinaendelea kunyesha.

Kama nilivyosema, mengi yanaweza kuelezwa na kwa kweli yanaendelea kuelezwa na wanunuzi ambao kwa maoni ya Muungwana, wanakwamisha maendeleo ya wakulima hawa.

> **Nasema hili ni la msingi zaidi kwa sababu maelekezo mbalimbali ambayo yamekuwa yakitolewa na serikali kwa nyakati tofauti kuhusiana na kadhia hii, bado hayajatekelezwa kwa ukamilifu na wanunuzi wa zao hilo.**

Wanunuzi wanadai kuporomoka kwa bei ya zao hilo katika soko la dunia kama sababu ya msingi ya wao kutowalipa fedha wakulima hawa pamoja na kwamba tayari wameshasafirisha pamba ya wakulima hawa kutoka AMCOS na kuipeleka kwenye viwanda vyao vya kuchambua pamba.

Kwa maana nyingine wanunuzi hawa ni kama vile wamewakopa wakulima, lakini kuwalipa watoto wa mjini wanasema, inakuwa 'ngoma nzito.'

Taarifa ambazo Muungwana amekuwa akizipata kutoka kwa viongozi wa baadhi ya AMCOS ni kwamba kwa miezi sasa wamekuwa wakiahidiwa kupelekewa fedha na wanunuzi karibu kila siku lakini siku, wiki, na sasa miezi inakatika, hakuna kinachoendelea zaidi ya kuacha kilio kwa wakulima.

Hali iko hivi hata baada ya Rais John Magufuli kuwa ametoa siku 14 Oktoba 9, akiwa Katavi kwa wanunuzi kuhakikisha wanawalipa wakulima fedha zao ili kujiandaa na msimu mpya wa kilimo.

Bado ni rai basi ya Muungwana kwa serikali isimamie maelekezo yake ili wakulima wa zao hili ambao bado hawajalipwa waweze kulipwa fedha zao ili zistawishe maisha yao.

Distributed via ippmedia



Wakazi wa Mbezi Msumi wakihangaika kutafuta usafiri wa kuwafikisha Mbezi kituoni. Mkwamo huu unaotokea mara kwa mara eneo la kwa Pesa Pesa. **PICHA: GAUDENSIA MNGUMI.**

# Kesi vigogo NSSF yapigwa kalenda

**Na Hellen Mwango**

KESI inayowakabili vigogo tisa wa Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF),akiwamo Kaimu Mkurugenzi wa Fedha, Jamila Vullu na wenzake wa kitengo cha fedha, imepigwa kalenda mpaka Novemba 7, mwaka huu.

Kesi hiyo ya uhujumu uchumi ikiwamo kughushi, wizi na kutakatisha zaidi ya Sh. bilioni mbili, ilipangwa jana kwa ajili ya kutajwa, lakini upande wa Jamhuri ulidai upelelezi haujakamilika.

Kesi hiyo ilitajwa mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Mfawidhi, Kelvin Mhina, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Simon, aliomba tarehe nyingine ya kutajwa, hivyo Hakimu Mhina alisema itatajwa tena Novemba 7, mwaka huu na washtakiwa wataendelea kukaa mahabusu.

Washtakiwa wengine mbali na Vullu ni mwandishi wa hundi, Abdul Njozi, meneja uhakiki, Amir Kapera, mhasibu, James Oigo, mhasibu mkuu, Hellen Peter na mhasibu mwandamizi anayeshughulikia matumizi, Ivonne Kimaro.

Wengine ni, kaimu meneja rasilimali watu, Tikyeba Alphonce na mhasibu Dominic Mbwete.

Wankyo alidai katika shtaka la kwanza washtakiwa wote wanadaiwa kati ya Julai mosi mwaka 2016 na Septemba 4 mwaka 2017 walikula njama ya kutenda makosa ya kughushi na kutakatisha.

Shtaka la pili mshtakiwa Njozi na Akiri wanadaiwa katika kipindi hicho, wakiwa watumishi wa umma, kwenye ofisi za Makao Makuu ya NSSF walighushi hundi 47 za Benki ya CRDB kwa akaunti namba 01j1028249500 yenye jina la NSSF zenye jumla ya Sh. 2,130,211,437.35.

Katika shtaka la tatu, washtakiwa wote wanadaiwa katika kipindi hicho, wakiwa Makao Makuu ya Shirika waliiba fedha hizo.

Washtakiwa hao pia wanashtakiwa kwa kosa la kusababisha hasara ya jumla ya Sh. 2,130,211,437.35 kwa kushindwa kutekeleza majukumu yao wakiwa watumishi wa umma.

**Kesi hiyo ilitajwa mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Mfawidhi, Kelvin Mhina, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam.**

Distributed via inmedia

# Jafo kuzindua Wiki ya Azaki

**Na Mwandishi Wetu**

MASHIRIKA 14 yaliyo kwenye Asasi za Kiraia (AZAKI), yatashiriki Wiki ya Asasi za Kiraia itakayofanyika mjini Dodoma kuanzia Novemba 4 hadi 8, mwaka huu kwa kutoa elimu na maonyesho mbalimbali ya kazi zinazofanywa na asasi hizo.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemeni Jafo, anatarajiwa kuzindua wiki hiyo ambayo kaulimbiu yake mwaka huu ni 'Ubia kwa Maendeleo'.

Mkurungenzi Mkuu wa Taasisi ya Foundation for Civil Society, Francis Kiwanga, aliwaambia Wahariri wa vyombo vya habari jijini Dar es Salaam jana, kuwa shughuli zitakazofanyika katika wiki hiyo ni pamoja na uelimishaji kwa kushirikisha serikali, wabunge, waandishi wa habari na wananchi.

Mada mbalimbali zitatolewa zikiwamo sekta za uchumi, afya, jinsia, watoto na watu wenye ulemavu.

Alisema lengo la Wiki ya Asasi za Kiraia ni kusherehekea mafanikio ya kazi za asasi na kuwa karibu na wadau wake na kuondoa dhana kwamba asasi hizo zipo kwa ajili ya misuguano.

Alisema lengo ni kuonyesha mbinu zinazotumiwa na asasi hizo kujaribu kufikia Tanzania inayotakiwa.

Kiwanga alieleza kuwa taasisi zaidi ya 500 kutoka Tanzania Bara na Visiwani zitashiriki kwenye wiki hiyo na kati ya hizo 150 zitaonyesha maonyesho ya kazi za asasi hizo.

Kadhalika katika kuadhimisha wiki hiyo, alisema AZAKI imeandaa tuzo ya uandishi wa habari uliotukuka katika maeneo mbalimbali likiwamo la usawa wa kijinsia.

"Tuzo 13 zitashindaniwa katika wiki hiyo kutoka kwa wateule 39 kati 166 walioingia kushiriki uandishi wa maeneo hayo," alisema.

Pia, alisema kutafanyika matembezi ya hisani yatakayoanzia Nyerere Square hadi Viwanja vya Jamhuri na kupokelewa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.



# Mangula aonya kutoa siri za vikao

**Na Happy Severine, SIMIYU**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara, Philip Mangula, amewaonya viongozi wa chama wanaotoa siri za vikao kwani kufanya hivyo ni kukiuka maadili na wanaobainika wachukuliwe hatua za kinidhamu.

Mangula akitoa onyo hilo jana mkoani Simiyu wakati wa mkutano wa Halmashauri Kuu ya CCM wilaya, mkoa na watendaji wa serikali wa halmashauri sita za mkoa wa Simiyu.

Mangula alisema viongozi ambao wanaotoa siri za vikao hawafai kuongoza chama na wanapobainika ni vema wakachukuliwa hatua za kinidhamu.

"Kumekuwa na tabia chafu kwa baadhi ya viongozi ndani ya chama chetu ambao wanatoa siri za ndani za vikao...na kama hamjui kufanya hivyo ni kukiuka kanuni za chama na endapo kuna viongozi watakaobaikika kufanya hivyo wachukuliwe hatua za kinidhamu mara moja," alisema Mangula.

Aliongeza kuwa viongozi wa chama na serikali wazingatie taratibu na kanuni za utendaji wa majukumu yao, huku akiwasihi kuacha majungu katika ofisi zao ili kuondoa migongano na migogoro.

Mangula pia alionya tabia ya baadhi ya viongozi wa chama kutumia madaraka yao kuwabugudhi watendaji wa serikali kisha kuupongeza Mkoa wa Simiyu kwa sera ya ujenzi shule bora na zahanati

Nae Mkuu wa mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka, alimhakikishia Mangula ushirikiano na chama na kuwaomba watendaji kuzidisha kasi ya kusikiliza malalamiko ya wananchi.

PINGO's FORUM
P.O BOX 14437, ARUSHA - TANZANIA.
TEL: +255 27 250 8965, 0786 542525 FAX: +255 27 250 8965
SAKINA KWAIDDI LUSH GARDEN ENTRANCE

TAARIFA KWA UMMA

PINGOs Forum ni shirika lisilo la kiserikali linahudumia wafugaji, wawindaji,wakusanya matunda na warina asali wa asili.

Shirika linapenda kuwatangazia umma wa watanzania na wanuafaika wote wa maeneo ya mradi kwamba tumepokea ufadhili kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali kama inavyo onyeshwa kwenye jedwali hapo chini kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 2020

| S/NO | Mfadhili | Namba ya mradi | Shughuli | Muda wa mradi | Fedha za mradi |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | FOUNDATION FOR CIVIL SOCIETY | FCS/MG/W2/19/1734 | Masuala ya sera | 07/2019 - 12/2019 | 100,000,000 |
| 2 | OXFAM GB | TANB40, RO 8994 | Usawa wa kijinsia | 06/2019 - 11/2019 | 121,000,000 |
| 3 | IWGIA | 8200-2111 | Mafunzo ya matumizi bora ya ardhi | 05/2019 - 11/2019 | 45,160,000 |
| 4 | Tanzania Land Alliance | LTSP | Mafunzo ya matumizi bora ya ardhi | 09/2018 - 11/2019 | 275,979,000 |
| 5 | TEBTEBBA | IWGIA/9021 | Huduma za Jamii | 11/2017 – 8/2020 | 134,635,970 |
| 6 | IWGIA CC | 4705 | Mabadiliko tabia nchi na mazingira | 06/2019 – 12/2019 | 48,398,258 |
| | | | | | |

215484502

Email: info@pingosforum.or.tz, Website: www.pingosforum.or.tz

# Kesi wafugaji wanaodaiwa kupiga askari hifadhini yapigwa kalenda

**Na Christina Haule, MOROGORO**

MAHAKAMA ya Mwanzo Mikongezi, Kata ya Doma wilayani Mvomero mkoani Morogoro imelazimika kuahirisha kesi ya kujeruhi iliyowahusisha wafugaji watatu wa jamii ya kimasai wanaodaiwa kuwajeruhi askari wanyamapori, baada ya mashahidi wanne wa upande wa washtakiwa kutofika mahakamani wakidaiwa kuugua malaria.

Washtakiwa hao wanadaiwa kuwajeruhi askari kwa marungu walipokuwa wakitoa mifugo iliyoingizwa kwenye msitu wa hifadhi.

Akiahirisha kesi hiyo, Hakimu wa Mahakama hiyo, Mussa Lilingani, alisema, amelazimika kuahirisha baada ya wafugaji hao kutokana na mashahidi hao kutofika mahakamani huku akiagiza itolewe hati ya kukamatwa kwa washtakiwa wengine watatu ambao wanadaiwa kukimbia baada ya tukio hilo.

Awali, hakimu huyo aliwataja washtakiwa hao kuwa ni Sperwa Kisakiri, Daniel Babalai na Kashuma Kishaki, akieleza kuwa siku ya tukio, washtakiwa hao wanadaiwa kuwajeruhi Emmanuel Willnely na Exavery Pius ambao ni askari wa Kamati ya Wanyamapori ya Maliasili ya Kijiji kwenye msitu wa hifadhi wa asili wa Kijiji cha Kihondo, Kata Doma.

Alisema askari hao walijeruhiwa na wafugaji walipokuwa wakiondoa mifugo iliyoingizwa hifadhini kinyume cha sheria.

Tukio hilo lilitokea Oktoba 8, mwaka huu katika msitu huo wa hifadhi na kesi hiyo namba 115/2019 ilisomwa kwa mara ya kwanza mahakamani huko Oktoba 11 na imepangwa kusikilizwa tena kesho.




Mratibu wa Mradi wa Action for Change (ACHA) na The Right Way (TRW), Jackson Sikahanga, akizungumza jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kuendesha mpango wa pamoja wa kutoa elimu ya uraia na uangalizi wa uchaguzi wa serikali za mitaa kwa mwaka 2019. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Mabalozi wapya watangaza neema

INATOKA UK 2

Tanzania itakuwa tayari kutoa ushirikiano wowote atakaouhitaji.

Kwa upande wake, Jenerali Karamba, taarifa hiyo ilisema, aliishukuru Tanzania kwa kumkaribisha na kumhakikishia Rais Magufuli kuwa katika kipindi chake atahakikisha matarajio ya Rais wa Rwanda, Paul Kagame, ya kukuza zaidi uhusiano wa Tanzania na Rwanda yanafanikiwa.

Rais Magufuli alimkaribisha Balozi Karamba na kumtaka ahakikishe biashara kati ya Tanzania na Rwanda inakuwa zaidi ikiwamo kutekelezwa kwa makubaliano yake na Rais Kagame wa Rwanda kutumia Bandari ya Tanga katika upokeaji na usafirishaji wa mizigo ya kwenda na kutoka Rwanda.

"Sisi ni ndugu na ni wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, mwenyekiti wetu ni Rais Kagame. Hatuna sababu ya kupoteza muda, nataka usukume sana suala la kuongeza biashara kati ya Tanzania na Rwanda ili nchi zetu zinufaike zaidi," alisisitiza Rais Magufuli.

# Jafo atoa maagizo sita uchukuaji fomu

INATOKA UK 2

**MARUFUKU KAMPENI KABLA**

"Kampeni kabla ya uchaguzi hairuhusiwi, naamini hata watu wakileta mbwembwe za aina yeyote, lakini zisiwe katika 'style' ya kampeni kwenye uchukuaji fomu, huwezi kumzuia kuchukua fomu kwa namna anayotaka," alisema.

Aliongeza: "Mtu kusindikizwa na rafiki zake kwenye kanuni halijawekwa, lakini jambo hilo linapaswa lisiwe kampeni."

Agizo kwa Ma-RC, Ma-DC

Jafo aliwaagiza Wakuu wa mikoa na wilaya kuhakikisha maeneo yanakuwa tulivu na watu watimize matakwa ya kidemokrasia.

Vyama vyaonywa

Alivitaka vyama vya siasa kuhakikisha vinatumia vizuri demokrasia kwa kupeleka watu wanaowakusudia na kuwadhamini kwa mujibu wa kanuni.

"Hatutarajii itokee changamoto ya aina yeyote na kama kuna jambo halijaeleweka vizuri, watu waliweza kuomba ufafanuzi na nimetoa ufafanuzi kwa vyama vyote vya siasa vyenye usajili wa kudumu na namna ya kuchukua na kurejesha fomu," alisema.

Alieleza kuwa anaamini ufafanuzi huo utakuwa umesaidia ili kushiriki vizuri katika mchakato huo kwa siku saba.

Katazo kwa watendaji

Alisema kutokana na uongozi kukoma kwenye nafasi hizo Oktoba 22, mwaka huu shughuli zote zipo chini ya watendaji wa vijiji na mitaa na zitaendeshwa kwa mujibu wa sheria na watashirikiana na watendaji wa kata husika.

"Agizo kwa watendaji wa vijiji na mitaa hawataruhusiwa kutekeleza jukumu lolote ambalo linapaswa kuamuliwa kwanza na Halmashauri za vijiji au mitaa," alisema.

Alifafanua kuwa kuna majukumu ambayo yanapaswa kuamuriwa na Halmashauri za vijiji au mitaa, hayapaswi kufanywa na mtendaji wa kijiji na lazima yaende kwa mtendaji wa kata na kuwasilisha kwa Mkurugenzi wa Halmashauri kuangalia namna ya kulitatua.

**TGNP YAFUNDA WANAWAKE**

Wanawake wenye dhamana za uongozi wametakiwa kuongoza kwa hekima na malengo mazuri yenye kuleta mafanikio, ili wawe kumbukumbu nzuri itakayowavutia vijana na vizazi vijavyo.

Mwenyekiti wa Bodi ya Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Assey Muro, aliyasema hayo jana alipokuwa akifungua mafunzo kwa wanawake zaidi ya 100 wa Dar es Salaam waliojitokeza kugombea nafasi mbalimbali za uongozi kwenye chaguzi wa Serikali za mitaa jijini hapa.

Muro alisema wanawake wamekuwa ni viongozi wazuri kuanzia kwenye kaya, usimama katika kuhakikisha familia hazipotezi mwelekeo bali zinapiga hatua za kimaendeleo, hivyo anaamini kuwa wanaopata uongozi wataendelea kuwa viongozi wazuri.

" Muwe mfano bora kwa vizazi vyetu, kijana akikaa awaze kuwa natamani kuwa kama akutaje jina kwa namna ulivyomvutia, sisi TGNP tuko pamoja katika kuhakikisha mnavuka na kufanikisha malengo ya maendeleo yaliyowekwa," alisema Muro.

Alisema wajitahidi kuhakikisha wanashiriki kikamilifu katika kutafuta njia ya kutatua kero zinazowakabili jamii wanapoishi, kama vile kukosekana kwa maji safi na salama, huduma bora za afya na elimu.

Mwezeshaji wa mafunzo hayo, Hilda Dadu, alisema malengo ya TGNP ni kuwajenga wagombea uelewa wa mchakato na uchaguzi ushiriki wa wanawake na kuweka mbinu za ushindi.

Alisema pia kupitia mafunzo hayo wanalenga kuwajenga uwezo wagombea kutambua jinsi ya kujenga ajenda za vipaumbele vitakavyowawezesha wakubalike. Kuweka mkakati wa pamoja ya kuweka pembeni tofauti za kiitikadi na kubeba agenda ya wanawake wakati wa uchaguzi na baada.

Katika Ilani ya Uchaguzi ya wanawake, uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2019 na uchaguzi Mkuu mwaka 2020 ambayo wanawake hao walipewa kuna madai kadhaa ikiwamo kuhoji vyama vya siasa kuwa na mapengo ya jinsia ndani ya uongozi wa vyama.

Pia vimetakiwa kuzingatia idadi ya wagombea wote nafasi za ushiriki wa wanawake isipungue asilimia 50, pia viweke mikakati ya kuwezesha wanawake na makundi maalum kwenye kampeni.

Ilani hiyo iliyobeba ajenda ya Mwanamke, Turufu ya Ushindi mwaka 2019/2020 imeandaliwa na taasisi tatu ambazo ni pamoja na TGNP Mtandao, Mtandao wa Wanawake na Katika na Women Fund Tanzania.

Ilani hiyo inabainishwa kuwa imelenga kuhamasisha wanawake, wapigakura kukataa kuendelea kutumia kama wapiga debe, wasindikizaji, waburudishaji katika kampeni na waathirika wa umasikini.

***Imeandikwa na Agusta Njoji, Dodoma na Beatrice Moses, Dar***

# DC azuia uchomaji wa nyumba za wananchi

**Na Gurian Adolf, NKASI**

MKUU wa Wilaya ya Nkasi mkoani Rukwa, Said Mtanda, amepiga marufuku kitendo cha askari wa Pori la Akiba Lwafi, kuchoma moto nyumba za wakazi wa kijiji cha Mpata Kata ya Kirando kisha kuwaondoa kwa nguvu kwa madai wanaishi ndani ya hifadhi.

Marufuku hiyo imetokana na askari hao kuvamia kijiji hicho na kuendesha operesheni ya kuwaondoa kwa nguvu wananchi hao pamoja na kuchoma moto nyumba zao, huku wakitoa siku tatu wakazi wengine wa kijiji hicho wawe wamehama.

Akizungumza na wananchi hao baada ya kupokea malalamiko yao, alisema amesitisha operesheni ya kuwaondoa na ameunda timu maalumu ya wataalamu wakiwamo maofisa ardhi watakaokwenda kupima eneo hilo ili kubaini mipaka kati ya kijiji na pori la akiba.

Alisema baada ya timu hiyo kuwasilisha ripoti ndipo serikali itabaini ukweli iwapo kijiji hicho kipo ndani ya hifadhi au sivyo, na kama kijiji hicho kipo ndani ya hifadhi, utaandaliwa utaratibu wa kuwaondoa.

Aliwataka wananchi hao kuendelee kuishi katika kijiji hicho bila kubugudhiwa na mtu yeyote hadi timu itakamilisha kazi yake na kuwa serikali itatoa taarifa kwao.

"Lengo la serikali ni kuona hakuna mtu anayeonewa na kama jambo hilo limefanyika, basi halitaendelea tena na kila mmoja atapata haki yake kulingana na taarifa ya timu itakavyobainisha ukweli wa jambo hilo," alisema.

Awali Mwenyekiti wa kijiji hicho, Raymond Makanta, alimweleza mkuu huyo wa wilaya kuwa wananchi wanaishi kwa taabu na kwa wasiwasi baada ya askari wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA) kuvamia kijiji hicho na kuwa wanahitaji msaada wa haraka kwa kuwa mali zao zimeharibiwa na wamepewa siku tatu wawe wameondoka kijijini hapo.

Diwani wa Kirando, Kakuli Seba, alimshukuru mkuu wa wilaya kwa kufika kwa wakati katika eneo hilo kwani amani ilikuwa imetoweka na kueleza kuwa kitendo cha kuwazuia askari hao kuendelea na operesheni inaonyesha kuwa serikali ipo kazini na inatatua kero za wananchi kwa wakati.

Alisema anaamini serikali italitafutia ufumbuzi wa haraka jambo hilo ili wananchi waendelee kuishi kwa amani na furaha kama ilivyokuwa awali.



Mwenyekiti wa Tanesco Saccos, Somoe Nguhwe, akizungumza wakati wa Mkutano Mkuu wa 51 wa wanachama, uliofanyika jijini Dar es Salaam wikiendi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wagombea CCM watakaotoa rushwa ya ngono kukatwa

**Na Marco Maduhu, KISHAPU**

KAMATI ya siasa ya Chama Cha Mapinduzi CCM (CCM) wilayani Kishapu mkoani Shinyanga, imewaonya wagombea wanawake kutoa rushwa ya ngono ambao watajitokeza kutia nia kwenye uchaguzi mkuu mwakani 2020.

Imesema mgombea atakayebainika kutoa rushwa ya aina yoyote ile ikiwamo ya ngono, watalikata jina lake ili lisewapo kwenye mchakato wa kupigiwa kura za maoni ndani ya chama, na hatimaye kuikosa nafasi hiyo ya uongozi aliyokuwa anaitaka.

Hayo yalibainishwa juzi na wajumbe wa kamati hiyo walipokuwa kwenye mkutano na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), uliokuwa na lengo la kujadili ushiriki wa wanawake kuwania nafasi za uongozi kwenye uchaguzi.

Walisema kwenye kamati yao wameshajiwekea mikakati kuwa mgombea yeyote ambaye atabainika kutoa rushwa ikiwamo ya ngono, wanalikata jina lake na kuwapitisha wale ambao hawajatoa kitu chochote, ili kuweza kupata viongozi waadilifu, waaminifu na wapigania maendeleo ya wananchi.

Mmoja wa wajumbe wa kamati hiyo Gregory Kibusi, ambaye ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi wilayani Kishapu, alisema mgombea ambaye anapenda kutoa rushwa ili apate kushinda huyo siyo mzuri katika utendaji kazi, na ndio maana wao wamejiwekea mikakati ya kukata majina yao.

"Tuna tumia nafasi hii kuwaonya wagombea wote ambao watajitokeza kutia nia ya kuwania uongozi katika uchaguzi mkuu mwakani, wakiwamo wanawake hasa wanaowania Viti Maalumu kuacha kujihusisha na masuala ya rushwa ya ngono, tukikubaini tunafyeka jina lako," alisema Kibusi.

Naye Mwenyekiti wa kamati hiyo, Shija Ntelezu, ambaye ni Mwenyekiti wa CCM wilayani Kishapu, alitoa wito kwa wanawake wajitokeze kwa wingi kuwania nafasi za uongozi kwenye uchaguzi mkuu, na watawapatia kipaumbele kama walivyofanya kupitisha wagombea uchaguzi serikali za mitaa.

Mwanaharakati kutoka TGNP Mtandao, Eva Juma, alisema wamefanya mkutano huo wa viongozi wa chama, ili kuondoa mitazamo hasi ya mwanamke kuwa hawezi kuwa kiongozi na kuacha tabia ya kukata majina yao, bali wawapitishe ili kuwapo na uwiano wa kijinsia kwenye uongozi.

## Balozi afurahishwa ushirikiano na wadau

**Na Sabato Kasika**

BALOZI wa Denmark nchini, Mette Nørgaard Dissing-Spandet, amepongeza ushirikiano wa mashirika ya kiraia na serikali katika kukabiliana na changamoto za jamii na kufanikisha miradi mbalimbali ya maji.

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari baada ya kutoka Kigoma alikokwenda kuzindua mradi wa maji unaotumia nguvu ya jua unaowahudumia wakimbizi wa kambi ya Nyarugusu.

Ilisema taarifa hiyo kuwa shirika la kimataifa lisilo la kiserikali la Water Mission Tanzania, linaendelea kuwanufaisha watu kwenye maeneo yenye shida ya maji nchini kwa kutekeleza miradi ya kuwapatia majisafi.

Alisema katika taarifa yake kuwa hadi sasa wenyeji 30,000 wa Zeze, Kasanda, Kakonko, Heru Ushingo, Mvugwe na Kazilamihunda-Juhudi wanapata majisafi na salama.

Aliahidi kwamba katika siku zijazo, Water Mission Tanzania na washirika wake wanatarajia kuwahudumia hadi watu 80,000 katika jamii zinazozunguka kambi nchini kote kwa kujenga miradi ya majisafi na salama.

"Mbali na miradi ya maji katika kambi za wakimbizi mkoani Kigoma, Tanzania, Water Mission Tanzania, imetekeleza miradi ya maji 24 kwenye maeneo mbalimbali ya vijijini nchini yenye changamoto ya kupata majisafi, tangu ilipoanza kutoa huduma nchini mwaka 2014," alisema.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa The Grundfos Foundation (Poul Due Jensen Foundation), Kim Nøhr Skibsted, alisema, mradi huo ulianza kufanyiwa kazi mwaka 2016 wakati taasisi za Grundfos Foundation na Water Mission zilipoondoa miundombinu ya mradi wa zamani uliokuwapo na kujenga mradi unaotumia teknolojia za kisasa na umeme wa jua.

"Lengo ni kuwapatia majisafi na salama maelfu ya wakimbizi kwenye kambi ya Nyarugusu na maeneo ya vijiji jirani. Mradi huu ni wa pekee miongoni mwa miradi ya maji iliyotekelezwa na taasisi yetu," alisema.

Mbali na kuwezesha jamii kupata majisafi zinapatiwa maarifa ya kutunza mradi na matumizi ya nishati mbadala kuendesha miundombinu yake.

"Mfumo wa ushirikiano wa wadau kufanikisha miradi kwa maeneo yenye mahitaji unapaswa kutumika sehemu mbalimbali duniani kama, ambavyo wadau wamekuwa wakishirikiana kuhakikisha eneo hili la wakimbizi linapata maji salama na kuondoa hatari ya milipuko ya magonjwa yatokanayo na ukosefu wa maji salama," alisema Skibsted.

Makamu wa Rais wa Mradi wa Kimataifa kutoka Water Mission International, Seth Womble, alisema kufanikisha miradi ya maji katika kambi za wakimbizi kumewaongezea kujiamini katika utekelezaji katika maeneo mengine nchini.

# Waziri ataka mradi wa umeme ulindwe

**Na Idda Mushi, RUFIJI**

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, amewataka wananchi na viongozi wa mikoa zaidi ya 11 inayotegemewa katika uzalishaji wa umeme wa maporomoko ya maji ya mto Rufiji wa Julius Nyerere, kulinda na kutunza vyanzo vyake vya maji.

Amewataka kutumia maji yaliyopo vizuri kwa shughuli za kilimo, mifugo na uvuvi ili mradi huo ukikamilika uweze kujiendesha.

Waziri Kalemani alisema hayo baada ya kutembelea mradi huo mkubwa wa kuzalisha umeme ambao kukamilika kwake kutawezesha kuzalisha Megawatts 2,115 zitakazoingizwa kwenye gridi ya Taifa na kuondoa changamoto ya kukatika ovyo kwa umeme, ambapo hii ni awamu yake ya tisa kutembelea mradi huo.

Alisema nia ya ziara yake ni kujionea maendeleo ya kazi zinazofanywa na mkandarasi, kubaini changamoto za kiusimamizi na manufaa na fursa hasa kipindi cha utekelezaji wa mradi,ambapo licha ya kuridhishwa na kasi ya ujenzi kwenda na muda, aliahidi kuendelea kufika katika mradi huo kila mwezi ili kuukagua na kubaini changamoto na fursa.

Waziri Kalemani alisema hali ya upatikanaji wa maji kwa sasa ni nzuri, maporomoko ya maji ya Mto Rufiji yanatakiwa kufika mita 1,000 kwa sekunde kwa siku wakati wa kiangazi na 1,100 wakati wa mvua, na kwamba wataalamu wamethibitisha hali hiyo ni nzuri ingawa alihimiza ulindwaji na utunzwaji wa vyanzo hivyo vya maji.

"Wote wanaotumia maji watumie kwa uadilifu mkubwa, niwatake wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya, wakurugenzi wa halmashauri, maofisa tarafa, wenyeviti wa halmashauri, vijiji na mitaa wahakikishe wanasimamia kwa dhati na kwa weledi mkubwa matumizi ya maji… lakini mwezi Mei niliunda timu ya uratibu wa shughuli za utekelezaji wa mradi inayosimamiwa na Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na taasisi nyingine ianze kupita mkoa kwa mkoa," alisema.

Msimamizi wa mradi huo kutoka Tanesco, Mhandisi Stephen Manda, alisema wanategemea Juni 14, 2022 watakuwa wamekamilisha mradi na kwamba mradi una kazi nyingi ikiwamo barabara mbalimbali za kufika kwenye mradi ikiwamo za kufika kwenye madaraja ya muda, na daraja la kwanza limeshakamilika huku miundombinu mbalimbali ikiwa imekamilika kwa asilimia 85.

# Gairo yapewa mtambo kuchuja maji wa bil. 2.3/-

**Na Frank Monyo**

SERIKALI imepokea mtambo wa kuchuja maji yenye chumvi (Reverse Osmosis) uliogharimu Sh. bilioni 2.3 utakaotumika kwenye mradi wa maji wa Gairo mkoani Morogoro.

Akizungumza baada ya kupokea mtambo huo uliotoka Italia jana, Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, alisema serikali imetumia gharama kubwa kununua mtambo huo kwa kuwa inawathamini wananchi wake na haitasita kuchukua hatua zozote zinazostahili kutimiza azma yake ya kufikisha asilimia 85 ya upatikanaji wa maji vijijini na asilimia 95 mijini ifikapo mwaka 2020.

Alisema hivi sasa serikali inapambana kumaliza kabisa tatizo la maji kwa wananchi katika maeneo yote yenye changamoto ya upatikanaji wa huduma ya maji ikiwamo Wilaya ya Gairo, mkoani Morogoro.

Prof. Mbarawa alisisitiza kuwa pamoja na kufungwa kwa mtambo huo, serikali inafanya utaratibu wa kutafuta chanzo kingine cha maji kitakachoongeza uzalishaji wa maji yatakayotosheleza na kumaliza tatizo la maji kwa Mji wa Gairo.

"Ifikapo Novemba, 2019 mradi utaanza kutoa huduma kwa wananchi hivyo nakuagiza Mkandarasi wa Kampuni ya Protecno Srl ya Italia umalize kwa haraka kazi ya ufungaji wa mtambo na pampu," alisema.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Loata Ole Sanare, aliishukuru Wizara ya Maji kwa kuchukua hatua ya kuukamilisha mradi huo ambao umechukua muda mrefu kukamilika na kumpongeza Waziri wa Maji kwa kutimiza ahadi yake ya kuleta mashine hiyo itakayoimarisha kiwango cha ubora wa maji, ambayo kwa maeneo ya Gairo yana changamoto kubwa ya chumvi nyingi.

Alisema kuwa serikali imepeleka takribani Sh. bilioni 16 katika Wilaya ya Gairo kwa dhamira ya kumaliza tatizo la upatikanaji wa maji na kuishukuru serikali kwa niaba ya wananchi wa Gairo kwa kusikia kilio chao cha mahitaji ya huduma ya majisafi na salama, hususan kwa Mji wa Gairo unaokua kwa kasi wenye wakazi wapatao 55,000.

Ujenzi wa mradi wa maji wa Gairo unatekelezwa kwa pamoja na makandarasi wa Kampuni za Serengeti Ltd na Protecno Srl chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA) kwa gharama ya zaidi ya Sh. bilioni 10, umelenga kuhudumia wananchi wapatao 32,808 na utainua kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji kutoka asilimia 38 kwa sasa mpaka asilimia 80 utakapokamilika.



Mufti wa Tanzania, Sheikh Abubakar Zuberi, akizungumza na waumini wa dini ya Kiislamu kwenye hafla ya uzinduzi wa majengo ya madrasa ya Mudira Maahad Ruwdhwa Darul-Mustwafa, katika Kata ya Chang'ombe, jijini Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Sababu vijana kupata kiharusi kwa kasi

**Na Romana Mallya**

MATUMIZI ya sigara, pombe, uzito kupita kiasi, kula bila mpangilio umechangia vijana wenye umri wa miaka 30 kuendelea kupata kiharusi.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Ubongo, Mishipa ya Fahamu na Uti wa Mgongo upande wa Upasuaji, Mugisha Clement, kutoka Hospitali ya Aga Khan, aliyasema hayo juzi na kueleza umri wa watu kupata kiharusi umeshuka na sasa kijana mwenye miaka 30 yupo kwenye hatari hiyo.

Akizungumza na Nipashe ikiwa ni Siku ya Ugonjwa wa Kiharusi Duniani, Dk. Clement alisema awali kundi la watu waliokuwa kwenye hatari ya kupata kiharusi lilikuwa ni kwa wale waliokuwa na umri kuanzia miaka 50 kuendelea, lakini sasa vijana wenye umri wa miaka 30 kuendelea wapo kwenye hatari hiyo.

"Vijana wapo kwenye hatari ya kupata kiharusi kwa sababu wengi wanavuta sigara, wanakunywa pombe, wanakula chakula kupita kiasi na bila mpangilio, wana uzito mkubwa na wanatumia dawa zinazohatarisha maisha yao.

"Vyote vinasababisha mtu kupata shinikizo la damu, ukiwa na shinikizo la damu katika umri mdogo kunauwezekano wa kupata kiharusi."

Dk. Clement alisema takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO) zinaonyesha kati ya watu wanne, mmoja atapata kiharusi. Alisema mazoezi ni dawa na kuwashauri watu kwa wiki angalau wayafanye mara mbili au tatu.

Alitaja viashiria vya kiharusi kuwa ni mtu kuwa na uzito mkubwa na kutaka watu wapunguze wanga na waongeze matumizi ya mboga za majani.

"Vijana wengi wanavitambi na hii ni moja ya hatari ya kupata kiharusi kwa sababu mwili unakuwa na mafuta mengi kwenye damu ambayo hujiweka kwenye kuta za mishipa ya damu kwa hiyo utapata shinikizo la damu mwisho wa siku itapasuka," alisema.

Vilevile alisema kwa wanaotumia sigara husababisha uharibifu kwenye kuta za mishipa ya damu na kuifanya ikakamae.

Naye Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Mishipa ya Ubongo, kutoka hospitali hiyo, Philip Adebayo, alisema zipo aina mbili za kiharusi ambazo ni mishipa kuziba na damu kushindwa kupita kama kawaida na ya pili ni mishipa ya kupitisha damu kupasuka.

"Kila mtu yupo hatarini kupata kiharusi, tuitunze miili yetu, tufanye mazoezi kwa sababu matukio ya ugonjwa wa kiharusi yanaongezeka hasa nchi zinazoendelea," alisema.

# Vijana watakiwa kuchangamka

Na Woinde Shizza, ARUSHA

VIJANA mkoani Arusha wametakiwa kuongeza thamani ya mazao ya nafaka na mifugo yanayozalishwa kwenye maeneo yao na kuchangamkia fursa za masoko ya ndani na ya nje ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Ofisa Vijana na Maendeleo Jiji la Arusha, Hanifa Ramadhani, alisema wakati akizungumza jana kwenye mkutano wa vijana kutoka asasi mbalimbali za kiraia.

Aliwaambia vijana wanapaswa kusindika bidhaa za nafaka na kutengeneza vitu mbalimbali vinavyohitajika katika jamii, badala ya kuacha mazao ya wakulima yakiharibika kwa kukosa soko kwa vile hayajaongezewa thamani.

"Kazi hii mnapaswa nyie vijana muichangamkie hasa kuongeza thamani na kuyapeleka sokoni ili mpate ajira na uhakika wa kipato kitakachowainua kiuchumi," alisema.

Mratibu wa Shirika lisilokuwa la kiserikali la Infoy, Laurent Sabuni, linaloshughulikia masuala ya maendeleo ya vijana alisema wanawafundisha vijana usindikaji wa bidhaa za vyakula, hususani lishe pamoja na namna ya kuvifungasha vyakula hivyo.

Sabuni alisema kuwa vijana wanapaswa kuchangamkia fursa ya kuongeza thamani mazao na kuyafungasha katika viwango vya ubora ili yaweze kukubalika katika masoko ya ndani na nje.

"Vijana licha ya kujishughulisha na ujasiriamali pia wanapaswa kuongeza thamani ya mazao ya nafaka kama mahindi, ngano na hata mazao ya mifugo kwa kuyachakata na kuyafungasha kwa ubora na kuyafikisha sokoni yakiwa katika hali bora ya kuvutia walaji wa ndani na nje," alisema Sabuni.

Kwa upande wa vijana, mmoja wa vijana wanaonufaika Fransisca Wilson, alisema, tayari wameanza kutengeneza unga wa lishe kwa kutumia nafaka, hivyo kuwasaidia kuinua kipato chao na kuchangia maendeleo katika jamii zao.

Leonard Paulo mnufaika mwingine wa mafunzo ya ujasiriamali, alisema kuwa mwamko wa vijana katika kuongeza thamani umeongezeka, huku changamoto kubwa ikiwa ni mtaji wa kuanzisha biashara.

**"Vijana licha ya kujishughulisha na ujasiriamali pia wanapaswa kuongeza thamani ya mazao ya nafaka kama mahindi, ngano na hata mazao ya mifugo kwa kuyachakata na kuyafungasha kwa ubora na kuyafikisha sokoni yakiwa katika hali bora ya kuvutia walaji wa ndani na nje," alisema Sabuni.**

# Chuma chakavu walalama NEMC

Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA

WAFANYABIASHARA wa chuma chakavu wamelalamikia hatua ya Baraza la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC) ya kuzuia usafirishaji wa chuma. Usafirishaji wa chuma utaanza wafanyabiashara hao watakapokuwa na leseni mpya.

Chuma chakavu ni ghafi ya kutengenezea bidhaa za chuma kama nondo, wateja wakubwa ni viwanda vya chuma.

Taarifa kutoka kwa wafanyabiashara wa chuma ya hivi karibuni zililalamikia hatua ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira, George Simbachawene aliyeagiza leseni zote za biashara ya chuma chakavu zifutwe, wakati mchakato wa leseni mpya ukiendelea.

Ilielezwa kuwa baadhi ya sababu za kufuta leseni hizo ni pamoja biashara ya chuma chakavu kufanyika kiholela bila ya kuwa na kanuni hivyo kuikosesha serikali mapato.

Aidha, ilitajwa kuwa ni hatarishi kwa mazingira. Akizungumza jijini Arusha kwa niaba ya wenzake muuza chuma chakavu kutoka mkoani Singida Yazid Mtanda, alidai kuwa wiki iliyopita maofisa wa NEMC Kanda ya Kati walizuia asisafirishe shehena ya tani 12 ya chuma chakavu kwenda Arusha kwa wateja wake.

"Nilikuwa nasafirisha shehena hii nilikuwa na vibali vyote, leseni ya biashara ya Manispaa ya Singida pamoja na kibali cha polisi," alisema.

Mtanda alidai kuwa hali kama hiyo imekwamisha usafirishaji wa chuma chakavu katika mikoa ya Mwanza, Morogoro, Dar es Salaam na Arusha.

"Wenzangu katika mikoa kadhaa nao wamelalamikia hatua hiyo ya NEMC kuzuia usafirishaji wa chuma chakavu hadi tuwe na leseni mpya na hatua yao hiyo ni kinyume na maagizo ya Waziri," aliongeza mfanyabiashara huyo.

Alisema hatua hiyo itasababisha viwanda vya nondo kukosa mali ghafi ya kuzalisha bidhaa hizo.

Kwa upande wake mmoja wa wamiliki wa kiwanda cha chuma kilichopo Dar es Salaam aliyeomba asitajwe jina gazetini alisema hali ya upungufu wa malighafi ya kutengenezea chuma imeanza kujitokeza.

"Kwa wiki nzima tunapokea takribani tani 20 za chuma chakavu ambazo ni malighafi ya kuzalisha chuma za aina tofauti na kwa wiki moja sasa hatujapokea hata tani moja kutokana na zuio hilo la NEMC," alilalama.

Alisema iwapo suala hilo halitapatiwa ufumbuzi wa haraka inaweza ikapelekea viwanda vingi vya chuma kusitisha uzalishaji na hivyo kuathiri uchumi wa nchi kwa kiasi kikubwa na Watanzania wakakosa ajira.

Mmiliki huyo aliongeza kuwa hata mchakato wa kupata leseni mpya ya kuendesha biashara ya chuma chakavu umejaa urasimu kinyume kabisa na maagizo ya Rais John Magufuli, aliyotoa hivi karibuni kuwa vibali vya NEMC visiwe kikwazo kwa wafanyabiashara na wawekezaji.

Kwa mujibu wa NEMC mchakato wa kupata leseni mpya biashara ya chuma chakavu huchukua zaidi ya siku 27 kupatikana kukiwa na mlolongo wa masharti ya kufuata.

Akizungumzia suala hilo Mkurugenzi wa NEMC, Samwel Gwamaka, alithibitisha kuwapo kwa zuio lakini akaongeza kuwa lina wahusu wafanyabiashara wanaosafirisha chuma chakavu nje ya nchi na si wa ndani.

"Biashara hii ilikuwa inafanyika bila utaratibu, sasa tumeweka utaratibu mpya ambao tutautangaza kuanzia sasa," alisema.


Distributed via ippmedia

Ofisa Mradi wa Shirika la Maendeleo la Mwedo, Scolastika Porokwa, akitoa elimu kwa kundi la wanawake na vijana wa jamii ya kifugaji katika Kijiji cha Kimokoa, wilayani Longido, Mkoa wa Arusha mwishoni mwa wiki, kuhusu ufugaji wa kisasa. **PICHA: DANIEL SABUNI**

# Wanufaika asali waaswa uzalishaji zaidi

Na Zanura Mollel, LONGIDO

WANUFAIKA 75 wa mradi wa nyuki wa Kijiji cha Kitendeni kilichopo Kata ya Kamwanga wilayani Longido, wametakiwa kufanya miradi na kuzalisha kwa tija.

Aidha, wanufaika hao wametakiwa kutafuta soko la uhakika watakalouza asali hiyo badala ya kubweteka. Katibu Tawala wa Wilaya ya Londigo, Toba Nguvila, aliyasema hayo jana wakati akikabidhi miradi hiyo kwa wanufaika hao na kusema kipaumbele cha serikali ni kuwainua wananchi wenye hali ngumu ya kimaisha.

Aliwaambia kuwa kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf) serikali inashughulika moja kwa moja na kaya za watu maskini

"Pongezi kwa Tasaf Longido kwa kuwajali watu hawa. Mnatekeleza agizo la serikali ipasavyo," alisema Nguvila.

Aliwaambia hapo awali hali za wanufaika hao kabla hawajaingia kwenye mradi zilikuwa ni mbaya. Aidha, kupitia ruzuku hizo wameanza kuimarika na kuwaomba kuzitumia kwa manufaa ili kujikwamua kiuchumi kwani mpango huo utafika mwisho lakini familia zao zitaendelea kuishi.

"Wanufaika ni wengi naomba kubalini kubadilisha maisha yenu, kupitia ruzuku hizi mnazopewa, msiende kununua nguo, kunywea pombe wala kuoa wake wengine," alihimiza Nguvila.

Aliwaambia kuhusu mizinga hiyo wawe na subira maana wataelekezwa namna ya kuitumia ili kupata asali hivyo ana imani watazalisha asali bora itakayowaongezea kipato kwani watauza katika masoko makubwa ya ndani na nje.

Nguvila alimtaka mtaalamu wa nyuki kutoka halmashauri, kuwatembelea mara kwa mara wanufaika hao wa mizinga na kuwapa elimu, huku akikagua kama mizinga hiyo inafanya kazi iliyokusudiwa na kuchukua hatua.

"Watembeleeni hawa watu, soko la asali lipo Longido tuna miti mizuri yenye kuzalisha asali ambayo haipatikani duniani kote," alisema na kumtaka Ofisa Ushirika wa Halmashauri kushirikiana na vikundi hivyo, katika kuwafundisha na kuwaelimisha namna ya kuibua fursa hizo za kiuchumi ili waweze kuinuka na kupiga hatua kiuchumi.

Mratibu wa Tasaf Wilaya, Saruni Lobulu, alisema mizinga hiyo itakabidhiwa kwa vikundi vitano kati ya saba vilivyopo katika kijiji hicho ambavyo vipo kwenye mpango wa Tasaf.

Alifafanua kuwa mizinga 116 ina thamani ya Sh. milioni 26 na vikundi vitagawanywa kwa watu 75, ambapo kila kikundi kitapewa mizinga 15.

# Bodaboda zaanza kusajiliwa Moshi

**Na Mary Mosha, KILIMANJARO**

KATIKA jitihada za kukabiliana na uhalifu, polisi mkoani Kilimanjaro, imeanza kusajili wamiliki na waendesha bodaboda kwenye maeneo yote zinakotolewa huduma hizo.

Hatua hiyo imelenga kuwadhibiti na kuwatambua pamoja na kukabiliana na matukio ya uhalifu yanayodaiwa kufanywa na baadhi ya vijana ambao hawatambuliki.

Mchakato huo unaendelea katika vijiwe vyote, kwa mujibu wa Mkaguzi Msaidizi wa Polisi wa Mkoa, Hamad Hoza, aliyesema hayo wakati wa kukabidhi viakisi mwendo kwa vijana wa bodaboda.

Makabidhiano hayo yalifanyika mjini Moshi baada ya kampuni ya mbegu za mboga na matunda East West Seed kutoa vifaa hivyo kwa polisi.

Alisema kwa kusajili wamiliki na vyombo vyao polisi itapunguza mkanganyiko wakati inapopata ajali ili kujua wamiliki wa bajaji au pikipiki na namna ya kutatua changamoto hiyo kwa haraka.

"Tumeanzisha huu mfumo ili kuepukana na matukio ya kihalifu yanayotendeka hasa nyakati za usiku, lakini naomba waendesha bodaboda na wamiliki hakikisheni mikataba mnayoingia inaeleweka na kulinda masilahi ya mteja, dereva na mmiliki," alisema Hoza.

Akikabidhi viakisi mwendo hivyo, Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya East West Seed, Coen Everts, alisema wameamua kuwapa vijana hao ili kupungunza matatizo ya ajali barabarani hasa nyakati za usiku.

"Utafiti unaonyesha waendesha bodaboda wengi ni vijana ambao taifa linawategemea, lakini wanafanya kazi katika mazingira magumu sana hasa nyakati za usiku. Wengi wao hawana viakisi mwendo na kusababisha kugongwa na vyombo vingine barabarani na baadhi kupoteza maisha na hata kupata ulemavu wa kudumu," alisema Everts.

Aliwaambia kuwa pamoja na utoaji wa vifaa hivyo pia wanaunga mkono jitiada za Jeshi la Polisi kuwasajili vijana kwenye kila kijiwe ili kupungunza migogoro miongoni mwao na kupunguza matukio ya kihalifu.

Baadhi ya vijana akiwamo Eliangaza Msofe walisema kwa kufanya hivyo wataleta manufaa kwa vijana na hata kuaminika zaidi kwa wateja na kwenye taasisi za kifedha hasa wakati wa kuomba mikopo.

**"Utafiti unaonyesha waendesha bodaboda wengi ni vijana ambao taifa linawategemea, lakini wanafanya kazi katika mazingira magumu sana hasa nyakati za usiku...**

# Muro aanza kupenya Hai

**Na Godfrey Mushi, HAI**

DURU za kisiasa mkoani Kilimanjaro, zinamtaja Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, kuwa ameanza mikakati ya chini kwa chini ya kusaka ubunge katika Jimbo la Hai.

Muro ameanza kuonyesha nia ya kumng'oa Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe.

Mwishoni mwa wiki, Muro alianza kazi ya kusaka wapigakura watakaomuunga mkono katika uchaguzi mkuu ujao wa mwaka 2020, alipokwenda kuendesha harambee ya ujenzi na ununuzi wa vyombo vya muziki vya Kanisa la EAGT, lililopo Mungushi-Majengo wilayani Hai.

Kwa vipindi tofauti, Muro amekuwa akishiriki mambo mbalimbali yanayofanyika wilayani Hai, huku akitajwa kuwa miongoni mwa wagombea wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), wanaotafuta kutaka kupewa ridhaa na chama hicho kugombea ubunge.

Jimbo la Hai linaongozwa na Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni (KUB) ambaye ni Mwenyekiti wa Chadema Taifa, Freeman Mbowe.

Katika moja ya kurasa kwenye mitandao ya kijamii, Muro ameandika, mambo mbalimbali zikiwamo salamu na shukurani.

Aidha, aliandika: "Tunashukuru Mungu tumemaliza salama harambe ya ujenzi na ununuzi wa vyombo vya Kanisa la EAGT Mungushi Majengo, wilayani Hai.

"Namshukuru sana Mc Lameck (Simbo) na ndugu zangu Cedrick Pangani, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Hai na katibu wake Msaki, kwa kushirikiana pamoja."

...'Mtu kwao, wakati wetu, ufina nkenyi (mcheza kwao), Jerry Muro, Mkuu wa Wilaya ya Arumeru'.

Mchuano huo ulioanza chini kwa chini na kuimarika kwa CCM mkoani Kilimanjaro, unaifanya mikakati ya kuwania ubunge mwakani kwa pande mbili hizo upinzani na CCM kuwa kama vita.



Baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Kiterini, Kata ya Kahe Mashariki, wakifurahia ushindi dhidi ya ardhi ya mwenzao Benjamin Thomas (aliyeshika karatasi), baada ya kumbwaga mmoja wa wavamizi wa shamba la ekari moja, katika Mahakama ya Ardhi Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro mwishoni mwa wiki. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Serikali yatoa somo la kuondoa migogoro

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, amewataka wafugaji kupunguza wingi wa mifugo kwani ni moja ya mbinu za kumaliza migogoro ya ardhi baina ya wafugaji na wakulima.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, alisema ipo haja ya wafugaji wa mkoa huo kuanza kupunguza idadi ya mifugo yao kwa kuuza ikiwa ni njia mojawapo ya kukabiliana na migogoro ya kugombea maeneo ya malisho kati ya wafugaji na wakulima.

"Tunategemea kwamba mfugaji wa sasa atakuwa na mbinu nyingi za kuishi vizuri kupitia mazao yake ya mifugo hasa hasa maziwa ambayo ni chakula, lakini ni zao la biashara, wafugaji wetu wakifuata taratibu na maelekezo ya wataalamu, wanaweza kufika mbali kwa kupitia uuzaji wa maziwa. Najua bado hatujachelewa," alisisitiza Mghwira.

Aidha, alisema shughuli za kilimo na ufugaji nchini zimeingia katika mageuzi ya kiteknolojia, hivyo mabadiliko hayo hayapaswi kuwafanya wabweteke na kuendelea kufuga kienyeji.

Mbali na kufurahishwa na maendeleo ya sekta ya maziwa, mkuu huyo wa mkoa alisema kuna haja ya jamii za kifugaji pia kuanza kufuga kisasa.

Alisisitiza kuwa ni lazima kupunguza idadi ya makundi makubwa ya mifugo ambayo yamekuwa yakiharibu mashamba ya wakulima na kusababisha migogoro ya mara kwa mara.

Mkuu huyo wa mkoa alisisitiza: "Viongozi wa vijiji, nataka waandae mpango mkakati wa kuisaidia jamii za wafugaji kuwa na shughuli mbadala za kuwaingiza kipato. Ninyi wafugaji fikirieni kupunguza sehemu ya mifugo yenu na kubakisha idadi ndogo ya mifugo, kwa sababu ongezeko la watu limesababisha ardhi kuwa finyu na haitoshi kwa malisho na kilimo."

Katika mahojiano na Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji wa Ng'ombe wa Maziwa Mwika (Mwidefu), Freckson Mlay, kuhusu ushauri wa kupunguza mifugo, alisema ni hatua muafaka.

Aliongeza kuwa gharama kubwa za malisho na kipato duni cha baadhi ya wafugaji ni chanzo cha tija ndogo kwa wafugaji wa ng'ombe wa maziwa.

Kwa mujibu wa Mlay, tafiti zinaonyesha malisho duni ya mifugo ndiyo yanayosababisha kushuka kwa uzalishaji wa maziwa.

"Tija ndogo kwa wafugaji wa ng'ombe wa maziwa katika ngazi ya kaya inasababishwa na gharama kubwa za lishe na uelewa finyu wa mbinu endelevu za ufugaji."

Alisema kwa wastani, ng'ombe wa maziwa wa Tanzania, wapo wanaozalisha lita tano za maziwa kwa siku, ikilinganishwa na nchi nyingine duniani ambazo ng'ombe anatoa lita 30 kwa siku na hivyo kutoa tija kubwa kwa wafugaji.

Nipashe
# TESA
Jumanne Oktoba 29, 2019
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 18

## Wanasayansi wanachunguza jinsi saratani 'inavyozaliwa'



Ukurasa 18

## JE, WAJUA?

Mabadiliko ya tabianchi yatishia amani Somalia?



Ukurasa 17

## Ukoloni uliwadhalilisha mama wanene- Mhadhiri



# Kahama yakabili changamoto zinazokwamisha wanafunzi wa kike

Ukurasa 16

## ELIMU KUTOKA POLISI

# Pundamilia (Zebra crossing) ziheshimike




Mwanafunzi akiongoza wanafunzi wenzake kuvuka barabara kwenye alama ya pundamilia. **PICHA: JESHI LA POLISI**

KUMEKUWAPO na tabia kwa baadhi ya madereva wa vyombo vya usafiri kutoheshimu uwepo wa matumizi ya alama za pundamilia (zebra crossing) na kutosimama kama sheria inavyoelekeza jambo linalosababisha kutokea kwa ajali zinazoweza kuepukika.

Nianze kwa kuwatazama wanafunzi hususani katika jiji la Dar es Salaam.

Miaka kadhaa iliyopita Kikosi cha Usalama Barabarani Makao Makuu, kilianzisha utaratibu kwa baadhi ya maeneo ya jiji la Dar es Salaam kwa wanafunzi kutumia vibao maalum kusimamisha magari maeneo yenye alama za pundamilia (zebra crossing).

Lengo la kuanzishwa kwa utaratibu huo ni kusaidia wanafunzi waweze kuvuka barabara kwa urahisi na bila hofu ya kugongwa na magari.

Nimekuwa nikishuhudia maeneo mengi wanafunzi wakipokezana kutumia kibao hicho kusimamisha magari ili wanafunzi wenzao waweze kuvuka.

Utaratibu huu wa vibao maalum wanavyotumia wanafunzi kusimamishia magari kwenye alama za pundamilia (zebra crossing) ni mzuri kwa sababu unasaidia hata wananchi wengine wenye hofu ya kuvuka katika alama hizo kwa urahisi.

Alama ya pundamilia (zebra crossing) ina sheria inayoisimamia ambayo inaeleza wazi kuwa:

"Dereva atasimamisha gari lake mpaka ahakikishe watembea kwa miguu wote wanaovuka kivuko cha pundamilia wamevuka.

Aidha, Dereva atalazimika kusimama katika kivuko cha waenda kwa miguu (zebra crossing) kwa dakika moja hata kama kwa kipindi hicho hakuna mtembea kwa miguu yeyote anavuka kivuko hicho.

Muda wote huo itamlazimu dereva kuwasha indicator zake zote za kulia na kushoto." Zebra Crossing Act. namba 568 volume II reversed version No. 2 article III publication of 2017.

Mwanasheria wa Kikosi cha Usalama Barabarani Makao Makuu, Mrakibu Msaidizi wa Polisi (ASP) Sokoni anabainisha kuwa:

"Yeyote atakayekiuka sheria hiyo adhabu yake ni Kifungo cha miezi mitatu au faini ya Sh. 30,000 au kunyang'anywa leseni kwa muda wa mwaka mmoja au vyote kwa pamoja."

Sheria hiyo inafahamika hata na watembea kwa miguu.

Binafsi nimeshuhudia watembea kwa miguu wakisimama kwa muda mrefu kusubiri kuvuka na labda atokee askari, dereva mwenye busara ama mwananchi mwenye ujasiri wa kusimamisha gari ili kuruhusu watembea kwa miguu hao wavuke.

Distributed via ippmedia

Msomaji, fanya utafiti japo wa dakika 10 tu kwenye maeneo yenye mkusanyiko mkubwa wa watu na ujaribu kutazama namna wananchi wanavyovuka kwa hofu kwenye alama za kuvukia (zebra crossing).

Wengine wanadiriki hata kuomba kuvushwa kwa hofu ya kugongwa na magari.

Hii inanionyesha ishara kwamba, utii wa sheria za usalama barabarani ni tatizo, kwani kama sehemu ndogo ya zebra crossing inatupa tabu, ni wazi kuwa maeneo mengine yana tatizo la ukiukwaji wa sheria za usalama barabarani kwa kiasi kikubwa.

Nitoe mfano mdogo wa Barabara ya Kilwa ambayo napita kila siku nikienda kazini.

Kuna zebra crossing kituo cha JKT na Ufundi, kila asubuhi lazima nikute askari anasimamisha magari kusaidia wanafunzi na wananchi wengine kuvuka barabara wakati alama za kuvukia zipo na zinafahamika.

Maswali yangu kwa wanaotumia vyombo vya moto, je, Kuna haja ya wanafunzi kutumia vibao maalum kuwashurutisha madereva kusimama ili wavuke kwenda shule?

Na je Kuna sababu ya kuweka askari kuwashurutisha madereva hata kwenye zebra crossing?

Madereva mnapaswa kubadilika na msiwe chanzo cha kuwatia hofu watembea kwa miguu pindi wanapovuka barabara.

Alama hizo zimewekwa kisheria, ni eneo ambalo mtembea kwa miguu anapaswa kuvukia barabara bila hofu kwasababu ndio eneo lake la kujidai kisheria.

Shime madereva badilikeni fuateni sheria, kanuni na taratibu za usalama barabarani ili kuokoa maisha yenu na watumiaji wengine wa barabara.

***Imetolewa na;***
***Kitengo cha Uhusiano***
***Makao Makuu ya Jeshi la Polisi.***
***S.L.P 9141***
***Dar es Salaam***
***Baruapepe habariphq@yahoo.com, habari.phq@tpf.go.tz***



## TUJIFUNZE KISWAHILI

**BARNABAS MARO**
marobarnabas@yahoo.com

# Jawabu wakatiwe na wakatiwe si zani

'ZANI' ni fujo au ghasia. Maana yake kila jawabu au jibu huwa na wakati wake na ufikapo huwa halisababishi fujo au mabishano yoyote.

Methali hii yatufunza umuhimu wa kusema mambo wakati unaofaa na wakati yanapoweza kukubalika bila ya kuleta mabishano.

Siku hizi kuna maneno mengi ya kihuni yanayozungumzwa mitaani kisha waandishi wa magazeti, redio na runinga kuyatumia kwenye vyombo vyao vya habari. Ni kama maneno hayo yamepata ithibati (kitu au muhuri unaodhihirisha ukweli; uthibitisho) ya Bakita.

Nimeandika mara nyingi kuhusu upotoshwaji wa maneno ya Kiswahili lakini ni kama kumpigia mbuzi gitaa! Atakuangalia tu huku akicheua* na kutafuna majani yake.

*Cheua ni tapika kama vile mtoto baada ya kushiba maziwa; kitendo cha kurudi/kurudisha chakula mdomoni kutoka tumboni; bweuka. Pia ni kipande cha nazi kilichokunwa na kubakishwa; kihanu.

'Cheu' ni mnyama anayecheua kama pundamilia, ng'ombe, nyati, mbawala, paa, kulungu, mbuzi, kondoo, swala/swara, (wasemavyo ndugu zetu wa Zanzibar) nyumbu, kiboko, ndovu, ngamia n.k.

'Chewa' ni neno litumikalo kwa maamkizi ya asubuhi; pepo za asubuhi zinazovuma kutoka mashariki. Pia ni aina ya samaki mkubwa wa rangi ya kijivujivu mwenye kichwa kikubwa na mdomo mpana.

Soma makala ifuatayo inayohusu jengo la Kim na Kanye West nchini Marekani. Kichwa kidogo kimeandikwa 'BATA BATANI' kwa herufi kubwa kama nilivyoandika.

'Bata'ni ndege mkubwa kuliko kuku, anayeishi porini au anayefugwa, mwenye vidole vilivyounganishwa na vigozi vyembamba vinavyomwezesha kuogelea. 'Bata bukini' ni bata mkubwa mweupe anayependa kula ukoka. 'Bata mwitu' ni bata asiyefugwa anayeishi karibu na maji. 'Bata mzinga' ni bata asiye na manyoya kichwani na shingoni. Sipati maana ya 'batani.'

'Meno' ni wingi wa 'jino.' Ni kitu cheupe kama mfupa, kigumu kilicho katika kinywa cha mtu au mnyama ambacho hutumika kutafunia chakula.

'Pembe' ni kitu kigumu chenye uwazi ndani ambacho huota katika kichwa cha mnyama kama mbuzi au ng'ombe; kitu chenye uwazi ndani na tundu nchani ambacho kikipulizwa hutoa sauti yenye ujumbe maalumu; baragumu. Pia ni mahali panapokutana na ncha au kingo za vitu viwili au zaidi; bangili za plastiki.

'Mkonga' ni kiungo kirefu chenye uwezo wa kupindapinda kilicho mbele ya uso wa tembo anachokitumia kushikia vitu. 'Mwiro' yaani mkonga wa tembo anaoutumia kama mkono wake.

Baada ya kufafanua na kueleza maana ya 'meno', 'pembe' na 'mkonga', je, ni sahihi pembe za ndovu kuitwa 'meno ya ndovu' kama isemwavyo mara kwa mara ilhali pembe zina kazi tofauti kabisa na meno?

Paragrafu ya pili ya gazeti fulani liliandika: "ZFF, wamempa shavu Morocco ndani ya kikosi hicho kinachotarajiwa kushiriki michuano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA) Senior Challenge Cup 2019, itakayofanyika nchini Uganda mwishoni mwa Novemba mwaka huu."

'Shavu'ni minofu iliyoko upande wa kulia na kushoto kwenye uso wa mtu. Pia ni kiungo anachotumia samaki kuvutia pumzi. Inapoandikwa "ZFF wamempa shavu Morocco" ina maana mtajwa hakuwa na shavu la upande mmoja? Waandishi wanapaswa kuandika maneno halisi badala ya kutumia maneno ya kihuni yenye maana tofauti na maudhui (wazo linaloelezwa katika maandishi au katika kusema).

Yaelekea mwandishi aliandika habari hii baada ya kutafsiri haraka haraka kutoka Kiingereza bila kurudia kuisoma kama inaeleweka au la. Matokeo yake haieleweki! Je, haikupita kwa wanaodusu (wanaosoma kwa makini kusahihisha) ili habari hiyo ieleweke? Mhariri wa michezo nae hakuipitia?

Gazeti la fulani la michezo lilikuwa na kichwa cha habari: "MZIKI MNENE Simba kikitoka kitu, kinaingia kitu buana." Lugha ya Kiswahili haina neno 'mziki' bali kuna 'muziki' na maana yake ni mpangilio wa sauti za vinanda zinazoimbika; mdundo unaotokana na mseto wa sauti za ala za muziki kama ngoma, tarumbeta, kinanda n.k. pamoja na uimbaji. Badala ya kuandikwa 'mziki mnene' ingeandikwa 'muziki mzito.' Hata hivyo Simba haichezi muziki bali hucheza kandanda.

'Kitu' maana yake ni jambo, mali au fedha, mnyama mweusi wa jamii ya paka na chochote ambacho si mtu au mnyama. Kuhusu 'buana' ni yaleyale ya waandishi kubadili lugha halisi ya Kiswahili na kuingiza maneno ya kihuni yazungumzwayo mitaani! Twajenga au twabomoa? 'Mtu' ni kiumbe hai chenye uwezo wa kimaumbile wa kuchagua na kuamua; binadamu, mja. Kwa hiyo hawezi kufananishwa na kitu.

Kitendo cha kufanya kazi ovyoovyo.

**Methali: Anayejitahidi hufaidi.**

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

TEKNOLOJIA

NA DANIEL SABUNI, ARUSHA

# Ifahamu Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania

TUME ya Nguvu za Atomiki Tanzania ni chombo cha serikali kilichoanzishwa mwaka 1983 na kujulikana kama Tume ya Taifa ya Mionzi (NRC) kwa lengo la kuwakinga Watanzania na madhara yanayoweza kusababishwa na mionzi.

Tume hiyo ilianzishwa baada ya kuona umuhimu wa vifaa vinavyotumika kuchunguza afya na matibabu kama 'X-ray' na mashine za ukaguzi wa watu na mizigo katika maeneo nyeti, vikitumika vibaya vinaweza kusababisha magonjwa kama saratani na kusababisha vifo.

NRC kwa wakati huo ilianzishwa kwa sheria ya Bunge Na. 5 ya Mwaka 1983, kutokana na kutokuwapo kwa chombo cha kudhibiti matumizi salama pamoja na matumizi hayo kuwapo kwenye baadhi ya sekta zikiwamo za afya

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa (TAEC), Peter Ngamilo anasema tangu wakati huo, Tume hiyo ilipanua shughuli zake nchini na kubadilisha muundo wake hasa utendaji wa shughuli muhimu na kufanikisha kuzaliwa kwa Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC), mwaka 2003 kwa sheria Namba 7 ya Bunge na kupewa mamlaka kisheria ya kusimamia na kudhibiti kwa niaba ya serikali matumizi salama ya mionzi nchini.

Lakini kuhamasisha na kuendeleza matumizi salama ya teknolojia ya nyuklia pamoja na kufanya utafiti na kutoa ushauri na taarifa mbalimbali kwa serikali kuhusu sayansi na teknolojia ya nyuklia.

Ngamilo anasema serikali imejenga maabara ya kisasa kwa ajili ya kusimamia na kudhibiti matumizi salama ya mionzi, iliyokamilika mwaka huu (2019) na kugharimu Sh. bilioni 2.6, ambayo itasaidia kufanya utafiti wenye hadhi ya kimataifa kwa kushirikisha vyuo vikuu, taasisi za utafiti na viwanda.

"Ndani ya jengo la maabara hiyo kuna vifaa vya kisasa vyenye thamani ya Sh. bilioni 2.5, vifaa hivi mbali ya kutumika katika kufanikisha shughuli za kisayansi na kitafiti, pia vinatumika kutoa kinga bora ya mionzi katika huduma za uchunguzi na tiba ya mionzi kwa wagonjwa na jamii," anasema.

Pia, kupitia uratibu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia chini ya Tume ya Nguvu za Atomiki, Tanzania imefanikiwa kupata vifaa vya maabara pamoja na vifaa tiba vyenye thamani ya Sh. bilioni 6.2 kutoka Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki Duniani (IAEA).

Vile vile, TAEC kupitia wizara hiyo katika kipindi cha miaka minne imefanikisha upatikanaji wa mashine za tiba ya saratani kwa njia ya mionzi zenye thamani ya Sh. bilioni 2.4 katika Hospitali ya Bugando ili kusaidia kutoa huduma ya tiba ya saratani kwa wananchi wa Kanda ya Ziwa ambao hufuata matibabu ya aina hiyo katika Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, jijini Dar es Salaam.

Mashine hizo zilipatikana kwa msaada wa Serikali ya India kupitia ubalozi wake hapa nchini na IAEA.

Mashine nyingine zaidi kutoka IAEA zikiwamo za kupangilia mfumo wa tiba (Treatment Planning System-TPS) zinatarajiwa kuwasili wakati wowote.

Msemaji huyo wa TAEC anasema Tume ya Nguvu za Atomiki ina dira ya kuwa kituo bora katika kusimamia na kuendeleza matumizi salama ya teknolojia ya nyuklia Afrika.

"Lengo kubwa la TAEC ni kusimamia na kudhibiti matumizi salama ya mionzi ili kulinda umma, wafanyakazi, pamoja na mazingira dhidi ya madhara ya mionzi na kuhamasisha matumizi salama ya teknolojia ya nyuklia kwa maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi," anasema.

Mkuu huyo wa Kitengo cha Mawasiliano wa TAEC yenye makao makuu Njiro, mkoani Arusha, anasema katika kipindi cha miaka minne, usimamizi na udhibiti wa mionzi nchini umeendelea kuboreshwa kwa TAEC kufanikiwa kufungua ofisi katika maeneo mbali mbali nchini ikiwamo Dar es Salaam, Horohoro, Holili, Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), Kabanga (Ngara) Kigoma na Kilambo (Mtwara), na Kasulumu (Mbeya).

Ofisi nyingine ni Mwanza, Mtambaswala (Mtwara), Mtwara, Mutukula (Kagera), Namanga (Arusha), Pemba, Rusumo (Kagera), Sirali (Mara) Tunduma (Songwe), Tanga, Tarakea Kilimanjaro na Zanzibar.

Teknolojia ya Nyuklia nchini hutumika katika maeneo mbalimbali kwa manufaa ya nchi kama kupima unene wa vyuma au mabati viwandani, kuhakiki ubora wa maungio katika vyuma kama vile madaraja na matangi ya mafuta.

Pia, kupima ujazo wa bidhaa za viwandani za vimiminika kama soda, bia na maji, kuhakiki ubora wa ujenzi wa barabara na majengo, kufanya uchunguzi wa saratani na kutibu saratani pamoja na kutafuta vyanzo vya maji.

TAEC pia ina matarajio ya kuanzisha mradi wenye kutumia teknolojia ya mionzi katika kuhifadhi vyakula visiharibike mapema, katika kuitikia sera ya kilimo kwanza na sera za viwanda.




Ofisi za Makao Makuu ya TAEC, Njiro, jijini Arusha. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



Baadhi ya mitambo katika maabara ya kisasa ya Tume iliyofungwa kwa ajili kusimamia na kudhibiti matumizi salama ya mionzi ambayo iliyokamilika mwaka huu.

> "Lengo kubwa la TAEC ni kusimamia na kudhibiti matumizi salama ya mionzi ili kulinda umma, wafanyakazi, pamoja na mazingira dhidi ya madhara ya mionzi...

ELIMU

NA SHABAN NJIA, MBOGWE

# Kahama inavyokabili changamoto zinazokwamisha wanafunzi wa kike



Wanafunzi wa kike, kidato cha nne, Shule ya Sekondari Masumbwe, wakiwa wameshikilia taulo za kike.

KUNA changamoto mbalimbali zinazowakabili watoto wa kike katika jamii, hasa za wafugaji katika dhima nzima ya kupata elimu.

Mojawapo ya changamoto hizo ni ile ya kuchukuliwa kama kitega uchumi ama chanzo cha utajiri kwa familia na zaidi zilizo maskini.

Kwamba hata kama familia ni maskini, inapokuwa imezaa mtoto wa kike, inakuwa na matumaini kuwa hali hiyo inaweza ikabadilika wakati wowote, yaani ni suala la muda tu, ng'ombe ambazo ni ishara ya utajiri kwa baadhi ya jamii zinaweza 'kumwagika' wakati wowote.

Na ndiyo maana watoto wengi wa kike katika jamii hizo bado wananyimwa fursa ya kuendelea na masomo, kipaumbele kikitolewa kwa watoto wa kiume, kwa imani kwamba ndio walio nguzo za kaya na hivyo jamii kwa ujumla wake.

Aidha, mtoto wa kike katika baadhi ya jamii ananyimwa fursa ya masomo kutokana na dhana kwamba, akipata elimu na kuolewa, faida itakuwa ni kwa familia ilikoolewa.

Na ndiyo maana nyakati zingine kumekuwa na taarifa kutoka maeneo mbalimbali nchini zikizinyonyea mkono baadhi ya familia zinazodaiwa kuhamasisha watoto wao wa kike wasifanye vizuri katika mitihani yao ya mwisho, hata kama uwezo wa kimasomo wanao kwa kisingizio kwamba hawana fedha za kuwasomesha.

> Wapo wanaoshindwa kuhudhuria shule katika kipindi cha hedhi kwa kuogopa kuchekwa... wanafunzi wa kike kwa mfano wanaosoma shule za sekondari zilizo pembezoni mwa miji wamekuwa wakikosa masomo.



Mkuu wa Chuo cha Saint Joseph College Shinyanga, Miraji Zahoro Chomoka (kushoto), akigawa taulo za kike kwa wanafunzi wa kidato cha nne shule ya Sekondari Masumbwe, Halmashauri ya Mbogwe kama moja ya njia za kukabiliana na changamoto za kukosa masomo. **PICHA ZOTE: SHABAN NJIA.**

Hata hivyo, ukiziweka pembeni jamii za wafugaji zinazoendekeza mtazamo huo kuna makabila ambayo yamejitahidi kupeleka watoto wa kike shuleni, lakini bado wanakatisha masomo yao kwa sababu mbalimbali zikiwamo mimba, ugumu wa maisha na kujitafutia ridhiki za kiuchumi.

Vilevile wapo watoto wa kike wanokosa masomo katika baadhi ya siku, pindi wanapoingia katika siku zao za hedhi.

Hili huwaathiri zaidi wanafunzi wanaotoka katika familia zilizo pembezoni, ambazo kimsingi hazina uwezo wa kuwapatia taulo za kike, ambazo ni za gharama.

### DC KAHAMA

Changamoto hizi kwa watoto wa kike ndizo zinamfanya Mkuu wa wilaya ya Kahama, Anamringi Macha, kuja na msimamo thabiti akilenga kuhakikisha wanaipata haki yao hiyo ya msingi ya kupata elimu bila mawaa.

Pamoja na mengine, Mkuu huyo wa wilaya anasimama katika ile dhana kwamba, ukimuelimisha mtoto wa kike umeielimisha jamii lakini na taifa kwa ujumla.

"Lakini ninalenga kuhakikisha kwamba wanafikia ndoto zao za kimaisha na taifa linapata viongozi na wataalamu wa kada mbalimbali zilizo muhimu kwa maendeleo ya nchi," anasema.

Akiwa kwenye kikao cha Baraza la Madiwani katika Halmashauri ya Msalala, anaelekeza kwamba mzazi katika wilaya yake atakayemshawishi mtoto wake wa kike kufanya vibaya kwenye mitihani yake, atachukuliwa hatua za kisheria.

"Tunajiwekea jukumu la kufuatilia mwenendo wa masomo ya mtoto wa kike kuanzia darasa la kwanza mpaka la saba na akibainika alikuwa akifanya vizuri shuleni na amefeli, mzazi atawajibika kisheria," anasema na kuongeza:

"Serikali haiwezi kutekeleza wajibu wake wa kusomesha watoto bure, halafu inakuwa na mzazi anayemtaka mwanaye asifanye vizuri kwenye mtihani wake wa mwisho...hili limekuwa likijitokeza mara kwa mara na asilimia kubwa wanaofanya hivyo huwa ni kwa wanafunzi wa kike."

Distributed via ippmedia

Akizungumzia takwimu za waliohitimu darasa la saba katika wilaya hiyo mwaka huu, Macha anasema kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Kahama ilikuwa na zaidi ya watahiniwa 16,000, huku Halmashauri ya Msalala ikiwa na watahiniwa 4,000.

Na ndiyo maana akawasisitizia madiwani katika kikao hicho kuhakikisha wanahamasisha wananchi kujenga vyumba vya madarasa ili wanafunzi waliofaulu waweze kuchukuliwa wote.

### WADAU WENGINE

Mkuu wa Chuo cha Saint Joseph College Shinyanga, Miraji Zahoro Chomoka, anazungumzia changamoto zinazokwamisha watoto wa kike kufikia ndoto zao kielimu, akijikita namna changamoto ya hedhi inavyochangia.

Anasema watoto wa kike wanashindwa kufanya vizuri kwenye mitihani yao ya mwisho kutokana na baadhi yao kukosa taulo za kike na mahitaji mengine yanayoambatana na kipindi hicho.

"Wapo wanaoshindwa kuhudhuria shule katika kipindi cha hedhi kwa kuogopa kuchekwa...wanafunzi wa kike kwa mfano wanaosoma shule za sekondari zilizo pembezoni mwa miji wamekuwa wakikosa masomo," anasema na kuongeza:

"Hukosa masomo wakati wakiwa kwenye siku zao kutokana na ukweli kwamba, wengi hawapati taulo za kike na hivyo kujikuta wakitumia vitambaa, magazeti, tishu au soksi ambazo si salama kiafya, hali inayochangia kufanya vibaya katika mitihani yao ya mwisho."

Akitoa takwimu za kimasomo za namna sababu hiyo ilivyo na athari, Chomoka anasema tatizo la hedhi kwa wanafunzi wa kike bado linasababisha wakose masomo kwa zaidi ya siku 50 hadi 60 kila mwaka, hivyo kudidimiza ufaulu wao ikilinganishwa na wanafunzi wa kiume.

### SULUHU

Ili kukabiliana na changamoto hiyo Chomoka anasema wameanzisha utaratibu wa kugawa taulo za kike kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari, katika mikoa ya Shinyanga na Geita.

Mkuu huyo wa chuo anasema lengo la hatua yao hiyo ni kuweka uwiano wa ufaulu kwa wanafunzi wa kike na wa kiume, kwa sababu kwa hivi sasa wanafunzi wa kiume wamekuwa wakifanya vizuri kuliko wa kike katika ujumla wake.

Anabainisha kuwa watoto wa kiume wanafanya vizuri kwenye mitihani yao ya mwisho, kwa sababu ya kutokuwa na changamoto kama walizonazo wenzao wa kike.

"Kwa sababu tumeanzisha utaratibu wa kugawa taulo za kike kwa watoto wetu, ninawataka basi wasiendelea kutumia vitambaa, magazeti, tishu au toilet paper, ambavyo ni hatari kwa afya zao," anasema.

Aidha, ana ushauri kwa wanafunzi wa kike watakaoingia kwenye siku zao zaidi ya siku nne hadi tano. Anawashauri wafike kwenye vituo vya afya ili kutambua tatizo ni nini, kwani mzunguko wa kawaida wa mwanamke huwa ni siku tatu.

### WALIMU

Zahara Abdallah ni Makamu Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekodari Masumbwe, iliyo katika Halmashauri ya Mbogwe.

Anasema katika jitihada za kupambana na changamoto ya wanafunzi wa kike kuendelea kukosa masomo pindi wanapoingia katika siku zao, wamekuwa wakiwapata elimu namna ya kukabiliana na changamoto hiyo.

"Mojawapo ya elimu ni ile ya kutoa taarifa kwa mwalimu wa kike pindi wanapopata mabadiliko ya kimwili ili kuangalia namna ya kukabiliana na suala hilo wasikose masomo," anasema na kuongeza:

"Pia tumekuwa tukiwanunulia taulo za kike wanafunzi kupitia fedha za dawa baridi zinazotolewa na serikali na huwapa pindi wanapoingia kwenye siku zao."

Hata hivyo, Mwalimu Zahara anakiri kwamba asilimia kubwa ya wanafunzi ni waoga kutoa taarifa pindi wanapoingia katika siku zao ili ofisi iweze kuwahudumia na hatimaye waendelee na masomo.

Anasema katika shule yake, kuna wanafunzi wa kike 908, hali inayowawia vigumu kumpatia kila mmoja wao taulo ya kike na ndiyo maana wanaendelea kupata misaada hiyo kutoka mashirika mbalimbali yasiyo ya kiserikali.

### WANAFUNZI

Akizungumza kwa niaba ya wenzake, mwanafunzi Sabi Malima wa kidato cha nne katika shule hiyo ya Masumbwe, anakiri kuwa wanakosa masomo wakati mwingine kwa kukosa taulo za kike.

"Hivyo huwa tunalazimika kukaa nyumbani hadi pale mtu unapomaliza siku zako na ukirudi shuleni unakuta wenzako wako mbele kimasomo," anasema.

---

HAKI, UWAJIBIKAJI & VITA YA RUSHWA

# Ukoloni uliwadhalilisha mama wanene- Mhadhiri

**Carlifornia,** Marekani



Sabrina Strings, Mhadhiri Msaidizi katika Chuo Kikuu cha California, Marekani. **PICHA: MTANDAO.**

KUNA watafiti waliofanya kazi zao na kueleza walichobaini, kwamba dhana ya unene ilivyohusishwa kwa muda mrefu na ubaguzi, hasa kuhusu urembo wa kinamama.

Inaelezwa hata kabla ya kuzagaa matangazo ya mitindo kushabikia watu wembamba, ukoloni ulishaingia katika mtazamo wa kuchukizwa na umbo la unene wa kinamama.

Ukoloni ulipochukua nafasi rasmi duniani, kunaelezwa kuliibuka fikra nyingi kama kigezo cha kuwazidi nguvu watu wengine na mojawapo ilikuwa imani iliyokuwapo kuhusu watu wanene na jamii ndogo zisizo na weupe.

Sabrina Strings, ni Mhadhiri Msaidizi wa masuala ya kijamii, katika Chuo Kikuu cha California, na mwandishi wa kitabu "Fearing the Black Body: The Racial Origins of Fat Phobia anaeleza kuwa waandishi, wanahabari watangazaji katika zama za ukoloni, walifananisha unene na kitisho, uvivu na udhaifu wa tabia.

Anasema, unene katika jamii za Magharibi mara nyingi hadi sasa wanahusishwa na tabia za upole au kuzubaa.

Mwanahistoria wa Marekani, Christopher Forth, anasema muda wa mageuzi ya kuchukizwa na unene ulianza mapema mwishoni mwa karne za 18 na 19, wakati ulipozidi kuhusishwa na hamu, pia starehe zisizo za kiungwana na waandishi katika Falme za Uingereza na Ufaransa, katika hilo walichukulia kuwa utamaduni usio wa kwao Magharibi.

"Zilivutiwa na walichokiona kuwa raia yoyote wa Ulaya angelikichukulia kuwa ni watu wanaotisha, wasio na afya na wanaosababisha kichefuchefu," anasema Forth.

Wasafiri waliotoka Ulaya kwenda Afrika Kaskazini na Magharibi, walieleza namna wanawake walivyonenepeshwa tayari kuozeshwa kiasi cha wao kushindwa kutembea.

Waturuki, jamii za Eskimo na Aborigine kutoka Australia, Wachina na Wahindi waliwachukulia jamii ya kuwa wanene kwa namna tofuati na hisia zao. Ilihofiwa kwamba, raia wa Ulaya waliozuru maeneo hayo walikuwa katika hatari ya kuwa wanene na kupanuka kwa falme za Uingereza na Ufaransa, kulichangia watu kuongeza ulaji na kupanuka viuno na matumbo.

Kwa mujibu wa Forth, wanaume wa Uingereza walipata sifa kwamba wana vitambi na wageni waliofika Uingereza kutalii walitumai kuwaona wanaume wa Kiingereza wanene

Pia, historia inatamka katika miaka ya 1850, miili ya watu walio wastani na wenye nguvu kama wanamichezo, ndio iliyovutia nchini Ufaransa na Uingereza.

Fikra iliyokuwepo katika jamii za Ulaya ni kwamba, watu katika jamii waliokuwa 'wenye busara'ni waliokula chakula kidogo na kuwa na miili ya wastani,

"Halafu tulikuwa na jamii za rangi tofauti na hususan Waafrika ambao walipenda ngono, chakula na kutokana na hilo walinenepa, " anasema mwandishi Strings.

Anaongeza:"Ni mpaka wakati wa kuanza biashara ya utumwa na kuzuka kwa sayansi ya rangi, ndipo jamii ya watu wasiotoka mataifa ya Magharibi, walipochukuliwa kuwa tofuati katika jamii, kwa misingi ya tofauti ya miili na tabia zao, ikilinganishwa na watu wa rangi nyingine."

Anaeleza kwamba, wakati watu wa mataifa ya Magharibi walipoanza kuona jamii za watu wenye rangi tofauti kama suala la utafiti, walianza kuwachukulia kama 'kiburudisho' na kuwakejeli Mojawapo ya mifano inayowataja kuabishwa kwa watu wanene, ni jamii ya Khoikhoi kutoka Kusini mwa Afrika,-wanaoelezwa kwamba waliheshimu makalio makubwa ya wanawake wao.

Tukio mojawapo ni mwanamama Sarah Baartman, aliyetoka Kusini mwa Afrika, anayeelezwa kuzungushwa hadharani katika maonyesho katika miji ya London, Uingereza na Paris,Ufaransa katika karne ya 18 na akapata kinachoitwa 'umaarufu' duniani, kupitia udhalilishaji.

Inadaiwa alipelekwa Ulaya kwa kudanganywa na daktari wa Uingereza kwa hoja ya kutibiwa, lakini alipofika huko, alizungushwa katika maonyesho huku umati ukikaribishwa kumtazama, pia kumgusa makalio yake.

Mama huyo alifariki mwaka 1815, lakini ubongo, mifupa ya mwili wake na sehemu zake miili yake zilionyeshwa katika jumba la ukumbusho Paris hadi mwaka 1974. Ni makumbusho yanayohusiana na unyanyasaji wa kikoloni na ubaguzi wa rangi.

Mhadhiri Strings anaamini kuwa unene 'haupongezwi au 'haushutumiwi' na umeshikana na rangi ya mmiliki wake.'Pia, rangi sio suala pekee la kufafanua aibu dhidi ya unene .

Inaelezwa, kadri muda ulivyosogea, unene ulihusishwa na weusi na kutisha, na wembamba ukapendelewa na wanawake wenye asili hasa wa Ujerumani na England.

Kwa hiyo, anajumuisha zama za aibu dhidi ya unene imekuwepo kabla ya utawala wa mataifa ya Ulaya na yalisaidia kushinikiza fikra na ubaguzi wa rangi ulioacha kovu baya.

## JE, WAJUA?

# Mabadiliko ya tabianchi yatishia amani Somalia?



Baadhi ya raia wa Somalia. **PICHA: MTANDAO.**

UCHUNGUZI mpya uliofanywa na Taasisi ya utafiti wa masuala ya amani duniani (SIPRI), umeonyesha mabadiliko ya tabianchi yanatishia kuleta changamoto kubwa kwa walinda amani wa sasa na baadaye nchini Somalia.

Ripoti hiyo inasema mabadiliko ya tabianchi yanaongeza changamoto zinazochangia kuimarika kwa makundi ya itikadi kali.

Miongo mitatu ya mzozo nchini humo imelipeleka taifa hilo kukabiliwa na ongezeko la ukame mkali. Matokeo ya mabadiliko ya tabianchi na yanayohusiana na hali ya hewa pia yanaongeza shinikizo kwenye mifumo iliyoelemewa ya kiutawala na Mahakama ya nchini humo.

Kulingana na ripoti hiyo, kitisho hiki ni kikubwa dhidi ya mchakato wa ujenzi wa taifa hilo, pia kizuizi kikubwa kwa Ujumbe wa Amani wa Umoja wa Mataifa nchini humo (UNSOM), katika kutekeleza majukumu yake kwa mafanikio.

Ripoti hiyo vilevile imegundua kuongezeka kwa visa vya mafuriko, ukame na njaa, kumeruhusu wanamgambo wa al-Shabaab kutumia mwanya huo kujionyesha kama wanaoweza kuisaidia jamii kuliko UNSOM.

Huu ni mkakati wao mpya, tofauti na awali ambapo waliwazuia watu kuondoka kwenye maeneo yao na kuomba misaada kwenye maeneo yanayodhibitiwa na serikali.

Mkakati huu wa sasa umewasaidia kuongeza ushawishi na jamii kuwachukulia kama wao ni bora zaidi ya ujumbe huo wa Umoja wa Mataifa.

Al Shabaab huchukuliwa kama mtoaji bora wa huduma kwa sababu ni kundi linalostahimili athari za mabadiliko ya tabianchi na UNSOM huonekana kuwa dhaifu katika kuliwekea udhibiti.

Hilo limewawezesha kupata uhalali kutoka kwa raia.

Aidha, watu wengi huchagua kwenda katika Mahakama za al-Shaabab, kwa madai kwamba hazina urasimu, na maamuzi yao hutekelezwa kwa sababu al-Shabaab bado ina uwezo wa kutumia nguvu.

Bila shaka hiki ni kitu ambacho kinahujumu mchakato mzima wa ujenzi wa taifa, kwa mujibu wa ofisa mmoja wa UNSOM aliyenukuliwa kwenye ripoti hiyo.

Ripoti hiyo inasema asilimia 94 ya jamii ya kuhamahama nchini humo, hasa wafugaji wanaishi katika umaskini mkubwa.

Mabadiliko ya tabianchi yamesababisha wafugaji kuhamia kwenye maeneo mapya wakisaka malisho hatua ambayo mara nyingine huwaingiza kwenye mizozo na wakulima.

Athari za mabadiliko hayo pia, zimechangia ongezeko la watu ambao hukimbia makazi yao na hadi sasa hawajulikani walipo.

Al-Shabaab hutumia fursa hiyo kuwakamata na kuwapa mafunzo ya kijeshi, hali inayosababisha kubadilika kwa muundo wa idadi ya watu na hata maeneo ya kikabila.

Katika nyakati nyingine mabadiliko haya hufifisha utekelezaji wa makubaliano ya kugawana madaraka ya ndani, lakini pia kudhoofisha juhudi za Umoja wa Mataifa za kujenga taasisi za kiutawala nchini humo.

Hata hivyo, UNSOM imekuwa ikifanya jitihada kadha wa kadha katika kukabiliana na ongezeko la athari za mabadiliko ya tabianchi.

Hatua hizo ambazo ni pamoja na kuanzishwa kwa vituo vya kuratibu operesheni za kupambana na ukame pamoja na uteuzi wa mshauri wa usalama wa mazingira, zinadhihirisha maono ya ujumbe huo ya muda mrefu na mfupi katika jamii za Kisomali. **DW**

## RIPOTI

# Wanasayansi wanachunguza jinsi saratani 'inavyozaliwa'

WANASAYANSI wa Uingereza na Marekani, wameungana kutafuta dalili za mapema za ugonjwa wa saratani katika juhudi za kugundua na kutibu kabla haijajitokeza.

Wanapanga "kuzalisha" saratani katika maabara ili kubaini muonekano wake "siku ya kwanza".

Hii ni moja ya tafiti zinazopewa kipaumbele na muungano huo wa kimataifa wa wanasayansi wanaofanya shughuli za ugunduzi wa mapema wa saratani.

Kufanya kazi pamoja katika mradi huo kunamaanisha watu wanaougua saratani watafaidika zaidi, unasema muungano huo.

**KUPIGA HATUA**

Kwa pamoja wanasayansi hao wanalenga kufanya uchunguzi kama vile wa damu, pumzi na kupima mkojo ili kuwabaini wagonjwa walio katika hatari zaidi.

Lakini pia kuimarisha mbinu ya ugunduzi wa mapema wa saratani na kuangazia kwa jumla dalili zisizoonekana za ugonjwa huo.

Hata hivyo, wamekiri kuwa hatua hiyo "ni kama kutafuta sindano gizani" na huenda ikachukua miaka 30.

"Tatizo la msingi ni kwamba hatujawahi kuona jinsi saratani inavyozaliwa katika mwili wa binadamu," anasema Dk. David Crosby, Mkuu wa kitengo cha ugunduzi wa mapema wa magonjwa katika taasisi ya utafiti wa saratani nchini Uingereza.

"Wakati inapogunduliwa, huwa tayari imejiimarisha." anaongeza.

Uchunguzi wa saratani kupitia vipimo vya damu umependekezwa kwa muda mrefu na wanasayansi.

Watafiti kutoka Manchester, kwa mfano wanakuza tishu za matiti ya binadamu kwenye maabara na seli za kinga za synthetic ili kuona ikiwa wanaweza kuona mabadiliko ya mapema kabisa, ambayo yanaweza kusababisha saratani.

Prof. Rob Bristow anasema ni sawa na "Kuwa na tishu hai inayoishi nje ya mwili wa mgonjwa."

Ukweli ni kwamba kuna hatari ya utambuzi zaidi wa magonjwa, kwa sababu seli zote zilizochunguzwa mapema zinaweza kubadilika na kuwa chanzo cha saratani.

Kwa hivyo wanasayansi wanazingatia hilo kwa kuangazia zaidi jeni za watu walizozaliwa nazo na mazingira waliokulia ili kutathmini hatari inayowakabili linapokuja suala la ugunduzi wa mapema wa ugonjwa wa saratani kwa mtu binafsi.

Uchunguzi wa kina wa MRI huenda ukawa mbinu ya mapema ya ugunduzi wa saratani ya tezi dume.

Ni kupitia njia hiyo wataweza kukabiliana na ugonjwa huo.

**'GHARAMA YA KUZIMA MOTO'**

Hadi leo wanasayansi wanasema, utafiti kuhusu ugunduzi wa mapema wa ugonjwa huo umefanywa kwa kiwango kidogo na kwamba changamoto inayotokana na ukosefu wa kufanyia majaribio matokeo ya utafiti kwa watu wengi, imerudisha nyuma juhudi za kufikia tiba kamili.

Dk. Crosby anasema ushirikiano huu "Utachangia kuleta mabadiliko katika mifumo ya afya na kuondokana na hali ya kukabiliana na saratani ikiwa katika kiwango ambacho gharama ya tiba iko juu na badala yake kubuni mbinu ya ugunduzi wa mapema ambayo pia gharama ya matibabu ni bei nafuu." **BBC**



Uchunguzi wa saratani kupitia vipimo vya damu umependekezwa kwa muda mrefu na wanasayansi. **PICHA: MTANDAO.**

KILA ZAMA NA KITABU CHAKE;

NA MICHAEL ENEZA

# Vibaka wataka kujiorodhesha mikopo elimu ya juu kimtandao




Ofisi za Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Nchini (HESLB). **PICHA: MTANDAO**

TAARIFA za kushangaza zimesikika hivi karibuni kuwa kulikuwa na majaribio 2700 ya kuingia kwa mabavu au mbinu tofauti katika dawati la mtandao la Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), inadhaniwa kutaka kuongeza majina katika orodha ya waliofanikiwa kupata mikopo, au kubadili majina na kuweka mengine.

Juhudi hizo za kupenya katika viunganishi kimtandao vya kufanyia kazi na kutoa majibu ya maombi ya mikopo ni sehemu ya uhalifu mtandaoni, ambao mara nyingi hulenga taarifa za fedha, uhamishaji malipo, n.k. Kujiorodesha kwa hila ni sawa na wizi wa mamilioni ya shilingi.

Tatizo linaloonekana bayana la upenyezi huo mtandaoni, kwani siyo mtu anayejipenyeza bali anaajiriwa kusuka mbinu za kupenya katika viunganishi kimtandao vya vitengo tofauti vya taasisi hiyo, ili kuingia katika orodha ya wanaokopeshwa.

Siyo ajabu pia wangerekebisha taarifa za awali katika mtiririko wake ili ziendane na nyongeza hiyo au badiliko kama hilo lililofanywa kinyemela kuhusu nani waliopitishwa kupata mikopo.

Ujanja huo una gharama kwa maana kuwa inawezekana kufuatilia na kujua kompyuta au simu janja iliyotumika kufanya shughuli hiyo iliunganishiwa wapi, na endapo kituo cha awali kabisa cha kutoa ishara zinazohitajiwa kimtandao kinagunduliwa, aliyetumika kifaa hicho anapatikana bila matatizo.

Kupenyeza katika mtandao na kuongeza majina kinyemela au kubadili majina yaliyopo, bila kujulikana, ni kutazamia kuwa orodha zinatayarishwa kwa haraka haraka tu na hakuna njia ya kuhakikisha kama zinaendana na taarifa za ziada ambazo zimeshikwa na watu wengine.

Endapo yanatokea majina ambayo hayako katika taarifa rasmi zilizowasilishwa au kutayarishwa kwa pamoja katika hatua ya awali ni lazima kuwe na hisia ya tatizo kujitokeza mahali fulani, lakini vibaka mtandaoni wanatazamia kuwa wahusika wa kupelekwa taarifa rasmi wanaongoja mwishoni. Siyo rahisi wafahamu kuwa imerekebishwa kijanja.

Ina maana kuwa njia ya kuhakikisha kwamba hatokei mtu akatafuta tu wakala wa kompyuta akaingia katika viunganishi husika akapenyeza majina na kufuta mengine ni kina cha mawasiliano kuanzia mwanzo hadi mwisho.

Kwa upande mwingine kuna suala la kina cha vizuizi vya kuingia katika viunganishi taarifa, kwa maana ya kupata ruhusa ya wahusika ngazi tofauti ambao ni washikadau katika orodha hiyo au wakati inatayarishwa.

Uhusiano huo wa kanzidata wakati wa kutayarisha orodha ya wanaokopeshwa na kuitoa rasmi kwa vyombo au taasisi tofauti ni kuwa kupeleka taarifa rasmi kuna kanuni zake, si taarifa ya kawaida ambayo inaingia tu katika sanduku la barua pepe la ofisi au mhusika fulani. Ni kizuizi kingine.

Wataalamu wa ofisi ya bodi ya mikopo wanasema kuwa wanafanya juhudi za kuunganisha kanzidata ya utayarishaji na urasimishaji wa maombi ya mikopo katika bodi na kanzidata zingine za taasisi zinazofanya kazi eneo hilo.

Mojawapo ni Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE), Tume ya Vyuo Vikuu (TCU) kuweka mtawanyiko wa uhifadhi nyaraka, hivyo mtiririko huo usifanyike eneo moja tu na kazi hiyo iishie hapo, hivyo wakitokea wajanja wakafaulu kuingia katika kanzidata ya bodi ya mikopo inakuwa rahisi kwao kutenda uhalifu. Endapo kuna mtawanyiko taarifa kinzani zinaonekana kwa haraka.

Licha ya kusema kuwa kulikuwa na tatizo la kutaka kuvunja na kuingia katika mtandao na inaelekea kuna watu wengi au wasomi wa kompyuta walikuwa wanaletewa kazi za kuingia katika orodha hiyo, labda kuna kilichojificha.

Mara nyingi hujuma za namna hiyo zinatoka ndani, mkopo uelekezwe jina hewa, fedha ziingie mifukoni mwa watu wajanja, si ajabu wanaofanya kazi mle mle. Ni upigaji 'dili' wa kawaida.

Haikutolewa taarifa kuwa majina feki yaliongezwa au kanzidata ilihujumiwa kumbukumbu zikaonyesha hitilafu mahali popote, ila tu kwamba kulikuwa na majaribio maelfu ya kuingia katika kanzidata husika ili kuongeza data za kughushi kuhusu wanaotakiwa au kukubaliwa kupelekewa mikopo.

Ina maana kimsingi kanzidata hiyo ilibaki salama lakini kulikuwa na wasiwasi kuhusu majaribio mengi tu ya kutaka kuingia katika hifadhi zake za nyaraka au taarifa na 'kurekebisha' kile walichokitaka.

Ila kwa msemo ule wa 'panapofuka moshi panaficha moto,' kwani haiwezekani kuwa hujuma kama hizo ziliwahi kufaulu awali?

Suala jingine ni tofauti kati ya hujuma inayofanyika kwa ndani halafu maofisa wakaongeza majina feki wanayotaka ili fedha ziingie katika akaunti wanazozijua wenyewe, na kujaribu kuingiza majina kutoka nje.

Ili hujuma ifaulu inabidi iingie kwa njia ambayo haitofautiani na shughuli hiyo kufanyika kikawaida, lakini watu 2700 wakiajiri wataalamu kuingia katika kanzidata ya bodi na kuweka majina yao katika orodha inayotayarishwa au iliyokamilika, ni wazi hapo kuna ishara ya vurugu na upachikaji wa taarifa za kuchekesha katika kanzidata.

Ikitokea asubuhi ofisa anaingia anakuta orodha mpya katika hifadhi ya orodha ya wanaokopeshwa, au mtiririko tofauti kabisa, lazima atajua kuna hitilafu ilitokea ni mamluki.

> Mitihani na matokeo ya kuomba kujiunga na vyuo itakuwa bado sana, au kwa wanaoendelea matokeo ya mitihani mwaka uliotangulia, labda ifahamike kuwa ni maombi ya awali.

Kuna taarifa za ziada ambazo zinaweza kubadili mtiririko wa maombi ya mikopo na hatua za utayarishaji wa orodha, kuwa dirisha la maombi lifunguliwe mwaka mzima, na siyo kipindi ambacho majina ya waliokubaliwa kujiunga na vyuo vikuu na wanaoendelea mwaka mwingine yameshatoka.

Ina maana kuwa wanafunzi au wanafunzi tarajiwa waweze kupeleka maombi yao wakati wowote, hali ambayo inaleta mkanganyiko fulani, kwani itakuwa haihusiani na matokeo ya mitihani ila vigezo vya kuomba vihusiane na masuala mengine.

Mitihani na matokeo ya kuomba kujiunga na vyuo itakuwa bado sana, au kwa wanaoendelea matokeo ya mitihani mwaka uliotangulia, labda ifahamike kuwa ni maombi ya awali.

Kuwapo kwa hatua mbili tofauti katika maombi ni kuwezesha majina kuwahi na kufanyiwa upembuzi wa awali, lakini kuna udhaifu kuwa suala la msingi zaidi ni mitihani na kuruhusiwa kujiunga vyuoni, hivyo inakuwa shida kuona tija ya maombi hayo ya awali.

Kwa upande mwingine, endapo kuna ofisa mwenye uwezo wa kutayarisha majina ya ziada akishirikiana na watu wengine wachache, anapata muda wa ziada wa kushughulikia mchakato huo ambao kimsingi ni hujuma, kwani mhusika akingoja hadi majibu ya mitihani yapokelewe au maombi ya kujiunga chuoni atakuwa amechelewa.

Kunakuwa na msongamano wakati huo na kazi hiyo inahitajiwa imalizike kwa haraka kwa vigezo mahsusi, bila kuwapo mwanya wa wakopeshwaji tarajiwa kufika ofisini kwa bosi huyo kwa maongezi marefu, au pia wakutane kwing-



WADAU

**SABATO KASIKA**

# Sauti za wadau

MATOKEO ya mtihani wa kuhitimu elimu ya msingi kwa mwaka 2019, yameshatangazwa kwa kutaja idadi ya wanafunzi waliochaguliwa kuanza kidato cha kwanza mwakani. Nini kifanyike baada ya matokeo hayo?



### SIMON MILANZI (MKAZI WA NACHINGWEA MKOANI LINDI)

KWA mzazi na mlezi yeyote anayejua umuhimu wa elimu, hawezi kusubiri kukumbushwa la kufanya, kwasababu anajua wajibu wake kwamba anatakiwa kumuandaa mtoto wake kwa ajili ya kuanza kidato cha kwanza mwakani.

Kwa maana hiyo kila kinachohitajika shuleni ni lazima aanze kukiandaa mapema ili tarehe ikifika awe amekamilisha.

Kwa hiyo ninaamini kwamba wazazi na walezi wote wanaojua hilo watakuwa tayari wako kwenye maandalizi ya kununua sare, madaftari na vitu vingine vya muhimu kwa ajili ya watoto wao, na wengine watakuwa wamewapeleka kwenye vituo vya masomo ya ziada ili wanolewe kabla ya kuanza kidato cha kwanza.

Hayo yote ni mema kwani lengo ni kuhakikisha mtoto anaendelea na masomo ya sekondari baada ya kufaulu elimu ya msingi.

Watoto waandaliwe kisaikolojia na kutambua kwamba wanapoanza kidato cha kwanza, lugha ya kufundishia huwa ni Kiingereza, siyo tena Kiswahili kama ambavyo wamezoea katika shule za msingi, hivyo wajiandae kwa hilo na kuona ni jambo la kawaida kuliko kufika wakajikuta wanakwama katika masomo, kwasababu ya lugha, kutokana na ukweli kwamba katika shule za msingi za umma, Kiingereza huwa ni somo.

Distributed via ippmedia

Vilevile jukumu la kufanya maandalizi ya kuingia kidato cha kwanza siyo la wazazi na walezi tu bali wanafunzi wenyewe nao wanapaswa kujiandaa.



### MUSSA MCHUPILA (MKAZI WA RUANGWA MKOANI LINDI)

SWALI lako ni zuri sana, hasa kwa kuzingatia kwamba kwenye elimu kumekuwa na changamoto nyingi zikiwamo zinazosababishwa na baadhi ya wazazi wasiojali umuhimu wa elimu.

Hivyo swali lako linaweza kuwasaidia wazazi wa aina hiyo wajue wajibu wao na kuutimiza.

Ninaposema suala la changamoto, ni kwamba wapo baadhi ya wazazi wanaowalazimisha watoto wao kufanya vibaya katika mitihani ya kuhitimu elimu ya msingi wakidai kwamba hawana fedha za kuwasomesha.

Wengine wakitaka watoto wao waolewe ili wapate mahari na wengine wakitaka watoto wa kiume wabaki nyumbani wakichunga mifugo au kufanya kazi zingine za nyumbani.

Sasa wazazi wenye tabia hiyo, hata kama watoto wao wakifaulu kwenda sekondari wanaweza wasiwapeleke na badala yake wakawaozesha au kuwaacha nyumbani wakifanya kazi tu bila kusoma.

Wazazi wa aina hiyo wakumbushwe kuwafanyia watoto wao maandalizi ili Januari mwaka ujao waanze masomo. Maadui maradhi na umaskini wataondolewa kwa elimu, bila kufanya hivyo wataendelea kutusumbua.

Kwa hiyo nitoe wito huu kwamba kila mzazi atimize wajibu wa kuhakikisha mtoto anapata haki ya kusoma bila kuchanganywa na mambo mengine, ambayo hayana msaada kwa maisha yake ya baadaye.

Kimsingi elimu inajumuisha ufahamu na mengine ya msingi ambayo mwanafunzi anayapata shuleni kwa ajili ya kuyatumia katika jamii inayomzunguka.



### MWASITI RAJABU (MKAZI WA MJINI MOROGORO)

JAMBO la msingi ni kwamba kumpa mtoto elimu ni kumuandaa kwa ajili ya maisha yake ya baadaye.

Ukifuatilia historia ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, utabaini kwamba alipenda sana Watanzania wasome ili waondokane na ujinga na pia waweze kujitegemea, ndiyo maana wanafunzi walifundishwa elimu ya kujitegemea.

Hayo yalifanyika enzi hizo, lakini cha kushangaza ni kwamba wakati huu wa karne ya 21, bado wapo baadhi ya watu wanaona kama elimu haina maana kwao na hawana mpango wa kufanya lolote kwa ajili ya maendeleo ya watoto wao kielimu.

Nimejaribu kuchombeza kidogo, lakini ninachotaka kukisema ni kwamba ni kweli wanafunzi waliofaulu mtihani wa darasa saba wa mwaka huu, wameshatangazwa, kinachofuata ni maandalizi ya kuingia kidato cha kwanza.

Wenye jukumu la kufanya maandalizi hayo ni wazazi na wanafunzi wenyewe. Kila mmoja ana sehemu yake katika maandalizi haya.

Mzazi amnunulie mtoto vifaa vya shule na mtoto naye avitunze akisubiri kuingia sekondari mwaka 2020.

Kila mmoja akifanya sehemu kwa uaminifu, nina uhakika kila kitu kitakwenda sawa bila changamoto yoyote, lakini upande mmoja ukizembea, basi maandalizi yanaweza yasifanikiwe.



### MASTIDIA SIMEO (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)

KATIKA maisha, hakuna jambo lolote linalofanyika bila maandalizi, hivyo unapouliza nini kifanyike baada ya matokeo ya mtihani wa darasa la saba, maana yake ni kwamba wanafunzi waliofaulu waanze maandalizi ya kuingia kidato cha kwanza ikiwamo kujinoa kwenye twisheni, kwa kuzingatia kwamba masomo ni yale yale ingawa yanaongezeka, lakini kikubwa ni lugha tu ndiyo huwa inawagonga wanafunzi wengi, kutokana na ukweli kwamba kuanzia darasa la kwanza hadi la saba, lugha ya kufundishia ni Kiswahili, lakini sekondari ni Kiingereza.

Kutojua Kiingereza kumekuwa kukiwafanya baadhi ya wanafunzi kudhani kuna jambo jipya sana na kumbe ni lugha tu. Hivyo wanatakiwa kufanya maandalizi ya kuwawezesha kuanza kidato cha kwanza wakiwa wanaelewa baadhi ya mambo ya sekondari badala ya kubweteka tu.

Wazazi wana sehemu kubwa katika kufanikisha maandalizi hayo lengo likiwa ni kuhakikisha kila mwanafunzi aliyefaulu anaingia kidato cha kwanza. Halafu bahati nzuri ni kwamba kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne, elimu ni bure. Unafuu huo unaotokana na serikali kuondoa ada. Hivyo tuutumie kusaidia watoto kupata elimu kwa kuwapa mahitaji yote ya shule.

Watakaoshindwa kutumia fursa hii ya elimu bure watakuwa na sababu zao wenyewe wanazozijua ambazo si za msingi. Lakini kwa wanaotambua kuwa elimu ndiyo kila kitu, hawawezi kuzembea, watafanya maandalizi kwa ajili ya watoto wao.



### EUNICE ROBSON (MKAZI WA JIJINI MWANZA)

MIAKA ya hivi karibuni matokeo ya darasa la saba yanatangazwa mapema sana, hali ambayo inawapa nafasi wazazi na walezi kujipanga vizuri kwa ajili ya kuwanunulia watoto wao mahitaji ya shule.

Hivyo wanachotakiwa kufanya ni kuhakikisha kila mmoja ambaye mtoto wake amefaulu, aandae mahitaji yote katika kipindi hiki cha miezi miwili iliyobakia kabla ya kumalizika kwa mwaka 2019, huku akitambua kuwa elimu ni miongoni mwa haki za msingi za mtoto, ambazo anatakiwa kuzipata bila kipingamizi chochote ingawa baadhi yetu tumekuwa hatuzingatii hilo hadi kutowasomesha watoto au kuwaacha waishie elimu ya msingi wakati wana uwezo wa kuendelea na sekondari.

Ninachotaka kukisema ni kwamba maandalizi kwa ajili ya waliofaulu kuingia sekondari yanatakiwa kufanyika sasa. Hicho ndicho kila aliyefaulu anapaswa kukifanya kwa kushirikiana na mzazi au mlezi ili masomo yatakapoanza, mwanafunzi awe na kila kitu kinachohitajika shuleni.

Ninajua wapo baadhi ya wanafunzi wanaweza kukatisha masomo kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo za wazazi kuwazuia na kuwapa majukumu mengine ambayo yanaweza kuwakwamisha wasiendelee na masomo.





# Wahitimu waonywa matumizi mtandao

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

WANAFUNZI wanaohitimu kidato cha nne nchini, wametakiwa kuwa mabalozi wazuri kwa jamii katika kuhakikisha kunakuwapo na matumizi sahihi ya elimu ikiwamo kuepuka kusambaza video na ujumbe unaokiuka sheria za nchi.

Ushauri huo ulitolewa mwishoni mwa wiki na Ofisa wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Mhandisi Charles Tothomas, wakati wa mahafari ya 26 Shule ya Sekondari Ivumwe inayomilikiwa na Jumuiya ya Wazazi wa Chama cha Mapinduzi (CCM).

Alisema kumekuwapo na tabia ya Watanzania kusambaza picha mbalimbali zinazokiuka maadili ya Mtanzania pamoja na sheria ikiwemo picha za ngono na kwamba vitendo hivyo vinatafsiriwa kuwa ni matumizi mabaya ya mitandao.

Mhandisi Tothomas alisema vijana wengi wamekuwa wakitumia simu zao kusambaza matukio ambayo hayanafaida kwa taifa la Tanzania na kusababisha mijadala isiyokuwa na manufaa kwa jamii.

"Wanafunzi mnaohitimu masomo yenu mwaka huu mnaenda huko mitaani na mtamiliki simu za mkononi, tafadhali nawaomba mkawe mabalozi wetu huko kuwakemea wenzenu ambao mnaona wanatumia vibaya mtandao," alisema Mhandisi Tothomas.

Pia alisema kuna uhalifu wa utapeli kwa kutumia mitandao hiyo hivyo wanafunzi hao wanatakiwa kuwa waangalifu wanapotumia simu hizo wakiwa nyumbani kwani watu wengi wametapeliwa.

Naye Mkuu wa Shule hiyo, Emery Muhondwa, alisema shule hiyo inakabiliwa na changamoto ya baadhi ya wazazi kutolipa ada kwa wakati hali inayosababisha wanafunzi kurudishwa nyumbani mara kwa mara.

Alisema kitendo cha kuwarudisha wanafunzi hao nyumbani kufuata ada kinasababisha pia wanafunzi hao kupitwa na baadhi ya masomo kwa madai kuwa wanapokuwa nyumbani vipindi vya darasani vinaendelea kwa wale waliolipa karo.

"Hatuwezi tukasema kwa vile baadhi tumewafukuza basi tusimamishe na masomo ili kuwasubiri hao, tutakuwa hatuwatendei haki waliolipa hivyo masomo yanaendelea kama kawaida," alisema Muhondwa.

Aidha akisoma risala ya wanafunzi wanaohitimu, Janeth Haule alisema awali wanafunzi waliojiunga kidato cha kwanza mwaka 2016 walikuwa 168 lakini kutokana na changamoto mbalimbali wengine waliacha na waliobaki ni 138.

# Mwanjelwa ahoji utekelezaji Mkurabita

**Na Nebart Msokwa, MBARALI**

NAIBU Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mary Mwanjelwa, ametoa wiki mbili kwa Mtendaji Mkuu wa Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (Mkurabita), kueleza mikakati ya mpango huo katika kuwanufaisha wananchi.

Mwanjelwa alitoa agizo hilo jana wakati akizungumza na wananchi wa kijiji cha Kapyo, wilayani Mbarali baada ya kubaini kuwa wananchi hawanufaiki kutokana na kutopewa elimu ya kutosha kuhusu mpango huo.

Alimtaka kueleza namna mpango huo unavyowanufaisha wananchi hasa wa vijijini ambao wanamiliki ardhi kwa kutumia hati za kimila na mali zingine wanazomiliki katika kupata mikopo kwenye taasisi za fedha.

"Hii elimu ilitakiwa kuwa endelevu, sasa ninyi mlikuja 2010 na sasa hivi inaelekea 2020, hawa wananchi yawezekana wengine walishatangulia mbele za haki na wengine wamezeeka. Sasa nataka mniletee taarifa ya utekelezaji wake," alisema.

Alisema mpango huo ulianzishwa kwa ajili ya kuwasaidia wananchi hivyo kama hauleti matokeo chanya tafsiri yake ni kwamba fedha zilizotumika zilipotea bure.

Awali wananchi wa kijiji hicho, walimweleza Naibu Waziri huyo kuwa licha ya mpango huo wa Mkurabita kufika katika kijiji chao na kuwasaidia kupata hati za ardhi za kimila lakini bado hawajui namna ya kunufaika nazo.

Mmoja wa wananchi hao, Herman Zambi, alisema wataalam wa mpango huo walifika katika kijiji hicho na kuwasaidia kupima mashamba na kuwapatia hati za kimila ambazo wanazo mpaka leo lakini hawajawahi kuzitumia.

Alisema hati hizo zinawasaida kuepuka migogoro ya ardhi pekee lakini si manufaa mengine ambayo wanaelezwa kuwa wanaweza kuyapata ikiwamo kuchukulia mikopo kwenye taasisi za fedha.

"Walikuja wakatuelimisha wakaanza kutupimia mashamba kila mtu na kipande chake lakini baada ya hapo hawakuja tena kutupa elimu ya namna ya kuzitumia hati hizi kwenye shughuli zingine," alisema Zambi.

Naye Halima Kibete alisema awali waliambiwa kuwa hati hizo zingewasaidia kutumika kama dhamana kwenye mikopo lakini hawakuelekezwa namna gani ya kuzitumia.

Alisema baada ya kuona hawanufaiki nazo baadhi walidhani kuwa zilikuwa ni mbinu za kuwashawishi ili wakubali kupimiwa ardhi yao na kwamba pengine haukuwa mpango wa Serikali.

Mtendaji Mkuu wa Mkurabita, Seraphia Mgembe, alisema walishatoa elimu ya matumizi ya hati hizo, lakini tangu watoe elimu hiyo, muda mrefu umepita na ndiyo sababu baadhi ya wananchi hawajui namna ya kujinufaisha nazo.

Alisema katika wilaya ya Mbarali, waliutekeleza katika vijiji viwili ambavyo ni Kopyo na Mabadaga na kwamba katika Kijiji hicho cha Kopyo mashamba 636 yalipimwa na kutolewa hati.




Vijana wa Wilaya ya Chunya, mkoani Mbeya, wakifanya mazoezi ya mgambo katika eneo la Kiwanja wilayani humo, mwishoni mwa wiki, huku wakiwa wameshika mitutu ya mfano. Mafunzo hayo, yalizinduliwa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Maryprisca Mahundi (hayupo pichani), mwanzoni mwa mwezi Oktoba. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wajiunga kuchangia NSSF kwa hiari

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

ZAIDI ya watu 400 ambao hawamo kwenye mfumo rasmi wa ajira mkoani Mbeya wamejiunga na Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii wa (NSSF) ambako wanachangia kupitia utaratibu maalum wa kujiwekea mafao ya uzeeni.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Meneja wa NSSF Mkoa wa Mbeya, Nurdin Mruma, wakati wa kongamano la wajasiriamali ambalo liliandaliwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya na kufanyika katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi.

Alisema mfumo huo wa kuwaandalia mafao ya uzeeni wananchi wasio kwenye mfumo rasmi wa ajira umeanzishwa na serikali kwamba unawahusu wajasiriamali wadogo, wafanyabiashara, wakulima na makundi mengine ambayo ajira zao sio rasmi.

Mruma alisema lengo la mfumo huo ni kutaka watu wa makundi hayo wapate mafao baada ya kufikia umri wa uzee kwa ajili ya kuendeleza maisha yao kama ilivyo kwa watumishi wa kwenye sekta rasmi.

"Serikali iliamua kuanzisha mafao kwa makundi haya baada ya kubaini kuwa na wao wanafikia umri ambao hawawezi tena kujitafutia kipato, mtu anafanya kazi ngumu za kujipatia kipato lakini akishazeeka hawezi tena kuzalisha na hivyo kuanza kuishi maisha tegemezi sasa huu mfumo ndio suluhisho," alisema Mruma.

Alisema ofisi yake imeelimisha makundi mbalimbali ya wananchi ili wajiunge na mfuko huo na kujiandalia maisha yao ya baadaye wakiwamo madereva wa bodaboda, wakulima na makundi mengine na kwamba mwitikio ni mkubwa.


Baadhi ya wananchi ambao walihudhuria kongamano hilo waliuomba uongozi wa shirika hilo kupanua wigo wa kutoa elimu ili wananchi wengi zaidi wanufaike kwa kujiunga. Mmoja wa wananchi hao, Paul Mwakitwange, mkazi wa Mbalizi, alisema elimu hiyo inatakiwa kuwafikia hata wananchi wanaoishi vijijini kwa madai kuwa pia kuna watu wengi ambao wanapata shida wakizeeka.

Alisema watu wa vijijini wanafanya kazi ngumu ambazo wakishazeeka hawawezi tena kuzifanya hivyo wanatakiwa wapewe elimu hiyo ili waanze kujiwekea akiba kabla nguvu za kufanya kazi hazijaisha.

"Wananchi wengi wa vijijini wanategemea kilimo na ufugaji kwa ajili ya kuendesha maisha yao, sasa mtu akishafikisha miaka 50 kwa miaka ya sasa nguvu zinaanza kupungua na akishafikisha 70 ndio tegemezi kabisa, wakielimishwa naamini watajiunga," alisema Mwakitwange.

Naye Zena Hansule alisema shirika hilo litasaidia kupunguza hata viwango vya umaskini kwa wananchi kwa madai kuwa wengi wa watu ambao huwa wanakabiliwa na umaskini ni wazee ambao huwa wanakuwa kwenye makundi ya watu wasiojiweza.

Kwa mujibu wa sheria ya mifuko ya hifadhi ya jamii, ili mwanachama apate sifa ya kupata mafao ya uzeeni, ni lazima afikishe umri wa kuanzia miaka 55 na awe amechangia mfuko huo kwa kipindi cha miezi 180.





# Mawakala watakiwa kuzingatia uaminifu

**Na Ibrahim Joseph, DODOMA**

MAWAKALA wa taasisi za kifedha, wamekumbushwa kuwa waaminifu na kuendelea kujenga imani kwa wateja huku wakishauriwa wakifungua ofisi kwenye miradi mipya inayojengwa jijini Dodoma.

Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Godwin Kunambi, alisema hayo alipozungumza kwenye mkutano wa mawakala wa benki ya NMB mkoani humo.

Kunambi aliwataka mawakala hao wa taasisi za kifedha kujenga uaminifu katika kutoa huduma za kifedha kwa wananchi waendelee kutumia huduma hiyo.

"Napenda niwape siri moja hata hizi benki zilianza kama mawakala na sasa ni benki kubwa, kwa hiyo hata ninyi mkiendelea kujenga uaminifu siku moja mtaweza kumiliki benki zenu wenyewe," alisema Kunambi.

Aidha, aliongeza kuwa wakati mwingine wananchi wameshindwa kuwatumia mawakala wa kibenki na kukimbilia kwenye matawi ya benki kwa kuhofia kufanyiwa utapeli na watoa huduma hizo.

Pia aliwaambia mawakala hao kuchangamkia fursa ya kuchukua ofisi kwenye miradi ya maendeleo inayojengwa katika maeneo mbalimbali.

Aliitaja miradi hiyo kuwa ni kituo kikuu cha mabasi na soko kuu inayojengwa Nzuguni ambayo yanatarajiwa kukamilika Desemba mwaka huu.

Mmoja wa mawakala hao, Jeremia Kitonka, alisema mafunzo hayo yamekuwa yakiwajengea uwezo wa kutoa huduma kwa wateja wao maeneo mbalimbali.

Aliwashukuru NMB kwa kuendelea kuwapa mafunzo hayo kila mwaka kwa sababu yanawapa mbinu mpya za kutoa huduma ikiwamo malipo ya mfumo wa kielektroniki wa serikali (GePG).

Kwa upande wake, Meneja Uhusiano wa Mawakala wa NMB makao makuu, Nehemia Simba, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo mawakala hao ili waweze kuongeza tija katika utoaji wa huduma kwa wateja.

Simba alisema NMB inalenga kuweka mawakala wengi nchini na kuwasogezea wananchi huduma karibu na maeneo walipo pamoja na kupunguza msongamano kwenye matawi ya benki hiyo.

**Kwa upande wake, Meneja Uhusiano wa Mawakala wa NMB makao makuu, Nehemia Simba, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo mawakala hao ili waweze kuongeza tija katika utoaji wa huduma kwa wateja.**

# Wazalishaji na wakulima wa zabibu wapewa somo

**Na Ibrahim Joseph, DODOMA**

SERIKALI imewataka wazalishaji na wakulima wa zabibu kujiunga kwenye vikundi vya ushirika ili kupata urahisi wa kupewa mikopo itakayowasaidia kukuza mitaji na uchumi.

Maelekezo hayo yalitolewa na Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, alipokuwa akifungua Tamasha la Urithi Wetu (Urithi Festival) kwa niaba ya Waziri Mkuu Kassim Majaliwa lililofanyika jijini hapa.

Aliwataka wakulima na wazalishaji wa zabibu kuunda vikundi ili kupata urahisi wa kupewa mikopo na taasisi za kifedha za ndani na nje.

Alibainisha kuwa mikopo hiyo itawainua ili kuzalisha mvinyo wa kutosha wa kuuzwa nje na ndani ya nchi ikiwa ni pamoja na kwenye hoteli kubwa za kitalii.

Alisema serikali inaendelea kutengeneza miundombinu rafiki ya kukuza uchumi hivyo wazalishaji kupitia vikundi watanufaika na mikakati hiyo.

Aidha, aliitaka Taasisi ya Utafiti wa Mazao (TARI)kutoa taarifa za utafiti wa mazao mara kwa mara ili wakulima waweze kunufaika na kazi hizo.

Halikadhalika , aliwataka wananchi hao kujenga tabia ya kutembelea kituo cha Tari cha Makutupora Dodoma ili kupata mbegu bora za mazao zikiwamo zabibu.

Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Aloyce Nziku, alisema lengo la matamasha mikoani ni kuutangaza utalii wa ndani ya nchini.

Dk. Nziku alisema wamepanua wigo wa kuendeleza uhifadhi wa utalii wa utamaduni wa ndani ili kufanikisha malengo ya kuwavutia watalii wa nje na ndani ya nchi kwenda kutembelea vivutio hivyo.

Aidha, Dk. Nziku, alisema utalii wa mvinyo na zabibu unaanzia ukiwa shambani ,viwandani na mpaka ukiwa dukani unaendelea kuwa kivutio.

"Kuna mtu hajawahi hata kuona mche wa mzabibu atapenda kufika shambani ili kuutazama lakini ambaye hajawahi kuona jinsi mvinyo unavyotengenezwa kiwanda naye atapenda siku moja afike kutembelea kiwandani huko, kwa hiyo hatua zote hizo ni kivutio cha utalii," alisema.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, alisema zabibu iliingizwa mkoani hapa mwaka 1950 kwa kuletwa na wamisionari wa Kiitaliano kwa ajili ya kutengeneza mvinyo kwenye makanisa.

Mkuu wa Mkoa alisema kilimo cha zabibu kimeendelea kutoa ajira kwa wakulima mkoani hapa ambapo zaidi ya ajira 20,704 zimezalishwa .

Alibanisha kuwa zao hilo linalimwa katika wilaya tatu ambazo ni Dodoma, Bahi na Chamwino na linavunwa mara mbili kwa mwaka.

Aliomba kuongezewa wataalamu zaidi wa kilimo cha zao hili ili kuwahudumia wakulima wengi hasa msimu wa kilimo unapoanza hadi mavuno ili kuongeza tija.



Watoto wa kituo Shime cha wanaoishi katika mazingira magumu, eneo la Makulu, jijini Dodoma, wakifurahia misaada mbalimbali baada ya kukabidhiwa na Shirika lisilo la kiserikali la Thamani ya Vijana Ujasiriamali na Ukuaji wa Kiuchumi (VYEEG), kituoni hapo, juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# `Ushirika uwatafutie wakulima masoko'

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

SHIRIKISHO la Vyama vya Ushirika (TFC) limetakiwa kuvifuatilia vyama vya ushiriki ili kuhakikisha kuwa vinawatafutia wakulima masoko ya mazao yao ikiwamo korosho, alizeti na pamba ili kuinua kilimo chake hapa nchini.

Agizo hilo lilitolewa jana na Kaimu Naibu Mrajisi wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Charles Malunde, katika mkutano wa kupanga mikakati ya kuviendeleza vyama hivyo uliofanyika jijini hapa.

Malunde alisema TFC inatakiwa kuwa mstari wa mbele kuhakikisha vyama vya ushirika vinawatafutia masoko wakulima wa zao la korosho, pamba, alizeti na mazao mengine kwa kuwa vina uwezo wa kutambua kirahisi masoko yalipo.

"Naomba msimamie hili la utafutaji masoko ya mazao, mnakuwa nyuma na kupelekea serikali kuingilia kati kutafuta masoko jambo ambalo halipendezi," alisema Malunde.

Aidha, aliwaambia baada ya mkutano huo ana imani kila chama cha ushirika kitabadilika ili kuhakikisha kinakuwa na hati safi ambazo zitawafanya kuwa salama kwenye masuala ya fedha na miradi ya maendeleo.

Alisema vyama vingi vya ushirika vimekuwa vikilegalega katika utendaji wao ikiwamo kuwa mstari wa mbele kuwahimiza wakulima wa mazao kujiunga na ushirika ili waweze kufanya kilimo chenye tija.

Akizungumzia suala la uanachama, alisema "Kuna vyama vya ushirika zaidi ya 11,000, lakini vilivyo hai ni 7,000 tu. Tunahitaji na hivyo vinginevyo viamke na kuwa hai."

Alisema viongozi wa vyama ambavyo haviko hai wanatakiwa kwenda kuanza upya ili kuhakikisha wanarudi kuwa wanachama hai kama vilivyo vyama vinginevyo vya ushirika.

Kiongozi huyo, alivitaka vyama kufuata sheria ili kuepuka kufungiwa na kwamba chama chochote cha ushirika kikiwa na hati mbaya ya kiutendaji Bodi ya Vyama vya Ushirika haitakuwa tayari kuendelea kufanya kazi na viongozi wa chama hicho.



# Waagizaji matairi wapewa onyo

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WAFANYABIASHARA wa matairi visiwani Zanzibar wametakiwa kufuata sheria ya uingizwaji wa bidhaa zenye viwango ili kuepusha ajali na uchafuzi wa mazingira.

Naibu Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, Hassan Khamis Hafidh, aliyasema hayo jana katika mjadala wa kuthimini hali ya matairi yanayoingizwa nchini na kutumika.

Alisema kuagiza matairi yenye ubora na viwango kutasaidia kufikia lengo lililokusudiwa la kuwa na biashara endelevu.

Hafidh alisema mipira isiyokuwa na viwango husababisha madhara mbalimbali ikiwamo kuongezeka kwa ajali zinazotokana na matairi hayo kupasuka mara kwa mara na hata kusababisha vifo.

Katika kuhakikisha hilo linatekelezwa, alisema wizara imejipanga kufanya jitihada za kudhibiti uingizaji wa mipira isiyo na ubora kwa kuwachukulia hatua za kisheria waagizaji.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Viwango Zanzibar (ZBS), Khatib Mwadini Khatib, alisema si vyema kwa wafanyabiashara kufanya udanganyifu wa kuingiza na kuuza bidhaa zisizo na ubora kwa kuwa kufanya hivyo kunaweza kusababisha athari kwa watumiaji.

Alisema kumekuwapo na changamoto za uingizaji wa matairi hayo jambo ambalo linapelekea kurudisha nyuma jitihada za kuimarisha maendeleo ya biashara hiyo.

Kwa upande wao, wafanyabiashara wa matairi wameomba watumiaji kupatiwa elimu ili kuepusha kasoro ambazo zinajitokeza wakati wakiwa safarini kwa kusababisha athari zaidi na kuahidi kufuata sheria za uingizaji wa bidhaa zenye kiwango.



Mafundi wakijenga miundombinu ya maji kwenye barabara mpya ya kiwango cha lami, inayounganisha eneo la Tandale na Mwananyamala kwa Manjunju, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Waziri achagiza vita udhalilishaji

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WAJUMBE wa kamati ya viongozi wa juu ya kupambana na vitendo vya udhalilishaji dhidi ya wanawake na watoto Zanzibar, wamewataka wananchi wote kujitolea katika kupinga vitendo hivyo, huku wakitaka mahakama kufanya kazi yake ili kuinusuru jamii na janga hilo.

Haya yalisemwa jana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Haroun Ali Suleimani, katika kikao cha pamoja kilichoandaliwa na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA) kilichofanyika Mazizini, Wilaya ya Magharibi B.

Alisema ni vyema jamii ikafahamu kuwa mahakama zimeanzishwa kusimamia sheria, hivyo ni vizuri kushirikiana nazo ili kufanya kazi ipasavyo katika kutoa hukumu za kesi kwenye kesi za udhalilishaji.

"Mahakama ziachiwe kazi zifanye kwa mujibu wa sheria ziliozopo juu ya makosa ya udhalilishaji. Si vyema baadhi ya watu kuziingilia mahakama badala yake waziamini na kuzipa ushirikiano," alisema.

Haroun alisema hawatawafumbia macho viongozi ambao huingilia vyombo vya sheria hasa katika kesi hizo kwa kuwa tabia hiyo inaweza kusababisha mustakbali mbaya wa taifa.

Hata hivyo, aliwataka wananchi kuripoti kesi hizo na kuacha tabia ya kuvunjika moyo kwa kuwa ushirikiano wao utasaidia kuondoa changamoto hiyo ya udhalilishaji hasa ubakaji.

# 'Wanawake, vijana changamkieni fursa'

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KATIBU wa Kamati Maalumu ya Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC), Idara ya Organazesheni CCM Zanzibar, Cassian Galos Nyimbo, amewataka wanawake na vijana wa Jimbo la Jang'ombe kutumia vizuri fursa ya ujasiriamali kwa kujiajiri.

Wito huo aliutoa jana wakati akizindua Kituo cha Mafunzo ya Ujasiriamali cha Jang'ombe kilichoanzishwa na Mwakilishi wa Jimbo hilo, Ramadhan Hamza Chande, katika eneo la Kilimani, Mnara wa Mbao, Unguja.

Alisema ujasiriamali ni kazi kama zilivyo kazi zingine katika jamii, hivyo ujuzi unaotokana na sekta hiyo unatakiwa kuthaminiwa na kupewa kipaumbele.

Nyimbo alisema mafunzo hayo ya ujasiriamali watakayopewa wananchi wa jimbo hilo kupitia kituo hicho, yawe na tija ya kujikwamua kichumi na kujiongezea kipato.

Alimpongeza mwakilishi huyo kwa ubunifu wake wa kuanzisha kituo kitakachozalisha wataalamu wengi wa ujasiriamali wenye uwezo wa kutengeneza bidhaa mbalimbali zenye viwango.

"Nakuombeni hiki kituo mkitumie vizuri kwani mkipata ujuzi wa masuala ya ujasiriamali mtakuwa mmejikomboa katika wimbi la umaskini na kuwa na uwezo wa kujiajiri wenyewe," alisema.

Naye Chande alisema lengo la kuanzisha kituo hicho ni kuwapatia ujuzi wa masuala ya ujasiriamali wananchi wa jimbo hilo hasa vijana na wanawake.

Alisema wakati akiomba kura za wananchi wampatie ridhaa ya uongozi aliahidi kuanzisha kituo hicho na kwa sasa ametekeleza ahadi hiyo.

Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2015-2020, alisema imeelekeza uanzishwaji wa vituo vya mafunzo ya ujasiriamali nchini, hivyo jimbo hilo limetekeleza maelekezo ya ilani hivyo kwa vitendo.

Alisema kituo kimesajiliwa na kupitia taratibu zote za kisheria pia wana wakufunzi waliobobea katika kufundisha utengenezaji wa bidhaa bora zinazokubalika katika soko la ndani na kimataifa.

Mwenyekiti wa UVCCM Mkoa wa Mjini Magharibi, Kamaria Suleiman Nassor, aliwapongeza viongozi wa Jimbo la Jang'ombe kwa ushirikiano wao uliozaa matunda ya kuanzisha kituo hicho kitakachowanufaisha vijana.

Alisema vijana wa jimbo hilo wanatakiwa kuchangamkia fursa hiyo kwa kujiunga kituo hicho ili wapate ujuzi utakaowawezesha kutengeneza bidhaa zitakazowapatia kipato.

# Majengo ya wakimbizi yawa kituo cha afya

**Na Restuta Damian, NGARA**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Ngara mkoani Kagera, imeanza ujenzi na ukarabati wa Kituo cha Afya Rukole Kata ya Kasuro ili kusaidia wananchi wa kata hiyo kwa kutumia majengo yaliyokuwa ya kambi ya wakimbizi.

Hayo yamesemwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Aidan Bahama, wakati akizungumzia hali ya kituo hicho kwenye eneo la ujenzi.

Bahama alisema ujenzi wa majengo hayo ambayo yalikuwa ya wakimbizi baada ya kurejea kwao mwaka 2007 yalitumiwa na halmashauri kwa kutolea huduma ya afya kwa kiwango kidogo.

Bahama alisema uamuzi wa kusaidia wananchi wa kata hiyo ni kuona baadhi ya majengo ya mochwari, sehemu ya mapokezi, sehemu ya upasuaji yameharibika zaidi.

"Majengo hayo yalikuwa ya wakimbizi na kama mnavyoona kuna mochwari imeharibika, sehemu ya upasuaji kutokana na kujengwa kwa tope...sasa walivyorudi kwao tumeamua kuyatumia kuwa kituo cha afya kwa uhitaji wa kata hiyo, alisema Bahama.

Alisema hivi sasa shughuli ya ujenzi inaendelea na kuwa majengo yanayojengwa ni sita ambayo ni nyumba ya watumishi, mochwari, maabara, sehemu ya mapokezi, na upasuaji yenye kwa gharama ya Sh. milioni 600.

Alisema ukamilishaji wa kituo hicho kutakifanya kuwa miongoni mwa vituo ambavyo vinatoa huduma ya afya kwa jamii na vilivyo bora kwa miundombinu.

Alisema fedha inayotumika katika mradi huo ni kutokana na Rais John Magufuli kutaka wananchi wapatiwe huduma kupitia miradi ya maendeleo kusogezwa karibu yao na kuacha kutembea umbali mrefu.

"Fedha hizi ni kati ya pesa Sh. bilioni 10 zilizotolewa na Rais kuja kwa wananchi kufanya maendeleo... niliona uhitaji wa kata hiyo na kutoa kiasi cha kufanya ujenzi wa kituo hicho," alisema Bahama.

Aliongeza kuwa kwa kuona wananchi wa kijiji cha Rukole, Kata ya Kasuro wanafuata huduma ya afya katika Hospitali ya Wilaya Nyamiyaga ambapo kuna umbali mrefu kufikia huduma hiyo.

# Walipakodi wapewa fursa zaidi ya kulipa madeni

**Na Mwandishi Wetu, PEMBA**

BODI ya Mapato Zanzibar (ZRB), inaendelea kutoa fursa ya kusamehe madeni ya walipakodi yatokanayo na adhabu, riba na faini, ili kutoa nafasi ya wafanyabiashara kusawazisha madeni yao.

Akizungumza na wafanyabiashara Gombani Chakechake Pemba, Ofisa Uhusiano wa Bodi hiyo, Makame Khamis Mohamed, alisema hiyo ni fursa muhimu kwa walipakodi hao, hivyo ni vyema kuitumia ili kusamehewa madeni yao.

Alisema serikali imeamua kusamehe madeni ya walipakodi yatokanayo na adhabu, riba na faini kwa asilimia 100 iwapo wafanyabiashara hao watakubali masharti yaliyowekwa.

"Hii ni fursa muhimu kwenu msiiache, ni vyema kuja na mkatimiza masharti yaliyowekwa, ili kukuza utamaduni wa uwajibikaji wa kulipa kodi," alisema.

Alieleza kama wafanyabiashara hao wataitikia wito huo wa msamaha wa madeni, ZRB inatarajia kupata Sh. bilioni 4.6.

"Kodi yako unayodaiwa itabaki pale pale isipokuwa utasamehewa kile kilichosababisha deni hilo kuongezeka ikiwa ni pamoja na adhabu, riba na faini, hivyo tunataraji mtafika kabla ya kumaliza muda uliowekwa," alisema Makame.

Alifahamisha kwa atayeomba msamaha huo, anatakiwa kujaza fomu maalumu ambayo inapatikana katika bodi hiyo, ambapo maombi hayo yalianza Julai 1 hadi Desemba 31, mwaka huu.

"Pia madeni yatakayosamehewa ni yale yaliyoanza Juni 30, mwaka huu kwenda miaka ya nyuma, hawa ndio watakaohusika na msamaha huu," alifafanua.

Akitaja kodi zinazohusika na msamaha huo ni ya ongezeko la thamani (ya ndani), ushuru wa bidhaa (katika huduma), ushuru wa stempu, ada za bandari, kodi za mafuta, hoteli na ardhi.

Aidha, alisema watu au taasisi au kampuni zinazohusika ni ambazo zimewasilisha ritani kwa kodi iliyostahiki kulipwa, lakini hakulipa kodi yote au sehemu ya kodi, pamoja na kutokuwasilisha ritani kwa kodi zilizostahiki.

"Pia ikiwa hukusajiliwa na bodi, lakini inajua au haijui kama ina wajibu wa kulipa deni la kodi, ina kodi inayotokana na makisio au ina kesi zilizopo mbele ya Bodi ya Rufani za Kodi, Baraza au Mahakama ya Rufani na imesajili dhamira ya kusawazisha kesi hizo nje ya mahakama," alieleza Makame.

Ofisa Elimu ya walipakodi kutoka Bodi hiyo, Badria Massoud Atae, alisema, lengo la mkutano huo ni kuzungumzia msamaha wa madeni yatokanayo na riba, adhabu na faini na kuwataka wafanyabiashara hao kuichangamkia fursa hiyo ambayo imewekwa kwa muda maalumu.

"Kinachotusikitisha ni kuwa kuna upandishaji holela wa kodi, pia hatujui kiwango maalum na badala yake unapandishiwa kodi kila unapokwenda kulipa na unapouliza huambiwi, hii inatuumiza sana," alisema Khamis Mohamed Haji, mfanyabiashara.

Naye Harith Badawi aliiomba bodi hiyo kutumia mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya kukusanya kodi, ili kuondosha usumbufu kwa wafanyabiashara hasa walioko vijijini.



Kiongozi wa Kikundi cha Vijana cha Faraja Carpentry, James Luwanda, akionyesha vitendea kazi wanavyotumia kutengeneza bidhaa zao, kwa wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria, walipofanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya vijana katika Mkoa wa Morogoro juzi. Kulia ni Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana na Ajira, Anthony Mavunde na (wa tano kulia) ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Najma Giga. **PICHA: OWM**

# Mizigo yaongezeka Bandari ya Mtwara

**Na Mary Geofrey**

IDADI ya shehena za mizigo inayohudumiwa katika Bandari ya Mtwara, imeongezeka kutoka tani 296,577 mwaka 2014/15 hadi tani 363,287 mwaka 2017/18.

Kadhalika, katika kipindi cha mwaka 2018/19 imehudumia meli 141 kutoka meli 66 mwaka 2017/18, ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 113.

Hayo yalielezwa jana mkoani Mtwara na Meneja wa Bandari hiyo, Mhandisi Juma Kijavara, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utendaji kazi wa bandari hiyo, namna walivyojipanga kuhudumia na kukuza uchumi wa mikoa ya kusini na nchi jirani.

Alisema mbali na kusafirisha korosho, bandari hiyo kwa sasa inasafirisha saruji, mafuta, makaa ya mawe, makasha, makontena pamoja na kushusha magari ambayo yanaenda nchi za Msumbiji, Zambia na Malawi. "Bandari ya Mtwara imevuka lengo lake kuhudumia meli kwa zaidi ya asilimia 100 wakati lengo lake lilikuwa ni kuhudumia meli kwa asilimia 66 na kusafirisha mizigo kwenda jirani zilizopo ukanda wa Kusini," alisema Kijavara.

Alisema bandari hiyo pia imefanikiwa kushusha magari zaidi ya 600 ya kiwanda cha Saruji cha Dangote yanayotumika kwa ajili ya kusambaza bidhaa hiyo kutoka mkoa huo kwenda mikoa mbalimbali nchini.

Aidha, Kijavara alisema kina cha maji katika bandari hiyo ni mita 12 na mita 9.5 chenye uwezo wa kubeba meli za ukubwa wa mita 230.

Alisema Agosti 22 mwaka huu, walipokea meli aina ya Mv Christiana yenye urefu wa mita 222 iliyoshusha kontena 1,800 kwa ajili ya upakiaji wa korosho.

"Hii ni meli kubwa kuliko meli zilizoingia katika bandari hii," alisema Kijavara.

Kwa upande wake, Ofisa Ununuzi na Ugavi wa Bandari ya Mtwara, Abdilah Salim, alisema katika mkoa huo kuna bandari bubu zaidi ya 140.

Alisema bandari hizo zipo kuanzia Kilwa mpaka Mtwara na 11 kati yao zinatarajiwa kuanza kurasimishwa na serikali.

Alisema kurasimisha kwa bandari hizo kutasaidia kuweka uwiano kati ya wafanyabiashara wanaotumia bandari kuu ambao wanalipa kodi na wale walio katika bandari bubu ambao hawalipi kodi inavyotakiwa na kuingizia serikali hasara.

Alisema hasara ya kutumia bandari bubu ni kuepuka maradhi kutokana na magonjwa ambayo yanaweza ambukizwa kupitia njia za mpakani na kupitisha dawa za kulevya na kupitisha bidhaa feki.

## HABARI KIMATAIFA

# Watega kamera chooni kuchungulia abiria

**TEXAS,** Marekani

MMOJA wa wafanyakazi wa Kampuni ya Ndege ya Southwest Airlines amefungua kesi mahakamani akiwashutumu marubani wawili kwa kuficha kamera katika choo cha ndege hiyo na kuwachungulia abiria ambao walikuwa wakienda kujisaidia.

Renee Steinaker anadai kwamba alibaini njama hiyo ya marubani hao wakati wa safari ya ndege ya mwaka 2017 kutoka mjini Pittsburgh hadi Phoenix.

Hata hivyo, baada ya kubainika, Rubani Terry Graham alimtaka Steinaker kukaa katika chumba cha rubani na rubani mwenzake Ryan Rusell, wakati alipotumia choo hicho.

Rubani na kampuni ya ndege ya South West Arlines wamekana mashitaka hayo kwamba kulikuwa na kamera iliyokuwa ikiwachukua abiria na wafanyakazi waliokwenda msalani.

Steinaker alidai kuwa Russell alimuonya kutosema kitu kuhusu kamera hiyo ambayo alisema ilikuwa mkakati wa usalama.

**Marubani hao hawakuitwa na kampuni hiyo ya ndege na wanaendelea na kazi yao kawaida kulingana na mashtaka hayo.**

Mfanyakazi huyo aliripoti kisa hicho kwa kampuni hiyo, lakini anadai msimamizi mmoja alimuagiza kutomwambia mtu yeyote kilichotokea.

Marubani hao hawakuitwa na kampuni hiyo ya ndege na wanaendelea na kazi yao kawaida kulingana na mashtaka hayo.

Katika taarifa iliyotolewa na kampuni ya Southwest Airlines iliiambia Shirika la Utangazaji la BBC kwamba kampuni hiyo haiweki kamera katika vyoo vya ndege.

Awali, kampuni hiyo ya ndege ya Marekani ilikataa kutoa tamko kuhusu kesi hiyo . Lakini katika taarifa nyingine ilieleza kuwa imechunguza madai hayo na kupata kwamba hakukuwa hata na kamera moja katika choo.

"Wakati kisa hicho kilipotokea siku mbili zilizopita, tulichunguza madai hayo na kuangazia hali hiyo na wafanyakazi waliohusika, Tunaweza kuthibitisha kutoka kwa uchunguzi wetu kwamba hakukuwa na kamera chooni, kisa hicho hakifai na kwamba kampuni hiyo haiwezi kukikubali'," ilieleza taarifa hiyo.

Katika majibu yao yalioandikwa kwa walalamikaji, Russell na Graham walikiri kwamba kulikuwa na kompyuta katika chumba hicho cha marubani lakini walikana madai mengine yoyote.

Saa mbili kabla ya safari ya ndege kuanza Februari 27, 2017, Graham alimuomba Stainaker kusalia katika chumba hicho cha marubani huku yeye akienda chooni, ilieleza sehemu ya malalamiko.

Kulingana na sera ya kampuni hiyo ya ndege wafanyakazi wawili wanafaa kuwapo katika chumba hicho cha ndege kila mara.

Russell alikiri kwamba kamera ilikuwa ikichukua watu moja kwa moja, huku akiwa na wasiwasi katika uso wake, kabla ya kumshauri Stainaker kutomwambia mtu yeyote na kwamba ulikuwa mkakati wa kiusalama.

Kamera hizo zilikuwa na siri kubwa zikiwa zimewekwa katika kila ndege aina ya 737-800, ilidaiwa kwamba Graham alimwambia mfanyakazi mmoja wa ndege.

Na kufuatia maelezo ya Russell, Stainaker alipiga picha ya kompyuta hiyo na simu yake, yalisema mashtaka hayo.

Wakati Stainaker alipolalamika, msimamizi mmoja alimtaka kunyamaza na kutolizungumzia kuhusu suala hilo na kwamba iwapo itajulikana hakuna mtu atakayesafiri kwa kutumia kampuni hiyo ya ndege.

Mashtaka hayo ya Steinaker yanataka alipwe Dola za Marekani 50,000 kama fidia kutoka kwa kampuni ya Southwest Airlines pamoja na marubani.

Goldman alisema mteja wake alikua amedhurika na suala hiyo ambalo lilimsababishia dhiki kali.

Mashtaka hayo yaliwasilishwa katika jimbo la Arizona, lakini imehamishwa katika mahakama ya wilaya mjini Arizona. **BBC**

## Nyusi atetea kiti chake cha urais

**MAPUTO,** Msumbiji

TUME ya Uchaguzi ya Msumbiji imemtangaza Rais Filipe Nyusi kuwa mshindi wa uchaguzi kwa asilimia 73 ya kura.

Pia kimekitangaza chama chake cha Frelimo kushinda asilimia 74 ya viti bungeni kufuatia uchaguzi wa uliofanyika Oktoba 15.

Chama kikuu cha upinzani, Renamo kimeyakataa matokeo hayo, kikidai kuwa uchaguzi huo ulikuwa umegubikwa na udanganyifu na vitisho.

Tume pia imemtangaza mgombea wa Renamo, Ossufo Momade, kuwa amepata asilimia 22 ya kura. Huku idadi ya wananchi waliojitokeza kupiga kura ni asilimia 51.

Katika bunge lenye viti 250, chama cha Frelimo kimepata viti 184, Renamo viti 60 na chama cha MDM viti sita. **DW**

## Uingereza kujitoa EU mwakani

**LONDON,** Uingereza

IKIWA zimebaki siku mbili kwa Uingereza kutangaza kujitoa Umoja wa Ulaya (EU) umoja huo jana ulikubali kuchelewesha kwa muda wa miezi mitatu Uingereza kujitoa kutoka umoja huo hadi Januari 31, mwakani.

Siku tatu kabla ya tarehe ya mwisho ya Uingereza kujitoa kutoka katika umoja huo hapo Oktoba 31, mchakato wa Brexit bado haujulikani mwelekeo wake wakati wanasiasa wa Uingereza hawako karibu ya kufikia muafaka juu ya vipi, lini na hata iwapo hatua ya kuachana na EU itawezekana.

Mataifa 27 ya EU yamekubaliana jana kuchelewesha Brexit hadi Januari 31, pamoja na uwezekano wa Uingereza kujitoa mapema iwapo bunge la Uingereza litaidhinisha makubaliano ya kujitoa. **DW**



Rais wa Botswana, Mokgweetsi Masisi (kulia) akiwa na mke wake, Neo Masisi, baada ya kutangazwa kuwa rais wa nchi hiyo. **PICHA: RFI**

# Wakristo Ethiopia wamlaumu Waziri Mkuu

**ADDISABABA,** Ethiopia

KANISA la Orthodox nchini Ethiopia limemkosoa vikali Waziri Mkuu, Abiy Ahmed kwa kile linachosema ni kushindwa kuzuwia machafuko ya kikabila na kidini ambayo hadi sasa watu 70 wameshafariki.

Kanisa linasema waziri mkuu huyo ameshindwa kuwalinda waumini wa kanisa hilo lenye ushawishi mkubwa nchini Ethiopia.

Ghasia zilizuka katika Mji Mkuu wa Addis Ababa na jimbo la karibu la Oromia siku ya Jumatano wiki iliyopita, baada ya mwanaharakati mmoja kuvishutumu vyombo vya usalama kwa kula njama ya mashambulizi dhidi yake,madai ambayo Jeshi la Polisi limeyakataa.

Afisa mmoja wa Jeshi la Polisi alisema siku ya Ijumaa kuwa watu 67 waliuawa katika machafuko hayo katika Jimbo la Oromia.

"Watu wanakufa na maswali yanaulizwa endapo kweli serikali ipo. Watu wanapoteza matumaini," alisema kiongozi wa Kanisa la Orthodox la Tawahedo, Markos Gebre-Egziabher, baada ya sala ya kuwaombea wafu kwenye Kanisa la Utatu Mtakatifu mjini Addis Ababa siku ya Jumapili.

Wafuasi wa kanisa la Orthodox ni takribani asilimia 40 ya wakazi wote milioni 110 wa Ethiopia.

Abiy, mshindi wa Tuzo ya Amani ya Nobel ya mwaka huu, alitoa kauli yake usiku wa Jumamosi, ambapo aliapa kuwafikisha wahalifu mikononi mwa vyombo vya sheria na kuonya kwamba machafuko yataongezeka endapo Waethiopia hawataungana.

Msemaji wa kanisa hilo aliliambia Shirika la Habari la AFP kwamba waumini 52 wa kanisa hilo, wakiwamo maofisa wawili wa kanisa, ni miogoni mwa waliouawa. Hata hivyo, idadi hiyo haikuweza kuthibitishwa. **DW**

# MWALIMU COMMERCIAL BANK PLC

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

| WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA 2019 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Robo Mwaka ya sasa 30-Sep-2019 | Robo Mwaka iliyopita 30-Jun-2019 |
|---|---|---|
| **A. MALI:** | | |
| 1. Fedha Taslimu | 512 | 440 |
| 2. Salio katika Benki Kuu ya Tanzania | 2,720 | 447 |
| 3. Uwekezaji katika Amana za Serikali | - | - |
| 4. Salio katika Benki nyingine na Taasisi za fedha | 210 | 377 |
| 5. Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 63 | 10 |
| 6. Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7. Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8. Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9. Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 4,000 | 4,000 |
| 10. Uwekezaji katika Amana Nyingine | - | - |
| 11. Mikopo Halisi Iliyopo | 16,378 | 16,311 |
| 12. Mali Nyingine | 5,282 | 5,484 |
| 13. Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14. Akaunti za udhamini | - | - |
| 15. Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,296 | 1,453 |
| **16. JUMLA YA MALI** | **30,461** | **28,522** |
| **B. DHIMA:** | | |
| 17. Amana za Benki nyingine na Taasisi za fedha | - | - |
| 18. Amana za Wateja | 11,660 | 8,268 |
| 19. Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20. Amana Maalumu | - | - |
| 21. Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22. Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23. Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 841 | 705 |
| 24. Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25. Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 19 | 4 |
| 26. Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo nyingine Zitakazolipwa Baadae | 170 | 228 |
| 27. Dhima Nyingine | 544 | 573 |
| 28. Madeni | - | - |
| **29. JUMLA YA DHIMA** | **13,234** | **9,778** |
| **30. MALI/(DHIMA) HALISI** | **17,227** | **18,744** |
| **C. FEDHA ZA WANAHISA:** | | |
| 31. Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 30,912 | 30,912 |
| 32. Akiba ya Mtaji | - | - |
| 33. Mapato Yaliyobakizwa | (9,658) | (9,819) |
| 34. Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (4,027) | (2,510) |
| 35 Akaunti Nyingine za Mtaji | - | 161 |
| 36. Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37. JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **17,227** | **18,744** |
| **38. DHIMA ZISIZO DHAHIRI** | | |
| 39. Mikopo Chechefu | 289 | 323 |
| 40. Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 302 | 253 |
| 41 Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| - Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 57% | 66% |
| - Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 1.7% | 1.9% |
| - Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 143% | 200% |
| - Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 55% | 58% |
| - Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 67% | 71% |
| - Ongezeko la Amana | 41% | 12% |
| - Ongezeko la Mali | 7% | -2% |

| TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO MWAKA ULIOISHIA 30 JUNI 2019 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Robo Mwaka ya sasa 30-Jun-2019 | Robo Mwaka iliyopita 31-Mach-2019 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Jun-2019 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 30-Jun-2018 |
|---|---|---|---|---|
| **I. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| Mapato (Hasara) Halisi | (1,517) | (1,416) | (4,027) | (4,019) |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | | - | |
| - Hasara katika Mali | 212 | 622 | 1,346 | 1,496 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (67) | (40) | (199) | 8,010 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 3,392 | 888 | 3,711 | (988) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 64 | (138) | 121 | 2,926 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (105) | (352) | (609) | (3,589) |
| - Kodi Iliyolipwa | - | - | - | - |
| - Mengineyo | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **1,979** | **(436)** | **343** | **3,836** |
| **II. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | - | - | - | - |
| - Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| - Ununuzi wa Mali za Kudumu | (36) | (5) | (41) | (471) |
| - Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| - Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | (179) | 946 | (3,119) |
| - Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| - Mengineyo | - | - | | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(36)** | **(184)** | **905** | **(3,590)** |
| **III. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | - | - | - | - |
| - Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| - Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| - Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| - Gawio Lililolipwa kwa Fedha taslimu | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| - Mengineyo | - | - | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za Kifedha** | **-** | **-** | **-** | **-** |
| **IV. Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| - Ongezeko / Punguzo Halisi katika Fedha Taslimu na Mali zinazofanana na Fedha Taslimu | 1,943 | (620) | 1,248 | 246 |
| - Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 965 | 1,585 | 1,557 | 644 |
| - Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 2,908 | 965 | 2,805 | 890 |

| TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30 SEPTEMBA 2019 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Mtaji wa Hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Ziada nyingine | Tengo la Ziada ya Jumla | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 30,912 | (9,976) | - | 179 | 179 | 21,294 |
| Faida (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | (4,027) | - | - | - | (4,027) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - |
| Ziada nyingine | - | 139 | - | (179) | - | (40) |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | 179 | - | - | (179) | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **30,912** | **(13,685)** | **-** | **-** | **-** | **17,227** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 30,912 | (4,120) | 114 | 204 | - | 27,110 |
| Punguzo kutokana na kupitisha IFRS9 | - | (288) | - | - | - | (288) |
| Faida (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | (5,503) | - | - | - | (5,503) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | | | | (25) | - | (25) |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | | 114 | (114) | | - | - |
| Mengineyo | - | (179) | - | - | 179 | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **30,912** | **(9,976)** | **-** | **179** | **179** | **21,294** |

| TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2019 (Kiasi kwa shilingi milioni) | Robo ya Mwaka sasa 30-Sep-2019 | Robo ya mwaka Linganishi 30-Sep-2018 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 30-Sep-2019 | Limbikizo la Mwaka linganishi 30-Sep-2018 |
|---|---|---|---|---|
| 1. Mapato ya Riba | 709 | 781 | 2,215 | 2,456 |
| 2. Gharama za Riba | 172 | 135 | 449 | 448 |
| **3. Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2)** | **537** | **646** | **1,766** | **2,008** |
| 4. Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - | - | - |
| 5. Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 62 | - | (53) | 8 |
| 6. Mapata Yasiyo ya Riba: | 169 | 64 | 311 | 162 |
| 6.1 Faida (Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za kigeni | 12 | - | 21 | 4 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 157 | 62 | 289 | 156 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | - | 2 | 1 | 2 |
| 7. Gharama Zisizo za Riba | 2,161 | 2,069 | 6,157 | 6,181 |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 922 | 886 | 2,629 | 2,695 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | - | - | - | - |
| 7.3 Gharama Nyingine | 1,239 | 1,183 | 3,528 | 3,486 |
| **8. Faida (Hasara) ya Uendeshaji** | **(1,517)** | **(1,359)** | **(4,027)** | **(4,019)** |
| 9. Tengo la Kodi ya Mapato | - | - | - | - |
| **10. Faida (Hasara) Halisi Baada ya kodi ya Mapato** | **(1,517)** | **(1,359)** | **(4,027)** | **(4,019)** |
| 11. Mapato Mengine Yaliyojumuishwa | - | - | - | - |
| **12. Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(1,517)** | **(1,359)** | **(4,027)** | **(4,019)** |
| 13. Idadi ya Waajiriwa | 56 | 63 | 56 | 63 |
| 14. Mapato kwa Hisa | -25 | -22 | -65 | -65 |
| 15. Idadi ya Matawi | 2 | 2 | 2 | 2 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| - Uwiano wa Faida kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -5% | -4% | -14% | -11% |
| - Uwiano wa Faida baada ya kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -9% | -6% | -21% | -16% |
| - Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 306% | 291% | 296% | 285% |
| - Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 3% | 3% | 9% | 9% |

**BAADHI YA MAELEZO**
**KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA 2019**

Katika kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| Richard Makungwa (Ofisa Mtendaji Mkuu) | ........................ (Imesainiwa) | 28 OKTOBA 2019 |
| Selemani Kijori (Mkuu wa Fedha) | ........................ (Imesainiwa) | 28 OKTOBA 2019 |
| Poniwoa Andrew (Kaimu Mkaguzi Mkuu wa Ndani) | ........................ (Imesainiwa) | 28 OKTOBA 2019 |

Distributed via ippmedia

**usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya sheria ya benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.**

| Jina | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| 1/ Herman Kessy | ........................ (Imesainiwa) | 28 OKTOBA 2019 |
| 2/ Ambrose Nshala | ........................ (Imesainiwa) | 28 OKTOBA 2019 |

## MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES AND FEES MADE UNDER REGULATION 11

| S/N. | ITEM/TRANSACTION | CHARGE/FEE |
|---|---|---|
| **1** | **Current Accounts** | |
| | (a) Required minimum opening balance | TZS 50,000 |
| | (b) Monthly service fee (breakdown per customer type) | TZS 7,500 |
| | (c) Cheque withdrawal over the counter | TZS 2,500 for amounts less than 5Mil otherwise 0.1% max TZS 100,000 |
| | (d) Fees per ATM withdrawal | TZS 1,300 |
| | (e) ATM mini statement | TZS 300 |
| | (f) Interim statement per page | TZS 2,500 |
| | (g) Periodic scheduled statement | 0 |
| | (h) Cheque book | TZS 500 per leaf |
| | (i) Dishonoured cheque | TZS 64,000 |
| | (j) Special clearance | n/a |
| | (k) Counter cheque | TZS 6,000 |
| | (l) Stop payment | TZS 38,400 |
| | (m) Standing order (Same bank) | Free |
| | (n) Balance enquiry | TZS 300 |
| | (o) New ATM card issuance | TZS 8,000 |
| | (p) ATM card renewal or replacement (indicate costs for different card types) | TZS 15,000 |
| | (q) Overdrawn account interest charge | 20% |
| | (r) Unarranged overdraft | 20% |
| | (s) Interbank transfer | TZS 10,000 |
| | (t) Bill payments through ATM | n/a |
| | (u) Deposit fee | 0 |
| | (v) Other (please specify) | n/a |
| **2** | **Savings Accounts (Disclose for product specific types)** | |
| | (a) Required minimum opening balance | TZS 5,000 |
| | (b) Monthly service fee | TZS 1,000 |
| | (c) Interim statement | TZS 2,500 |
| | (d) Account closure | TZS 20,000 |
| **3** | **Electronic Banking** | |
| | (a) Internet banking monthly fee | n/a |
| | (b) Internet transfers | n/a |
| | (c) SMS banking | TZS 1700 |
| | (d) Other | n/a |
| **4** | **Foreign Exchange Transaction** | |
| | (a) Purchase/sale of TCs transactions over the | n/a |
| | (b) Purchase of foreign cheque | n/a |
| | (c) Sale/purchase of cash passport | n/a |
| | (d) Telegraphic transfer | n/a |
| | (e) Telex/SWIFT | n/a |
| | (f) Tranfer from foreign currency denominated account to local current account (within bank and to other bank) | 0 |
| **5** | **Personal Loans** | |
| | (a) Processing/Arrangement/Appraisal fee | 3% |
| | (i) Personal loans | 17% |
| | (ii) Overdrafts | 22% |
| | (iii) Mortgage finance | n/a |
| | (iv) Asset finance | n/a |
| | (b) Unpaid loan instalment | 20% |
| | (c) Early repayment | two months interest |
| | (d) Valuation fees | n/a |
| | (e) Other | n/a |

**Deposit Rates**

| Fixed Deposit - TZS | 3 Months | 6 Months | 12 Months |
|---|---|---|---|
| 1 - 2 Mln | 1.5% | 2.5% | 3.5% |
| 2 - 10Mln | 2.0% | 3.0% | 4.0% |
| 10 - 50 Mln | 2.5% | 3.5% | 4.5% |
| 50 - 100 Mln | 3.0% | 4.0% | 5.0% |
| 100 - 300 Mln | 3.5% | 4.5% | 5.5% |
| 300 - 500 Mln | 4.0% | 5.0% | 6.0% |
| 500m - 1Bln | 4.5% | 5.5% | 6.5% |
| Above 1 Bln | Contact Treasury | | |

| Savings Account - TZS | Accrue on Daily Cleared balance paid Monthly |
|---|---|
| 0- 50k | 0.5% |
| 50k - 1mln | 1.0% |
| 1 - 10mln | 1.5% |
| 10 - 100mln | 2.0% |
| Over 1mln | 2.5% |

**Base Lending Rates**

| | Loan Type | Base rate | |
|---|---|---|---|
| 1 | Short term (up to 1year) | 19.5% | +/-4.5% |
| 2 | Medium term (2-4 years) | 21.5% | +/-1.5% |
| 4 | Term loans (over 5 years) | 19.0% | +/-4.0% |

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| | Name | Designation | Signature | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Richard Makungwa | Chief Executive Officer | | 28 OCTOBER 2019 |
| 2 | Leticia Ndongole | Ag. Head of Business Development & Marketing | | 28 OCTOBER 2019 |
| 3 | Selemani Kijori | Head of Finance | | 28 OCTOBER 2019 |

215485102

**Head Office**

**Mlimani Tower - Mezzanine Floor,**
**Sam Nujoma Road**
**P.O.Box 61002,**
**Dar es salaam**
**Phone: 022-2772954/7**
**email: info@mcb.co.tz**
**Customer Care No.:**
**0629331151|0629331755|0800750033**


**Mlimani Branch**
**Mlimani Tower - Ground Floor**
**Sam Nujoma Road**
**Dar es salaam**

**Samora Branch**
**Samora Avenue**
**Consolidated Holding Building Ground Floor**

**Regional Office - Morogoro**
**19, Plot E, Nkomo Street**
**Phone: +255 622 005 574**
**Morogoro**

**Regional Office - Mbeya**
**90, Plot L, Sokomatola Street**
**Phone: +255 766 903 575**
**Mbeya**

**Regional Office - Mwanza**
**18, Plot A, Kirumba Street**
**Phone: +55 788 138 238**
**Mwanza**



## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### MCHANGANYIKO

**2 ACRE YARD FOR RENT**

Facing New Julius Nyerere International Airport.
Call: +255 754 375 967.
Email: gold@goldtz.net

### VIWANJA / MASHAMBA


**SHAMBA LINAUZWA**

Shamba la Ekari 13 linauzwa liko Mlandizi barabara iendayo Bagamoyo, lina miti ya matunda inayozaa, lina umeme. Lina maji ya DAWASCO na maji ni matamu. Pia kuna kisima kirefu. Kwa mawasiliano piga simu namba 0655 099825 / 0767 237404 / 0715 237404.


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**


### KUPOTEA KWA VYETI




NARRY JOHN TESHA anatangaza kupotelewa na vyeti vifuatavyo:Cheti cha kidato cha nne index namba S.3964-0059 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2011 katika Shule ya Sekondari Joyland Girls, Cheti cha kidato cha sita chenye index namba S.1757-0511 kilichoctolewa na Baraza la Mithihani la Taifa katika Shule ya Sekondari Bendel Memorial, Cheti namba 7416/T.2014 kilichotolewa na Chuo Kikuu Cha Ardhi mwaka 2018 na Cheti cha Bodi kilichotolewa na Tanzania institute of Bankers

Yeyote atakaviona atoe Taarifa kituo chochocte cha Polisi.
Polisi Taarifa: DAR/KIJ/RB/417655/2019

115483202

### KUPOTEA KWA RESULT SLIP



MAID A KASIMU MAGOTA anatangaza kupotelewa na Result Slip yenye index namba S-4260-0020 iliyotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2018 katika Shule ya Sekondari Ilowola.

Yeyote atakaeiona atoe Taarifa kituo chcochocte cha Polisi.

Polisi Taarifa:
MTW/RB/405759/2019

115483302

**Mirathi.**
**Form II**
**Citation**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Kintuku**
**Usimamizi wa Mirathi No.02 .......2019**

**Ombi la Mashala Mwandu kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu Mwandu Masanja Malesa.**

**Kwa yeyote anayehusika**

Watu wote wanaodai kuwa na mahusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo, wanaalikwa kija kuhudhuria kesi wakitaka tarehe 29/10/2019 kabla huyo muombaji hajateuliwa kuwa Msimamizi wa Mirathi hiyo. Tarehe 08/09/2019

115484602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA KILOSA**
**YAH: MAOMBI NA:202/2019**

**JOHN J.DINYA(Suing as next friend)LISPAMETHOD KIKOTI AND ANTHONY METHOD KIKOTI........MLETA MAOMBI**

**VERSUS**

MANYUSI ANTHONY KIKOTI.........1 MJIBU MAOMBI
AYUBU METHODI KIKOTI................2 MJIBU MAOMBI
COSMAS CHUWA................................ MJIBU MAOMBI

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA MANYUSI ANTHONY KIKOTI**

Popote Ulipo Unaarifiwa Ufike ktk baraza la ardhi na Nyumba la wilaya ya Kilosa,Tarehe 04/12/2019 mwenyewe binafsi au mwakilishi wako bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa.Endapo hautaudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.

Imesainiwa leo tarehe 23 Mwezi 09 Mwaka,2019.

215482802

IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO
DISTRICT AT MOROGORO
PROBATE AND ADMINISTRATION
CAUSE NO.....9.....OF 2019

In the matter of the Estate of the late...
LETTER OF ADMINISTRATION

BY 1...AMADEI KAMILI SAIDI
2..................


All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceeding if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above- named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 04 day of ....11...2019

Dated at MOROGORO this.. 24...day of ...10...2019

215482902

### KUPOTEA KWA CHETI



STEVEN G. NYAHURO anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.0784/0130 kilichotolewa na BARAZA LA MITIHANI LA TAIFA KUPITIA AIRWING HIGH SCHOOL mwaka 2016.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: DAR/CHA/RB/146181/2019.

115483801


**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0767 223311**

Distributed via ippmedia

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Tupigie 0767 223

Nipashe
MWANGA WA JAMII


**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# POCHETTINO: PENALTI YA LIVERPOOL ILIKUWA LAINI



**LONDON,** England

MAURICIO Pochettino anaamini kwamba Liverpool walipewa "penalti laini" wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Tottenham kwenye Ligi Kuu ya England, lakini akakubali maamuzi hayo.

Mchezo wa Jumapili pale kwenye dimba la Anfield ulionekana kama ungemalizika kwa sare ya bao 1-1 hadi mwamuzi, Anthony Taylor alipotoa adhabu ya penalti kwa beki wa kushoto wa Spurs, Serge Aurier kwa kumfanyia faulo, Sadio Mane ndani ya eneo la penalti.

Mohamed Salah alipiga na kufunga penalti hiyo zikiwa zimesalia dakika 15 mpira huo kumalizika baada ya Jordan Henderson kusawazisha lile la Harry Kane dakika ya 47.

Kocha wa Tottenham, Pochettino anahisi kwamba, penalti hiyo haikuwa sawa, lakini aliamua kukubali uamuzi na matokeo yake.

"Sitaki kulaumu nahitaji kukubali matokeo ya mwamuzi na VAR," alisema wakati akizungumza na waandishi wa habari.

"Kiufundi pengine ni penalti kwa sababu ilionekana kama wawili hao waligusana. Lakini kwa ukweli, mpira ulionekana kabisa umeondoka.

"Ni tukio unaloliona kwamba ni laini mno. Penalti ilitolewa na tunahitaji kukubali maamuzi ya mwamuzi na VAR."

Distributed via ippmedia

# Salah hajaumia sana, asema Klopp

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amesema kwamba majeraha ya Mohamed Salah si makubwa kama ambavyo walifikiria mwanzo baada ya kuumia kwenye mchezo wa Ligi Kuu England dhidi ya Tottenham juzi, Jumapili.

Nyota huyo wa kimataifa wa Misri alikosa wiki mbili baada ya kuumia 'enka' mwanzoni mwa Oktoba, na kumlazimu kukaa nje wakati wakitoka sare ya kufungana bao 1-1 dhidi ya Manchester United.

Salah alirudi uwanjani wakati Liverpool ikiibuka na ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya Genk kwenye Ligi ya Mabingwa Jumatano iliyopita na alianza dhidi ya Tottenham.

Hata hivyo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, alijitonesha kwenye mchezo huo wa Liverpool wakiibuba na ushindi wa mabao 2-1 na alitolewa nje na nafasi yake kuchukuliwa na Joe Gomez dakika tano kabla ya mpira kumalizika.

Virgil van Dijk pia alionekana kuumia, lakini Klopp alitoa hofu kwamba, mchezaji huyo yupo fiti.

"Virgil aliumia mguu. Alipata maaumivu kidogo, lakini atakuwa fiti," alisema akiiambia Sky Sports.

"Mo ana tatizo na 'enka' lakini hajaumia kwa kiwango kikubwa zaidi, na atakuwa fiti muda si mrefu.

"Haitakuwa vizuri kulazimika abakie uwanjani. Tuna wachezaji wengine na tuna nafasi ya kubadilisha na tulifanya hivyo.

"Hajaumia kwa kiwango kikubwa. Si kwa kiwango hicho atapona muda si mrefu, lakini naamini atarudi dimbani haraka."







# *Emery alalama kunyimwa penalti, bao*

**LONDON,** England

SIRI na hasira zimeendelea kuzunguka uamuzi wa kukataliwa kwa bao la ushindi la dakika ya 85 la Arsenal wakati wakitoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Crystal Palace juzi, Jumapili.

Gunners wanaamini walistahili ushindi kupitia bao hilo baada ya beki Sokratis Papastathopoulos kuunganisha mpira huo kimyani kufuatia kona kupigwa kabla ya kuchezwa na kurudi na kumkuta mpigaji huyo.

Baada ya kushangilia, na licha ya kutokuwapo kulalamika kutoka kwa wachezaji wa Palace, bao hilo lilikataliwa kwa madai kulikuwapo na faulo kabla ya kufungwa iliyofanywa na Calum Chambers.

Lakini marudio ya video ya bao hilo, ambayo ilionyeshwa uwanjani kwa namna yoyote ile, yanathibitisha kwamba ukweli Chambers alisukumwa na kisha kurushwa wakati wa mzozo.

Wakati Kocha wa Crystal Palace, Roy Hodgson baada ya mechi aliwaambia wanahabari "nimeona hilo sasa na kuelewa kwa nini halikukubalika". Lakini uamuzi huo ni wa kushangaa kwa Unai Emery.

"Ile haikuwa faulo," alisema Emery. "VAR ilisema ilikuwa faulo lakini niliangalia baada na ilikuwa goli.

"VAR ni chanya na tunahitaji VAR. Lakini tunahitaji kusimamia hilo katika njia sahihi."

Kocha huyo wa Arsenal, Emery alikwenda mbali zaidi kwa kuelezea namna walivyonyimwa penalti mbili dhidi ya Sheffield United Jumatatu ya wiki iliyopita.

"Ilikuwa ya kushangaza kuangalia penalti ile. Katika mechi ya mwisho hapa [Emerates] dhidi ya Bournemouth, tulistahili penalti ya wazi kabisa, ya wazi kabisa kuliko hii ya usiku huu [juzi], lakini hawakuangalia. Sawa, haikuwa muhimu katika matokeo ya mwisho kwa sababu tulishinda bao 1-0. Wiki iliyopita ugenini kwa Sheffield, tulipata penalti ya wazi kupitia kwa Sokratis wakati tukiwa 0-0. Kilikuwa kipindi kizuri lakini hawakuangalia. Tunaheshimu hilo na tulipoteza," Emery alilalama.

# Kane asema Spurs ilibweteka kwa Liver

**LONDON,** England

HARRY Kane amebainisha kwamba, Tottenham ilikosa nafasi kujijenga kutokana na ushindi wa Ligi ya Mabingwa wiki iliyopita, wakati walipokubali kipigo cha mabao 2-1 kutoka kwa Liverpool.

Baada ya nahodha huyo wa England kuwapa bao la kuongoza Spurs sekunde ya 47 katika mchezo huo, alishuhudia mabao mawili ya kipindi cha pili kutoka kwa Jordan Henderson na Mohamed Salah.

Spurs waliingia kwenye mchezo huo wakitoka kupata ushindi wa mabao 5-0 dhidi ya Red Star Belgrade kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku kocha Mauricio Pochettino akielezea kiwango hicho kuwa bora zaidi kwa mechi zao zinazokuja.

Kane sasa anaona kwamba, Spurs walishindwa kuendeleza kile walichokifanya kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, na hivyo kujikuta wakipoteza pale Anfield.

Akizungumzia kipigo hicho, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, aliiambia Sky Sports: "Uliona jinsi tulivyooanza mchezo: tulikuja na nia ya kusukumiza mbele mashambulizi, kucheza na kusaidia kupata mabao. Lakini ni kama tulibweteka tu.

"Tulijaribu kufanya kila kitu kushinda mchezo na tulishindwa kwenda kwenye njia yetu. Inaumiza, lakini ni ngumu kunyoosha kidole kwa sasa.

"Wakati wowote unapopoteza mchezo, si ishara nzuri kwa mchezo unaokuja mbele yetu. Inakatisha tamaa. Tunataka kuchukua timu yetu ifanye vizuri kwenye Ligi Kuu. Bado hatujafanya vizuri vya kutosha.

"Tunachoweza kufanya kwa sasa ni kuangalia mbele mchezo wetu dhidi ya Everton wiki ijayo."



# MAN UTD TIMU YA KWANZA KUFUNGA MABAO 2,000



Distributed via ippmedia

**LONDOND,** England

KLABU ya Manchester United imekuwa timu ya kwanza kufunga mabao 2,000 kwenye Ligi Kuu ya England, wakati Scott McTominay alipofunga dhidi ya Norwich City, juzi Jumapili.

Kiungo huyo mwenye umri wa miaka 22, zao kutoka kwenye akademi ya United, alifunga kwa shuti lililompita Tim Krul kuwafanya 'Mashetani Wekundu' hao kuwa mbele kwa bao 1-0, mchezo uliopigwa pale kwenye dimba la Carrow Road katika dakika ya 21 kbala ya kushinda 3-1.

Arsenal ni ya pili kwa kufikisha mabao 1,860, huku Liverpool ikiwa na mabao 1,795 na Chelsea mabao 1,793 wakiwa nafasi ya tatu na nne.

Mark Hughes alifunga bao la kwanza la United kwenye Ligi Kuu ya England baada ya maboresho Agosti 15, mwaka 1992, wakati United ikiibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Sheffield United.

Cristiano Ronaldo alifikisha bao la 1,000 kwa Mashetani Wekundu hao wakati alipofunga la kufutia machozi wakiwa wamechapwa mabao 4-1 na Middlesbrough Oktoba mwaka 2015.

# *Xhaka kawakosea mashabiki - Emery*

**LONDON,** England

UNAI Emery amesema Granit Xhaka alikosea 'kuwajibu' mashabiki wa Arsenal waliokuwa wanamzomea wakati timu hiyo ikitoka sare ya kufungana mabao 2-2 na Crystal Palace, juzi Jumapili.


Nahodha wa 'Washika Bunduki' hao wa London, alionyesha ishara ya kushika masikio kama hasikii vizuri mashabiki walivyokuwa wakimzomea wakati alipotolewa nje, kabla ya kuvua jezi na kuelekea vyumba vya kubadilishia nguo.

Arsenal walikuwa na mabao ya awali kupitia kwa Sokratis Papastathopoulos na David Luiz, huku Luka Milivojevic na Jordan Ayew wakisawazisha na kuihakikishia pointi moja Palace.

Akizungumzia kitendo cha Xhaka baada ya mchezo huo, Emery aliiambia BBC: "Alikosea. Alikosea, lakini tutakwenda kuzungumza zaidi kuhusu hali hii. Nilikuwa wa kwanza kumsikiliza yeye na kuwa mtulivu, lakini kwa uhakika alikosea kwa kufanya tukio hilo."

Aliwaambia waandishi wa habari: "Tupo hapa kwa ajili ya mashabiki. Tunafanya kazi kwa ajili yao na unahitaji kuwaheshimu kwa sababu ni jukumu lao kutushutumu."

Wakati alipoulizwa kama Xhaka atabaki kuwa nahodha, Emery alisema: "Sasa si muda wa kuzungumza kuhusu hilo.



# DONDOO SOKA
## MAGAZETI Y AYA




Distributed via ippmedia

# POGBA SASA NJE HADI DESEMBA - SOLSKJAER

## Ni enka badala ya mguu, anahitaji muda kuwa fiti kabisa, sidhani kama atarejea kabla...

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer ameweka wazi kuwa kiungo Paul Pogba anajiandaa kuwa nje ya uwanja hadi Desemba mwaka huu akiuguza majeraha ya kifundo cha mguu ['enka'].

Nyota huyo wa United alipatwa na jeraha hilo katika mechi dhidi ya Southampton Agosti 31, mwaka huu na ilionekana kulizidisha baada ya kucheza mara mbili aliporejea.

Pogba hajacheza tena tangu walipotoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Arsenal Septemba 30 na Solskjaer hategemei kurudi kwake kwa mwezi ujao.

**"Sidhani kwamba tutamuona labda kabla ya Desemba," Solskjaer aliwaambia wanahabari. "Atakuwa nje kwa muda.**

"Anahitaji muda kuwa fiti kabisa, kuimarika kabisa, hivyo sidhani kama atarejea.

"Pengine dhidi ya Sheffield United [Novemba 24] baada ya mapumziko ya mechi za kimataifa, lakini labda Desemba kabla ya kuweza kumuona.

"Ni enka badala ya mguu. Mimi si daktari lakini kuna majeraha pale ambayo yanahitaji uponyaji."

Pogba, ambaye amekuwa akihusishwa na kutua LaLiga kuitumikia Real Madrid na Serie A kwa mabingwa Juventus, amecheza mechi tano za Ligi Kuu msimu huu bila kuifungia bao United.

Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 26, kwa ujumla msimu huu katika mashindano yote amecheza mechi sita wakati huu United ikiwa nafasi ya saba kwenye Ligi Kuu England na ikiwa katika michuano ya Europa League na Kombe la Ligi (EFL Cup).

## ZISIKUPITE

### UNITED KUJITOSA KWA SANCHO

MANCHESTER United inajiandaa kufika dau inalohitaji Borussia Dortmund wakati ikijaribu kumsajili mshambuliaji Muingereza Jadon Sancho. Klabu hiyo ya Ujerumani inaweza kuhitaji takriban pauni milioni 100 kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19. ***(Mirror)***

### COUTINHO: BUNDESLIGA NGUMU

PHILIPPE Coutinho amekiri Bundesliga ni ligi 'ngumu' kuweza kuchomoza, lakini amesisitiza ni mwenye furaha kwa vyote na kiwango chake. ***(Daily Mirror)***

### LACAZETTE AMGUSA EMERY

ALEXANDRE Lacazette amelipenda chapisho la Instagram lililomkosoa Kocha wa Arsenal, Unai Emery na nahodha wa klabu hiyo, Granit Xhaka baada ya sare ya bao 2-2 dhidi ya Crystal Palace. ***(Daily Mail)***

### NEWCASTLE KUMFUATA JAMES

KOCHA wa Newcastle, Steve Bruce anapanga kwenda kumsajili kwa mkopo beki wa Chelsea na England U-20, Reece James, 19. ***(Sun)***

### MBAPPE BADO LULU REAL

KURUDI kwa wachezaji wa Real Madrid wanaocheza kwa mkopo, akiwamo Dani Ceballos, 23, aliyepo Arsenal, kunaweza kuongeza nafasi yao ya kutoa ofa kwa mshambuliaji wa Paris St-Germain, Kylian Mbappe. ***(AS)***

### RAKITIC AKARIBISHA OFA

KIUNGO wa Croatia, Ivan Rakitic, 31, amekaribisha "ofa" kuelekea dirisha la usajili la Januari na Manchester United na Juventus wakimfuatilia. ***(Marca)***

### BALLON D'OR YA MANE - DROGBA

DIDIER Drogba amemuunga mkono Sadio Mane kushinda tuzo ya Mwaka ya Ballon d'Or na anatumai winga huyo Msenegal atakuwa mchezaji wa pili kutoka Afrika kutwaa tuzo hiyo. ***(Daily Mail)***

### BALOTELLI KUIGHARIMU BRESCIA

MPIGAPICHA anapanga kutuma bili ya kuvungwa kwa kamera yake kwa Brescia, baada ya nyota huyo wa zamani wa Liverpool na Manchester City, Mario Balotelli, 29, kuipiga teke kufuatia kitendo cha kukerwa na mabadilo ['kufanyiwa sab']. ***(Sun)***

### IBRAHIMOVIC ATAKIWA NAPOLI

RAIS wa Napoli, Aurelio de Laurentiis amesema anavutiwa kumsajili Zlatan Ibrahimovic, 38, ambaye atakuwa mchezaji huru dirisha dogo la usajili la Januari mkataba wake na LA Galaxy utakapomalizika. ***(ESPN)***

### SCHOLES AMVUTA OZIL UNITED

PAUL Scholes anaamini klabu yake ya zamani, Manchester United inapaswa kujaribu kumsajili kiungo asiyekubalika Arsenal, Mjerumani Mesut Ozil, 31, ili saidie kutatua matatizo katika safu yao ya ushambuliaji. ***(BT Sport, via Evening Standard)***

### WERNER MTEGONI CHELSEA

CHELSEA imeongeza kujiamini kwamba kufungiwa kwa klabu hiyo kusajili kutafutwa na inatazama uwezekano wa kumsajili mshambuliaji wa Bournemouth na England, Callum Wilson, 27, na straika wa RB Leipzig, Mjerumani Timo Werner, 23. ***(Sun)***

HABARI MICHEZO

## Azam waimulika Kagera Sugar

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Klabu ya Azam FC umesema kwa sasa wanaendelea kuzivutia pumzi timu zilizopo mbele yao baada ya kufungwa bao 1-0 na Ruvu Shooting juzi, Jumapili ikiwa ni siku chache kabla ya kupoteza kwa idadi hiyo dhidi ya Simba.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Kocha msaidizi wa timu hiyo, Idd Cheche alisema vijana wake walipata nafasi nyingi za wazi, lakini walishindwa kuzitumia.

"Wachezaji wetu walishindwa kutumia nafasi, wenzetu wakazitumia wakapata bao," alisema Cheche.

Alisema watayafanyia kazi makosa machache yaliyojitokeza ili yasijirudie kwenye michezo ijayo ya Ligi Kuu hususan mechi inayofuata ya Novemba 4, mwaka huu dhidi ya Kagera Sugar.

Alisema licha ya kuwapo kwa ushindani mkubwa, akili yao ni kuendelea kushika nafasi ya juu katika msimamo wa Ligi Kuu wakati huu wakiwa nafasi ya nane na pointi tisa baada ya kushuka dimbani mara tano.

## Taliss-IST bingwa Taifa kuogelea

**Na Mwandishi Wetu**

KLABU ya Taliss-IST imeshinda ubingwa wa mashindano ya wazi ya kuogelea baada ya kukusanya pointi nyingi zaidi ya timu nyingine saba.

Katika mashindano hayo yaliyofanyika kwenye Bwawa la Kisasa la Shule ya Kimataifa ya Tanganyika (IST) Masaki, klabu hiyo ilikusanya jumla ya pointi 2,207.

Klabu ya Bluefins chini ya kocha na mwasisi, Rahim Alidina ishika nafasi ya pili kwa kupata pointi 1,281 wakati Klabu ya Morogoro, Mis Piranhas ikishika nafasi ya tatu kwa kupata pointi 830.

Klabu ya Dar es Salaam Swimming Club (DSC) ilimaliza katika nafasi ya nne kwa kupata pointi 750. Waogeleaji wa kike wa klabu hiyo walikusanya pointi 373 huku wanaume wakijikusanyia pointi 377.

Nafasi ya tano ilikwenda Mwanza ambao walipata pointi 468, huku FK Blue Marlins ikishika nafasi ya sita kwa kupata pointi 429 na Uwcea Moshi Kilimanjaro ikikusanya pointi 325 na Champion Rise katika nafasi ya nane kwa kupata pointi 244.

Meneja wa timu ya Taliss-IST, Hadija Shebe aliwapongeza waogeleaji wake kwa ushindi huo akisema: "Ushindi huu ni faraja kwetu na umetokana na juhudi na ushirikiano baina ya makocha, wazazi, wadau na waogeleaji kwa ujumla."

# YANGA NI TSHISHIMBI NA FEITOTO TU- PYRAMIDS

**Na Somoe Ng'itu,** MWANZA

LICHA ya timu yake kupata ushindi wa mabao 2-1 katika mchezo wa kwanza wa mechi ya mchujo ya kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika, Kocha Mkuu wa Pyramids, Sebastien Desabre, amesema wachezaji wawili wa Yanga waliowasumbua ni viungo, Feisal Salum "Feitoto" na nahodha Papy Tshishimbi pekee.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Desabre, alisema Feitoto na Tshishimbi walicheza katika kiwango kizuri na walikuwa na mashambulizi ya hatari katika mchezo huo ambao mshindi wa jumla atatinga hatua ya makundi ya michuano hiyo inayofanyika kila mwaka barani Afrika.**

Desabre alisema pamoja na kupata ushindi katika mechi hiyo, bado ana kibarua cha kwenda kumalizia kazi nyumbani waliyoianza ugenini katika Uwanja wa CCM Kirumba.

"Ilikuwa ni mechi ngumu, uwanja haukuwa rafiki kwa wachezaji kuonyesha soka maridhawa, lakini hiki ni kipindi cha kwanza kimemalizika, kuna dakika nyingine 90 tutakazocheza baada ya wiki moja, tutaenda kujipanga vizuri zaidi kuhakikisha tunashinda na kusonga mbele," alisema Desabre.

Mfaransa huyo alisema pia Yanga ni timu nzuri na kwa kufahamu hivyo, hawatabweteka na ushindi walioupata katika mchezo wa juzi, ambao umewaweka mguu mmoja ndani kuelekea hatua ya makundi.

Kwa upande wa Kocha Msaidizi wa Yanga, Noel Mwandila, alisema kikosi chao kina nafasi ya kusonga mbele katika mashindano hayo, kwa sababu wanaweza kupata ushindi kwenye mchezo wa marudiano.

Hata hivyo, Mwandila alisema mwamuzi wa mchezo huo hakutenda haki kwa upande wao na kuhitaja kadi ya kwanza ya njano aliyoonyeshwa Kelvin Yondani haikuwa sahihi na hivyo, jana hakustahili kuonyeshwa kadi nyekundu.

"Mwamuzi hakutenda haki, kadi ya kwanza aliyoonyeshwa Yondani haikuwa halali, ila ile ya pili ilikuwa sahihi, maana yule mchezaji aliyemfanyia faulo alikuwa anaelekea kufunga, hii si sawa," alisema Mzambia huyo kwa niaba ya Kocha Mkuu, Mwinyi Zahera, ambaye aligoma kuzungumza na waandishi wa habari.

Kocha huyo aliongeza kuwa mashabiki wa Yanga hawatakiwi kukata tamaa baada ya kupoteza mchezo huo, kwa sababu katika mchezo wa soka lolote linaweza kutokea nyumbani au ugenini.

"Tuna nafasi, muda wa kurekebisha makosa tunao, tutayasahihisha na kujipanga upya kwa ajili ya mchezo wa marudiano, tumeshawajua kwa karibu, wanafungika," Mwandila alisema.

Kikosi cha Yanga kiliondoka jijini hapa jana na kurejea Dar es Salaam tayari kuanza maandalizi ya mchezo wa marudiano unaotarajiwa kuchezwa nchini Misri Jumapili wiki hii.



Beki wa Yanga, Mapinduzi Balama, akitoa kashikashi kwa kiungo wa Pyramids, Mohammed Fathi (kulia) wakati wa mechi ya mchujo kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa Uwanja wa CCM Kirumba mwishoni mwa wiki. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

## 'Simba isisingizie uwanja ushindi kiduchu'

**Na Focus Nicus**

LICHA ya kukubali kipigo cha bao 1-0 walichokipata juzi katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha, Kocha wa Singida United, Ramadhani Nsanzuryimo, ameitaka klabu ya Simba kuacha kusingizia ubovu wa uwanja kutokana na matokeo finyu waliyoyapata.

Bao pekee la dakika ya 42 kupitia kwa Miraji Athumani, ndilo lililoizamisha Singida United ambayo inatumia Uwanja wa Sheikh Amri Abeid kama dimba lake la nyumbani kufuatia Bodi ya Ligi kuufungia Uwanja wa Namfua mkoani Singida kutokana na kukosa ubora eneo la kuchezea.

Baada ya mechi hiyo Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu alisema moja ya mambo yaliyochangia timu yao kushindwa kuibuka na ushindi mnono ni pamoja na ubovu wa uwanja kwa kuwa walishindwa kucheza soka lao la pasi za chini.

"Tunashukuru tumepata ushindi kwa kuwa cha muhimu ni pointi tatu, lakini uwanja haukuwa rafiki kutokana na kutokuwa na ubora eneo la kuchezea hivyo tulishindwa kucheza pasi zetu za chini," alisema.

Hata hivyo, Nsanzuryimo alisema kikosi chake kilicheza vizuri na kuidhibiti Simba kucheza soka lao na kwamba si suala la uwanja bali waliwakamata.

"Kama uliangalia nadhani uliona namna tulivyocheza, hapa si suala la uwanja kwani ina maana sisi tulicheza uwanja tofauti na wao? Pamoja na uwanja kutokuwa bora lakini wote tulicheza hapo, hivyo hapa ni suala la kuwadhibiti," Nsanzuryimo alisema. "Simba ni timu bora na iliyoandaliwa vizuri, huwezi kuilinganisha na Singida, lakini kwa ujumla vijana wangu walicheza vizuri na tunaendelea kuijenga timu."

Hiyo ni mara ya tano Simba na Singida United zinakutana na mara zote Wekundu wa Msimbazi hao wameshinda.

Simba iliyopo kileleni mwa ligi hiyo, itashuka tena dimbani kesho, Jumatano Katika Uwanja wa Kambarage mjini Shinyanga kuivaa Mwadui FC wakati siku hiyo Singida United ikiwa mwenyeji wa JKT Tanzania hapo Sheikh Amri Abeid.

Michezo
Jumanne Oktoba 29, 2019
Nipashe



Pogba sasa nje hadi Desemba - Solskjaer

UKURASA 30

# YANGA: MSIMAMO HATIMA YA ZAHERA HUU

## ●●● Moto wawaka kuanzia Kirumba hadi Dar, Kocha Pyramids awataja Feitoto, Tshishimbi kuwa...

**Na Somoe Ng'itu,** MWANZA

WAKATI kikosi cha Yanga kikitarajia kuondoka nchini keshokutwa, Alhamisi kuelekea Misri kwa ajili ya mchezo wa marudiano dhidi ya Pyramids FC, uongozi wa klabu hiyo umesema kwa sasa haujafanya uamuzi wowote kuhusiana na hatima ya Kocha Mkuu, Mwinyi Zahera, ambaye mashabiki wa timu hiyo walipaza sauti juzi wakitaka atimuliwe.

**Yanga iliyokuwa jijini hapa ikiwakabili Pyramids katika mchezo wa kwanza wa mchujo kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika na kukubali kipigo cha mabao 2-1, ilirejea jijini Dar es Salaam jana asubuhi na kuwapa wachezaji wake mapumziko ya siku moja.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela, alisema uongozi ulisikia "kilio" cha mashabiki wao, lakini uamuzi wa kuachana na Zahera, bado haujatolewa.

Mwakalebela alisema kuwa matokeo ya mchezo wa juzi yaliwaumiza wengi, lakini uongozi unasubiri ripoti ya kiufundi ambayo ndio itatoa mwongozo wa hatima ya kocha huyo ambaye juzi alitupiwa chupa za maji na mashabiki wa timu hiyo baada ya kushuhudia wakipoteza mechi dhidi ya Pyramids kwenye Uwanja wa CCM Kirumba.

"Hakuna uamuzi wowote ambao tumeufanya kuhusu Zahera, hatukuwa na nguvu ya kufanya kikao chochote baada ya mechi, na tayari muda huu (jana saa 5:20 asubuhi) tumeshafika Dar es Salaam, nami niko klabuni kwa ajili ya kuanza maandalizi ya safari," alisema Mwakalebela.

Mbali ya mashabiki wa Yanga katika Uwanja wa CCM Kirumba waliokuwa wakiimba Zahera aondoke, shabiki wa Yanga kutoka Mbezi jijini Dar es Salaam, Mshamu John aliyekuwapo uwanjani hapo, alisema haridhishwi na kiwango cha Zahera, na anautaka uongozi wa klabu hiyo uachane naye kwa sababu anaipeleka "shimoni" timu yao.

"Nilijua tunashinda kabisa hii mechi, lakini nilichokishuhudia ni maumivu, tumetumia fedha nyingi kufika Mwanza, tumewekeana ahadi kibao huko nyumbani (Dar es Salaam), Zahera hatufai, anapanga wachezaji wake, timu haichezi, yaani tulikuwa kama tuko ugenini, aende tu, atuachie timu yetu," alisema shabiki huyo lakini moto huo ukiendelea kufukuta kwa mashabiki wa timu hiyo ndani ya viunga vya Jiji la Dar es Salaam.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli, aliliambia gazeti hili kuwa kikosi chao kilifika Dar es Salaam salama na kesho kitaanza mazoezi ya kujiandaa na mechi ya marudiano inayotarajiwa kuchezwa Jumapili jijini Cairo.

"Timu imeshafika Dar es Salaam salama, leo (jana) tumewapa mapumziko wachezaji wetu, kesho (leo), wataanza mazoezi rasmi kwa ajili ya mchezo wetu wa marudiano, maandalizi ya safari yako katika hatua za mwisho, tunatarajia kikosi chetu kitaondoka nchini kwenda Misri Oktoba 31," alisema Bumbuli.


Aliongeza kuwa matokeo ya mchezo wa juzi hayajawakatisha tamaa, wanajipanga zaidi kwa ajili ya mchezo wa marudiano ambao wanaweza kuwashangaza wenyeji wao kwa kuwaondoa katika michuano hiyo.

"Tuna dakika nyingine 90 zimebaki, hakuna ambaye ameshafuzu, tunafanya kama tulichofanya Botswana, tuko tayari kwenda kupambana kwenye Uwanja Juni 30, kitaeleweka hapo hapo Cairo," aliongeza ofisa huyo.

Baada ya kutoka Misri, Yanga yenye pointi saba kwenye Ligi Kuu Bara na iliyocheza mechi nne itasafiri kwenda Mbeya kuwafuata Mbeya City na Tanzania Prisons katika michezo miwili ya ligi hiyo ambayo mabingwa watetezi Simba wakiwa kileleni kufuatia ushindi wa mechi zote sita walizocheza.

Katika hatua nyingine, Kocha Mkuu wa Pyramids, Sebastien Desabre, ameondoka na majina ya wachezaji wawili wa Yanga ambao inaaminika atakwenda kuandaa mikakati ya kuwakaba vilivyo kwenye mechi ya marudiano baada ya kueleza walikuwa tishio kwao. Katika mechi hiyo, Desabre aliwataja viungo, Feisal Salum "Feitoto" na nahodha Papy Tshishimbi kwa walikuwa hatari kwao kutokana na kusukuma mashambulizi mbele ikiwa ni pamoja na kuisumbua safu yao ya ulinzi.

TULIAGA...



Kiungo wa Arsenal, Matteo Guendouzi akimchezea madhambi mshambuliaji wa Crystal Palace, Wilfried Zaha nje ya 18 wakati wa mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa kwenye Uwanja wa Emirates juzi na kumalizika kwa sare ya mabao 2-2. **HABARI UK. 28**

## Maajabu mabao ya Miraji Simba

**Na Adam Fungamwango**

WINGA mpya machachari wa Simba Miraji Athumani ameendeleza moto wake akiwa na kikosi hicho kwa kufunga bao la nne msimu huu wakati wakiikwanyua Singida United 1-0 kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha juzi, rekodi zikionyesha kuwa kila anapofunga hakuna tena ongezeko la bao lingine kwa timu yake.

Aidha, Miraji pia kila anapofunga basi timu yake huondoka na ushindi kwenye mechi husika tangu kuanza kwa msimu huu.

Kwa mujibu rekodi zetu, mchezaji huyo anapofunga basi biashara inakuwa imeishia hapo na kinachofuata ni Simba tu kuanza kusherehekea ushindi kwani haipotezi wala kuongeza bao lingine na ni mara moja tu, wapinzani wakifunga goli la kufutia machozi.

Maajabu ya mabao ya Miraji yalianza kwenye mechi ya kwanza ya Ligi Kuu ambayo Simba ilicheza dhidi ya JKT Tanzania kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Ilikuwa ni Agosti 29, Simba ilipoichapa JKT Tanzania mabao 3-1, Miraji alifunga bao la tatu dakika ya 62. Simba haikufunga tena bao, ingawa JKT Tanzania ilipata bao la kufutia machozi dakika ya 87.

Mechi nyingine ilikuwa ni Septemba 13, mwaka huu kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, Miraji alipofunga bao la pili dakika ya 69 dhidi ya Mtibwa Sugar. Baada ya hapo hakuna bao lolote lililofungwa kwenye mechi hiyo Simba ikishinda mabao 2-1.

Kwenye mechi dhidi ya Biashara United iliyochezwa Septemba 29, Simba ikishinda mabao 2-0 kwenye Uwanja wa Karume mjini Musoma, Miraji alifunga bao la pili dakika ya 53 na baada ya hapo timu yake haikuongeza wala kuruhusu bao lolote.

Jumapili iliyopita kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha, Miraji alifunga bao dakika ya 41 na si Simba yenyewe iliyoongeza wala Singida iliyopata bao baada ya hapo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042